

**M A P**

Mapinduzi Yako ya Kifedha

**NGUVU YA KUPUMZIKA**

**I N D**

**GARY KEESEE**

**U Z I**

**M A P**

Mapinduzi Yako ya Kifedha

**NGUVU YA KUPUMZIKA**

**I N D**

**GARY KEESEE**

**U Z I**

**Your Financial Revolution**

*Power of Rest*, Kiswahili By Gary Keese

© Gary Keese, 2022

Originally published in English

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

You can reach Faith Life Now Ministries on the Internet at

FaithLifeNow.com

**Mapinduzi yako ya Kifedha**

*Nguvu ya Kupumzika*, Kiswahili na Gary Keese

© Gary Keese, 2022

Awali kilichapishwa katika lugha ya Kiingereza

ISBN: 978-1-945930-03-4

Faith Life Now

P.O. Box 779

New Albany, OH 43054, USA

Unaweza kufikia Faith Life Now Ministries kwenye mtandao kupitia

FaithLifeNow.com

Nataka kuweka wakfu kitabu hiki kwa mke wangu, Drenda, kwa sababu ni kutia moyo kwake, shauku yake ya mambo ya Mungu, na upendo wake kwangu na kwa familia yetu ambavyo vimenitia moyo kwa miaka hii yote. Pamoja tumethibitisha kwamba ndoto kweli hutimia!

Gary Keesee



# YALIYOMO

<b>UTANGULIZI</b> .....	ix
<b>SURA YA 1:</b> Pumziko – Jambo La Kimsingi .....	1
<b>SURA YA 2:</b> Haki Za Kisheria .....	13
<b>SURA YA 3:</b> Ufalme Ndio Jibu Lako .....	29
<b>SURA YA 4:</b> Samaki Mkubwa .....	45
<b>SURA YA 5:</b> Kusafiri Kwa Ndege Ni Bora Kuliko Kutembea .....	55
<b>SURA YA 6:</b> Kuna Mengi Ya Ziada Maishani Kuliko Kulipa Bili! .....	71
<b>SURA YA 7:</b> Hili Haliwezekani .....	81
<b>SURA YA 8:</b> Sehemu Maradufu .....	91
<b>SURA YA 9:</b> Zaidi Ya Kutosha .....	103
<b>SURA YA 10:</b> Siri Ya Sehemu Maradufu .....	121



# UTANGULIZI

Siku tulipotoka huko mashambani ilikuwa siku yenye huzuni na furaha. Tulikuwa tumeishi katika nyumba hiyo ndogo, nzee, na iliyokuwa imeharibika kwa karibu miaka tisa, na sasa nilikuwa ninabeba mizigo ya mwisho kwenda kwa gari letu. Nilikuwa ninaelekea kwa nyumba yetu mpya tuliyokuwa tumejijengea wenyewe, nyumba ya Kigeorgia iliyokuwa na futi za mraba 7,700, kwenye ekari 55 za mashamba ya kifahari ya Ohio, na yenye ekari 20 za misitu na mabwawa. Ilikuwa ndoto ambayo ingekuwa ngumu kufikiria miaka michache awali.

Ingawa tulikuwa tukiondoka pale mashambani, niliipenda nyumba hiyo kuukuu. Naam, hata kama ilikuwa na madirisha yaliyovunjika, chumba kichafu cha kuhifadhi vitu, na mashambulizi ya mara kwa mara ya nyuki tuliyovumilia tulipokuwa tukiishi huko. Kumbukumbu nyingi zilikuja akilini. Watoto wangu wawili kati ya watano walizaliwa pale pale.

Tulikuwa na nyakati nyingi nzuri huko lakini pia nyakati nyingi za mashinikizo ya kifedha na kukata tamaa. Kulikuwa na mambo mengi tuliyopaswa kujifunza. Ijapokuwa ni vigumu kuwaza kuhusu hayo sasa, tulipohamia nyumba hiyo nzee ya mashambani miaka tisa awali, hatukuwa na uwezo wa kulipa kodi ya \$300 kwa mwezi. Magari yetu yote mawili yalikuwa yamechakaa, maana tulikuwa tumeyatumia kwa mamia ya maelfu ya maili, na haki yangu ya kuyamiliki ilikuwa karibu kuchukuliwa. Wakati huo, ilionekana kana kwamba kila mtu alitudai pesa. Tulikuwa na kadi kumi za mkopo zilizokuwa zimeghairiwa kwa sababu ya kutumika kupita kiasi; mikopo kutoka kwa kampuni mbili; malipo yetu ya gari mbili; kunyakuliwa kwa haki ya umiliki na shirika la kulipa ushuru; makumi ya maelfu tuliyodaiwa na jamaa zetu; na orodha inaendelea. Tuliishi maisha ya manusuru kifedha, huku tukiweka rehani kwa kila kitu tulichokimiliki



wakati mwingine ili kununua chakula tu. Vitu tulivyomiliki vilikuwa vizee sana, vilikuwa vimeharibika maana tulivinunua vikiwa vimetumika tayari.

Hali yetu mbaya ya kifedha wakati huo haikuwa na matumaini hata kidogo ya kuwa na siku nzuri usoni. Kusema kweli, sikuwa na matumaini mengi kwamba mambo yangeweza kubadilika. Niliipenda familia yangu, nilikuwa na mke mwema, lakini nilikuwa ninawapitisha kuzimu ilipohusu suala la kifedha!

Nilikuwa nikinywa dawa za kupunguza mafadhaiko, ili kukabiliana na mashambulizi ya hofu ambayo yalikuwa yamenitawala kila siku maishani mwangu. Acha tuseme kwamba sikuwa mtu mzuri wa kukaa karibu naye. Nilikuwa nauza bima ya maisha, huku nikitumia kamisheni niliyolipwa kukidhi mahitaji, wala sikuwa nikienda mahali popote kwa haraka, isipokuwa katika janga la kifedha zaidi na zaidi. Polepole tulizidi kuingia katika madeni hadi hatukuwa na njia nyingine ya kukopa. Hapa ndipo nilipohisi kwamba nimeangamia. Hofu na wasiwasi ziliniingia akilini. Niliogopa hata kuondoka nyumbani kwangu, ambalo si jambo nzuri ikiwa unafanya kazi ya uuzaji na kulipwa kamisheni.

Mke wangu alifikiri angempe-teza mume wake, na hofu ya kulea watoto wanne tuliokuwa nao wakati huo peke yake ilimsononesha. Laki-ni

**TULIPOANZA KUMTAFUTA  
MUNGU ILI KUPATA MAJIBU  
NA KUELEWA KANUNI,  
TUMAINI LILIANZA  
KUONGEZEKA MIOYONI  
MWETU MAANA TULIONA  
MUUJIZA MMOJA BAADA  
YA MWINGINE WAKATI  
TULIPOTUMIA YALE AMBAYO  
MUNGU ALITUONYESHA.**

yeye ni muumini mkubwa wa nguvu ya maombi na hakukata tamaa kunihusu. Pamoja tuliomba kisha tukaanza kutafuta kanuni za Ufalme wa Mungu. Tulipoanza kumtafuta Mungu ili kupata majibu na kuele-wa kanuni, tumaini lilianza kuongezeka mioyoni mwetu maana tuliona muujiza mmoja baada ya mwingine wakati tulipotumia yale ambayo Mungu alituonyesha.

Wakati mwafaka ulifika usiku mmoja ambapo Mungu alinionyeshwa kwamba nilipaswa kuanzisha kampuni yangu katika nyanja ya kifedha

kusaidia watu kutoka kwa madeni na kuwafundisha kanuni alizokuwa akinionyeshwa. Wakati huo, kuanzisha kampuni iliyoonyesha watu jinsi ya kutoka kwa madeni lilionekana kuwa jambo la kushangaza maana sisi wenyewe bado tulikuwa na madeni mengi. Tuliomba kuhusu jambo hilo, lakini Bwana akatuambia kwamba tulipotoka na kuanza kufundisha kanuni

Zake, tungepata uhuru wetu pia. Ilikuwa safari ya imani kuanzisha kampuni kwa sababu hatukujua jinsi ya kufanya hivyo, lakini tulistahimili. Kampuni ilikua, na pesa ilizoleta zilitoa familia yetu kwa madeni kabisa katika miaka miwili na nusu. Nitazungumza zaidi juu ya kampuni yetu katika sura inayofuata, lakini kwa sasa, fahamu tu kwamba maisha yetu yalibadilika sana! Hakuna jinsi ninavyoweza kueleza tulivyohisi kuwa huru, jinsi tulivyohisi kuingia kwenye duka la magari na kulipia gari jipya pesa taslimu. Jinsi tulivyohisi kubuni, kujenga, na kulipia nyumba yetu mpya. Kile tulichokuwa tukifurahia kilikuwa zaidi ya chochote tulichoweza kufikiria.

Naam, nyumba ile ya mashambani ilikuwa na kumbukumbu kadhaa. Nilipoenda kuchukua sanduku la mwisho kutoka nyumbani, nilimpita mke wangu akiwa amesimama kwenye kile chumba chetu kidogo cha kulia. Alinitazama huku machozi yakimtoka. Hayakuwa machozi ya huzuni bali machozi ya furaha na pia ya hisia alipokumbuka yote ambayo Mungu alikuwa ametufundisha pale. Nilipigana na machozi pia nilipotazama kwa mara ya mwisho vyumba vyote, huku nikikumbuka kwa hisia zilizochanganyika kila kitu kilichofanyika humo. Tulikuwa tunafunga msimu mmoja wa maisha na kwenda kwenye eneo jipya. Nini kilikuwa mbele yetu sasa? Safari yetu ilikuwa imetupeleka katika mahali pa huzuni na kukosa tumaini, kisha katika mahali palipojaa matumaini. Nilipokuwa nikitoka nje na sanduku la mwisho, nilisimama na kutazama nyuma kwa nyumba huku nikitabasamu. “La, sitakukosa. Nina mahali pazuri zaidi sasa.”

Bila shaka kuhamia nyumba yetu mpya lilikuwa jambo la kusisimua. Lakini jambo bora zaidi kuhusu safari yetu ni kwamba hatimaye tulipata pumziko! Ningeweza sasa kufikiria kuhusu maisha yangu ya baadaye wala sio kuhusu kulipa bili tu. Kuishi katika pumziko Lake katika miaka mingi kumekuwa kama ndoto iliyotimia kabisa! Kuwa na magari yaliyolipiwa ni pumziko. Kutokuwa na madeni ni pumziko. Kuwa na nyumba ya ndoto yangu kwenye ekari 55 zilizolipiwa ni pumziko. Kuona tabasamu kwa uso wa mke wangu anapoenda madukani bila wasiwasi juu ya pesa ni pumziko. Zaidi ya kuwa na kila kitu tunachohitaji, kuwa na pesa za kutosha kuweza kutoa mamia ya maelfu ya dola kwa wengine ili kusaidia katika kazi ya Injili ni pumziko. Lakini pengine badiliko kubwa zaidi maishani mwangu lilikuwa kutoamka kila siku nikiwa na shinikizo na hofu ambayo ilikuwa imezunguka maisha yangu yote katika ile miaka ya mwanzoni. Kuwa na uwezo wa kuota mambo mazuri tena badala ya kuota jinsi ya kuweza kuishi wiki moja zaidi ni pumziko.

Ndio, siku nilipokuwa nikipakia mizigo ya mwisho kwenye gari ili kwenda kwa nyumba yetu mpya ilikuwa ya huzuni na furaha. Lakini niamini, furaha ya pumziko tuliyoigundua mimi na Drenda ilipita mawazo machungu ya kuziacha kumbukumbu za ile nyumba ya mashambani kiasi kwamba tulijihisi kama watoto wawili wadogo wa umri wa kwenda shule tena, tulichekacheka na kuota pamoja.

Najua unachofikiria. Laiti ingekuwa mimi. Laiti jambo kama hilo lingenifanyikia ili niweze kucheka, kuota, na kuweza kuzingatia kitu kingine ila kulipa bili tu. Ingawa sasa hivi unaweza kuona ni vigumu kuamini, mimi ninakuhakikishia kwamba kile mimi na Drenda tulichogundua kitapatikana kwako jinsi kilivyokuwa kwetu. Ombi langu ni kwamba tunaposhiriki hadithi yetu, utatiwa moyo kutumia sheria na kanuni za Mungu maishani mwako pia.

Kwa kweli si vigumu sana; unahitaji tu kugundua nguvu ya pumziko!

*Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu; kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.*

— Mathayo 11:28-30

# SURA YA 1

## PUMZIKO – JAMBO LA KIMSINGI

**KUPUMZIKA** - kuwekwa mahali au kusaidiwa ili kukaa katika nafasi maalum, mfano au kipindi cha kustarehe au kuacha kujihusisha na shughuli ngumu au yenye shinikizo. (Maana imetolewa kutoka *Google*.)

Je, Umechoka? Je, umezidiwa kwa siku nyingi na hujawahi kutimilika? Je, hitaji lako la pesa ndilo linaloongoza maamuzi yako kuhusu mahali unapofanya kazi au jinsi unavyofanya kazi au muda gani unafanya kazi? Je, inaonekana kana kwamba hutawahi kutoka kwa madeni? Je, inaonekana kwamba unaishi maisha ya mbio za panya kama methali inavyosema? Ikiwa ndio, hauko peke yako.

Umewahi kuona gurudumu la panya? Nina hakika umeliona, lakini ikiwa sivyo, ni gurudumu ambalo huwekwa ndani ya kizimba cha panya. Panya anaweza kupanda kwenye gurudumu hilo na kukimbia na kukimbia na kukimbia hadi anachoka. Lakini kuna shida moja tu na gurudumu hilo. Haijalishi panya huyo amekimbia kwa kasi gani au kwa muda gani, yeye akichoka kabisa huwa anashuka kutoka hapo, na kurudi katika hali ileile aliyokuwa alipoanza. Hakuna kinachobadilika. Anaweza kupanguza jasho kutoka kwa uso wake mdogo ulio na manyoya akiwa na hisia ya kuridhika. Lakini hakuna kilichotimizwa ili kumfaidi maishani; bado amefungwa kwenye kizimba bila uhuru. Hii ndiyo hali ya kawaida ya watu wengi, na maisha yao ya kifedha. Wanafanya kazi kwa bidii wiki nzima na kuchoka kupita kiasi kisha wanapata afweni kidogo katika wikendi, lakini Jumatatu asubuhi inapofika, wanajikuta mahali sawa kabisa na walivyokuwa wiki

iliyopita. Kile wamefanya tu ni kunusurika wiki moja zaidi.

Hii ilikuwa picha ya maisha yangu kwa miaka tisa mirefu. Nilikuwa nafanya kazi kwa bidii kwa masaa 15 hadi 18 kwa siku, na nilifanya kazi kwa bidii, lakini baada ya kulipa zaka yangu, bili zangu, na kodi, hakukuwa na chochote kilichosalia. Kwa kawaida, nilipungukiwa na kile nilichohitaji na polepole nikaanza tabia ya kukopa ili kuishi. Shinikizo la kifedha lilipoongezeka, nilijisukuma zaidi na zaidi, lakini sikufaulu. Nilipotathmini maendeleo yangu, nilipata kwamba bado nilikuwa nikirudi nyuma.

Jambo hili bila shaka lilisababisha madhara fulani ya kihisia. Kukata tamaa na woga niliopambana nao kila siku polepole uliathiri akili yangu na mwili wangu. Mashambulizi ya wasiwasi, hofu kali, na kupooza kulianza kuathiri mwili wangu polepole. Madaktari hawakuweza kujua ni kitu gani kilichoniathiri. Hofu ilitawala mawazo yangu kiasi kwamba sikujua kama ningeishi au kufa. Niliendelea katika maisha ya kukopa kutoka kwa maduka ya mikopo na kutoka kwa jamaa kwa karibu miaka tisa! Kufikia hapo sikuwa na mahali pengine pa kukopa, na nilikuwa na maoni ya chini sana juu yangu. Ungeweza kukusanya jinsi nilivyojitathmini na kifaa cha kukusanya vumbi, pamoja na furaha yoyote iliyosalia maishani mwangu.

Wadai walikuwa wakipanga foleni kunifungulia mashtaka, na hapo ndipo jambo lilipotokea. Huku kukata tamaa kukiwa kumeshinikiza pumzi yangu yote, nilipigiwa simu. Ilikuwa kama simu nyingine yoyote ya asubuhi: “Bw. Kesee, kama unavyojua, unamdai mteja wetu kiasi X cha pesa. Unafikiri unaweza kutuletea pesa hizo lini? Vema, Bw. Keesee, nimekupigia simu mara tatu na umesema vivyo hivyo. Usipotuletea pesa hizo kabla ya siku tatu kuisha, mteja wangu ataanzisha mashtaka dhidi yako kuhusu deni hili. Unaelewa, Bw. Keesee? Siku tatu. Kwaheri.”

Simu hiyo ilinipiga kama tani ya matofali. Si kwamba sikujua jinsi hali yetu ya kifedha ilivyokuwa mbaya. Sikuwa na pesa. Kila kitu nilichomiliki kilikuwa kimezeeka. Jokofu langu lilikuwa tupu. Familia yangu nzuri ilikuwa ikilala karibu na mahali pa kuwashia kuni ili kupata joto kwa sababu sikuwa na pesa kununua mafuta ya kupasha joto. Sikuwa na mahali pa kugeukia. Marafiki na familia yangu walikuwa wamechoka kunitoa kwa matatizo yangu. Nikiwa nimechanganyikiwa, taratibu nilipanda ghorofa hadi kwa chumba changu na kujilaza kitandani. Niliomboleza na kumlilia Bwana anisaidie.

Nafikiri nilishangaa jinsi Bwana alivyozungumza nami kwa haraka. Haikuwa sauti ya kusikika bali ilikuwa sauti ya ghafula iliyotoka rohoni na akilini mwangu kwa nguvu. Jambo la kwanza Bwana aliloniambia ni

kwamba janga nililokuwa nalo halikuwa kwa sababu Yake hata kidogo. Nafikiri alisema hivyo kwa sababu nilichanganyikiwa kidogo kwa nini Yeye, kulingana na mtazamo wangu, hakuwa ametusaidia. Tulikuwa washirika wa kanisa nzuri, tulikuwa wakarimu tulipoweza, na tulilipa zaka zetu mara nyingi. Lakini Yeye alisema nilikuwa katika janga hilo kwa sababu sikuwa nimejifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Aliniambia kwamba Ufalme Wake haufanyi kazi kama ulimwengu unavyofanya kazi inapohusu pesa, na ilibidi nijifunze mfumo Wake wa Ufalme wa kushughulikia fedha ikiwa nilitaka kuwa huru.

Nakumbuka nilikimbia chini na kumshika Drenda na kumwambia kwamba Bwana alikuwa amenena nami na kwamba jibu lilihusu Ufalme Wake. Bila shaka, tulichanganyikiwa kidogo, maana tulifikiri tulielewa Ufalme Wake ni nini. Hata hivyo, kama nilivyosema awali, tulishiriki katika kanisa nzuri, sote tulimpenda Mungu, na tulijua tulikuwa njiani kuelekea mbinguni. Lakini tulikuwa karibu kutambua jinsi tulivyokuwa na ufahamu mdogo sana kuhusu Ufalme Wake na jinsi unavyofanya kazi.

Nilifurahi kwamba Mungu alikuwa amenena nami na alikuwa amefunua jibu—Ufalme Wake. Maana yake bado haikuwa imeeleweka, lakini nilitiwa moyo. Ukweli ni kwamba sikuwa na habari yoyote Mungu alimaanisha nini alipotamka neno *ufalme*. Nilikuja kutambua kwamba jibu langu na Drenda ambalo tulikuwa tumetamani sana na kutafuta lilikuwa katika neno hilo moja.

Siku hiyo mimi na Drenda tulishikana mikono na kuomba. Kwanza, tulitubu kwa Mungu kwa kutotenga wakati kujifunza Neno lake na jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi inapohusu fedha. Pili, mimi kama kichwa cha familia yetu nilitubu kwa Drenda, kwa kutuingiza katika janga hilo. Sisi sote tuliomba na kukubali kwamba tumeazimia kujifunza jinsi Ufalme unavyotenda kazi na kuishi maisha tofauti na yale tuliyokuwa nayo kwa miaka tisa.

Njia bora ya kueleza kile kilichofuata ni kuangalia kibonyezi cha taa. Ingia kwenye chumba kilicho na giza na ubonyeze kibonyezi cha taa. Ghafula Mwanga! Unaweza kuona. Hivyo ndivyo ilivyokuwa Mungu alipoanza kutufundisha kuhusu Ufalme wake. Ilikuwa ni kama mtu aliwasha kibonyezi cha taa, kisha tukaanza kuona mambo ambayo hatujawahi kuona hapo awali. Tulianza kuelewa kwamba Ufalme wa Mungu ni serikali yenye sheria zisizobadilika. Tuligundua kwamba tunaweza kujifunza sheria hizo na kupokea nguvu na hekima ya Mungu kupata utajiri tuliohitaji.

Tulifurahi sana lakini bado tulikuwa tumechanganyikiwa sana.

Kulikuwa na baadhi ya mambo ya kustaajabisha yaliyotokea Mungu alipoanza kutufundisha jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Sitazungumzia nyingi ya hadithi hizo za mwanzoni hapa maana ziliangaziwa katika kitabu cha kwanza katika mfululizo huu, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa Mwaminifu*. Unaweza kupata nakala katika [garykeese.com](http://garykeese.com). Unahitaji pia kupata kitabu changu, *Faith Hunt*, ambacho kitakurudisha nyuma hadi mwanzo kabisa wakati Mungu alipoanza kunifundisha jinsi ya kuvuna riziki kupitia kwa uwindaji wangu wa kulungu. Lakini ili kufupisha mambo, hebu nikupe mfano mmoja hapa.

Kama nilivyokuambia tayari, tulikuwa na madeni chungu nzima. Kudaiwa na shirika la ushuru, kudaiwa na maduka ya ukopeshaji, kadi 10 za kukopesha zilizokuwa zimeghairiwa, na mikopo 3 ya kampuni za fedha kwa riba ya 28%. Tulidaiwa na daktari wetu wa meno, maduka ya kuosha mavazi, wazazi wetu, na marafiki zetu. Taja yeyote, tulim dai. Kiasili, hatukuwa na tumaini. Biashara yangu ya kuuza bima haikuwa ikienda vizuri, hata kama nilikuwa nikifanya kazi kwa bidii. Lakini sasa baada ya kuona Ufalme ukifanya mambo ya ajabu sana (tena, soma hadithi hizi katika vitabu viwili vilivyotajwa hapo juu), tulitiwa moyo kwamba Ufalme ulikuwa jibu letu. Hatukujua kwa jinsi gani, lakini tuliadini tulikuwa katika njia sahihi.

Kisha usiku mmoja Mungu alinipa ndoto kwamba nilipaswa kuacha kampuni yangu ambapo nilikuwa nimefanya kazi kwa miaka tisa na kuanzisha kampuni yangu mwenyewe—sasa pata hili—ili kuwasaidia watu kutoka kwa madeni! Najua; linasikika kama jambo la kichaa, sivyo? Kama ningejua jinsi ya kutoka kwa deni, ningefanya hivyo miaka mingi awali. Lakini hivyo ndivyo hasa alivyofanya. Kwa kweli nilishtuka kidogo. Sikuwa na ufahamu wa jinsi ya kuanzisha kampuni yangu mwenyewe au yale yaliyohusika. Lakini kampuni ya kusaidia watu kutoka kwa madeni? Jamani! Kwa hilo nilihitaji mtu wa kuniambia jinsi ya kufanya hivyo!

Nilipoanza kuomba kuhusu jinsi jambo hili lingelivyoweza kutokea, Roho Mtakatifu alibadilisha maisha yangu. Ilitokea wakati mteja wangu mmoja wa biashara yangu ya bima aliponipigia simu. Oh, nilisahau kukuambia kwamba nilikuwa nikifanya kazi katika tasnia ya huduma za kifedha nikiuza bima na dhamana wakati haya yote yalifanyika. Najua, ni kama vile fundi bomba aliye na tatizo kwake la mfereji unaodondoka maji anavyoshughulikia mifereji ya watu wengine, huku akipuuza shida ya kwake. Ingawa polepole nilikuwa nimeanza kutofaulu katika kazi yangu ya huduma za kifedha, uzoefu na maarifa ya kijumla niliyoyapata katika tasnia

hiyo kwa miaka tisa, sasa ulikuwa muhimu sana katika yale ambayo Mungu alitaka kunionyesha.

Nilipokuwa nimeketi mezani pamoja na mteja wangu na mke wake jikoni mwao, tulipitia uwasilishaji wa kawaida, ambapo tulitathmini hali yao kifedha kwa kuuliza maswali mbalimbali na kujaza kile tunachoita fomu ya taarifa. Kimsingi taarifa hii ilitumiwa kuamua kiwango cha bima ya maisha walichopaswa kuwa nacho. Tulipokuwa tukipitia orodha yao ya madeni, wote wawili walikasirika na mke akaanza kulia huku wakieleza jinsi wote wawili walivyokosa matumaini. Wote wawili walikuwa wakifanya kazi za mchana kutwa na pesa hazikuwatosha kila mwezi.

Sasa mimi baada ya kuishi hivyo kwa miaka tisa, na Mungu akaanza kunifundisha pamoja na Drenda kuhusu Ufalme, unaweza kufikiria jinsi nilivyohisi kuwahusu. Kama mimi na Drenda, wote walikuwa Wakristo lakini bila ujuzi wa jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Wakati huo, kwa kweli sikuweza kueleza mengi juu ya Ufalme isipokuwa baadhi ya mambo ya awali ambayo Mungu alikuwa ametuonyesha tayari, ambayo nilishiriki nao, na, bila shaka, nilishiriki baadhi ya hadithi za kustaajabisha tulizokuwa tumeona zikitukia katika hali yetu.

Bila shaka, ningeweza kuona kwamba bima ya maisha haikuwa shida yao kuu. Nilichukua muda kuwaeleza yale ambayo Mungu alikuwa ananifundisha kuhusu Ufalme, lakini nilitamani jambo ambalo ningeweza kufanya ili kuwapa majibu halisi ya kifedha kuhusu hali yao.

Ofisini usiku huo, nilipokuwa katika shughuli za kumaliza siku yangu huku nikichambua mrundiko wangu wa kawaida wa mafaili na jumbe nilizohitaji kujibu, ghafla niliwaza. Je, ingekuwaje kama ningechunguza kwa kina picha yao yote ya kifedha badala ya kuangalia suala lao la bima ya maisha tu? Je, kuna chochote ambacho ningeweza kufanya? Je, kama ningetafuta pesa? Ninachomaanisha ni kwamba je, ingekuwaje kama ningepata njia za gharama nafuu za kufanya mambo ambayo tayari walikuwa wakifanya? Lengo langu lingekuwa rahisi, kutafuta njia za bei nafuu zaidi za kufanya mambo ambayo tayari walikuwa wakifanya, kisha kuongeza pesa zozote zilizopatikana kwa pesa zao na kwa madeni. Lilionekana kama pendekezo rahisi, lakini kwa kweli sikujua mengi kuhusu nyanja nyingine yoyote ya kifedha ila ya bima ya maisha. Na ninahitaji kukuambia kwamba hizi zilikuwa nyakati za kabla ya siku za mtandao. Utafiti niliohitaji kufanya ungefanywa kwa njia ya kizamani—kupitia kwa simu na saraka ya orodha ya simu na biashara.

Nilifanyia hilo kazi wiki nzima maana nilipaswa kukutana na mteja



wangu tena wiki iliyofuata. Nilishangazwa na kiasi cha pesa ambazo ningeweza kuokoa kwa mwezi mmoja nilipochukua muda wa kuchunguza kwa kina kila eneo la kifedha. Nilipomaliza, kiasi cha fedha kiliongezeka hadi mamia ya dola kwa mwezi. Kwa kikokotoo changu cha fedha, nilijumlisha madeni yao yote kisha nikatumia pesa zilizookolewa kwenye malipo yao ya kawaida ya kila mwezi. Nilipoangalia jibu kwa skrini nilistaajabu—ilikuwa miaka 6.2. Mteja wangu angechukua miaka 6.2 kulipa madeni yake yote, ikiwemo rehani ya nyumba yake, bila kubadilisha mapato yake. Naam, umesoma vema, bila kubadilisha mapato yake ya kila mwezi. Nilishtuka nikafikiri nilikuwa nimakosea mahali, kwa hivyo nilirudia hesabu hiyo tena na tena hadi niliposadiki kwamba nilikuwa na jibu sahihi. Je, hili lawezekana? Kwa nini kila mtu hajui hili?

Kwa haraka nilichukua faili za wateja wengine kadhaa nilizokuwa nazo na kuzichunguza haraka nazo zilikuwa matokeo yale yale. Kila mmoja wao angeweza kutoka kwa deni katika miaka 5 hadi 7, pamoja na rehani yao, bila kubadilisha mapato yao ya kila mwezi. Muda sasa ulikuwa umeyoyoma ofisini huku nikimaliza hesabu zangu, lakini furaha iliniingia nilipokuwa nikielekea nyumbani. Ikiwa kile nilichopata kilikuwa kweli, na hesabu zangu zote zilionyesha hivyo, basi hili lilikuwa jambo kubwa, kubwa sana.

Nilikuwa na hamu ya kujua jinsi mteja wangu angeitikia habari hii. Kwa ajili ya mkutano wangu nao, niliamua kuchapisha hesabu hiyo kwa njia rahisi kwa ukurasa mmoja. Kusudi langu lilikuwa kuwapa tumaini tu. Hakukuwa na manufaa yoyote kwangu katika hilo, maana nilijua huenda hawangeweza kununua bima ya maisha. Lakini nilijua wangetaka pia kusikia kile nilichokuwa nimegundua. Wiki iliyofuata nilirudia tena mahesabu yangu na nikawa na uhakika zilikuwa sahihi.

Nilipogonga kengele ya mlango wao, nilihisi wasiwasi kuhusu mkutano wetu. Nilipoketi mezani katika jikoni lao, niliwaeleza kile nilichofanya wiki nzima na hesabu zao. Niliwaonyesha hesabu hizo kwa utaratibu huku nikiwaeleza jinsi nilivyookoa pesa, pamoja na majina ya makampuni na nambari za simu zozote ambazo zingehitajika katika kutekeleza yale niliyowaonyesha. Niliona kwamba walianza kuchangamka walipoona pesa zilizookolewa zikiendelea kuongezeka. Lakini nilipofikia hitimisho kwamba wangeweza kutoka kwa madeni kabisa katika miaka 6.2, pamoja na rehani yao, wakiwa na malipo yale yale ya kila mwezi, wote wawili walianza kulia, wakati huu kwa shangwe. Waliketi machozi yakiwadondoka, huku wakisema jinsi walivyoshtushwa na matokeo hayo. Kisha wakaanza kuruka juu huku wakinikumbatia, na tukawa na wakati mzuri wa sherehe usiku huo.

Hebu tuseme ukweli: Je, shirika la ushuru litakuambia jinsi ya kulipa kodi kidogo? Je, mwenye benki atakuambia jinsi ya kuepuka kulipa riba? La, mfumo mzima umeundwa kuchukua pesa zako, sio kuzilinda. Nilifahamu kwamba kile nilichokuwa nimegundua kilihitaji kufundishwa kwa kila familia huku Amerika! Maisha yangu yaliguswa sana usiku huo, na nilitaka kumfanyia kila mteja niliyekutana naye vivyo hivyo.

Kwa hiyo, tukiwa na habari hiyo na kwa uthibitisho wa ndoto ambayo Mungu alinipa, mimi na Drenda tuliacha kampuni ya bima ya maisha ambapo nilikuwa nikifanya kazi na tukaanzisha kampuni yetu, tukifanya kile nilichokuwa nimemfanyia mteja yule. Katika miaka hiyo ya mwanzo, tuliita kampuni yetu, "Faith-Full Family Finances." Jina hilo lilisema wazi kile tulichokuwa—ukielewa Ufalme na imani, fedha zako zitajaa. Ninakubali halikuwa jina la kufaa sana kwa kampuni—hebu jaribu kulitamka mara kumi mfululizo—lakini lilifanya kazi. Baadaye tulibadilisha jina kuwa Forward Financial Group, ambalo liko hadi sasa na kampuni inaendelea kuimarika.

Kwa kweli, fedha zetu binafsi bado hazikuwa zimejaa. Bado tulikuwa na madeni hayo yote, lakini tulifahamu kwamba tulikuwa tumepata njia ya kufuata. Tulipozindua kampuni yetu mpya, tulikuwa na furaha pamoja na wasiwasi kidogo. Tulikuwa na mengi ya kujifunza kuhusu kuanzisha na kuendesha kampuni, lakini kikwazo kikubwa tulichokabiliiana nacho kilikuwa jinsi ya kutengeneza pesa kwa kufanya hivyo. Changamoto yetu ilikuwa tulihisi hatungeweza, na hatukutaka kuwatoza watu pesa ili kuwasaidia kutoka kwa madeni. Hiki kilikuwa kikwazo kikubwa ambacho tulitumia muda mrefu sana kuomba na kufanya uamuzi. Kwa ufupi, Bwana alituoonyesha mkakati wa ajabu wa kuanzisha kampuni na kuifanya izalishe pesa bila kuwatoza wateja ada.

Kisha, ilitubidi tutafute njia ya kuharakisha mahesabu marefu ya taarifa za wateja wetu tulizokuwa tukifanya kwa kuandika na mkono. Nilifahamu kwamba ingenilazimu niwe na programu ya kompyuta ili kuweza kufanya kile tulichokuwa tukifanya, lakini sikujua chochote kuhusu kompyuta au jinsi ya kupata mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Tena, Mungu alifanya jambo la ajabu. Nilipokea simu kutoka kwa mtu ambaye alikuwa anaishi mbali nasi kwamba alikuwa amesikia habari zetu. Yeye kama mteja alitaka kuona kile tulichokuwa tukifanya. Alikipenda na tulipokuwa tukizungumza, niligundua kwamba alikuwa mtaalamu wa programu za kompyuta na alikuwa na kampuni yake binafsi kama kazi ya kando. Nilizungumza naye kuhusu hitaji letu, naye alisema kwa

shauku sana kwamba alitaka kutusaidia katika yale tuliyokuwa tukifanya. Nilimwambia tulikuwa tunaanzisha kampuni yetu na hatukuwa na pesa za kumlipa, ingawa tayari alikuwa ametupunguzia malipo kwa kiasi kikubwa. Lakini bado alitaka kutufanyia kazi hiyo na akasema tumlipe kila wakati pesa zilipoingia. Hivyo ndivyo tulivyofanya.

Watu walipenda biashara yetu. Kwa nini wasingeipenda? Ilikuwa bila malipo, na watu walipenda kuokoa pesa ili kutoka kwa madeni. Biashara ilinawiri haraka, na tuliweza kutoka kwa madeni katika miaka miwili na nusu. Punde tulikuwa na wawakilishi zaidi ya 300 walioshiriki mpango wetu kotekote nchini. Kando na kuweza kulipia magari yetu pesa taslimu, tulijenga na kulipia nyumba ya ndoto zetu. Kampuni yetu ilikua na imetuwezesha kutoa mamia ya maelfu ya dola ili kusaidia Injili na watu kwa miaka mingi.

Baada ya miaka 30, “Mpango wa madeni,” kama tunavyouita, ungali unatolewa bila malipo. Kampuni ilipanuka katika utume wake kadiri miaka ilivyosonga. Tulianza kuzingatia uwekezaji wa kustaafu baada ya majanga ya kifedha ya miaka ya 2001 na kisha 2008 ambapo mamilioni ya watu walipoteza asilimia 50% hadi 80% ya akiba zao za kustaafu. Tulitafiti njia salama za uwekezaji kisha tukazindua kipengele hicho cha biashara yetu katika mwaka wa 2001. Ninajivunia kusema kwamba kati ya zaidi ya dola milioni mia moja za wateja wetu tunazosimamia sasa, hakuna hata senti moja iliyopotea katika miaka 16 iliyopita, yenye machafuko ya kifedha nchini mwetu na duniani. Na kama mpango wetu ulivyokuwa tangu awali, hakuna ada, wala ada ya usimamizi au ya wakala inayolipishwa mwanzoni au kila mwaka kwa wateja wetu wa uwekezaji. Ikiwa umechoka kucheza kamari na pesa zako za kustaafu, unaweza kufikia Forward Financial Group kwa nambari 1-(800)-815-0818 au [Forwardfinancialgroup.com](http://Forwardfinancialgroup.com) kwa maelezo zaidi.

**WAZO MOJA RAHISI  
KUTOKA KWA ROHO  
MTAKATIFU LILIBADILISHA  
MAISHA YETU MILELE!  
NAAM, ILITUBIDI  
TULIFANYIE KAZI, LAKINI  
MUNGU ALITUONYESHA  
JINSI YA KUFANYA HIVYO.**

Inashangaza sivyo? Wazo moja rahisi kutoka kwa Roho Mtakatifu lilibadilisha maisha yetu milele! Naam, ilitubidi tulifanyie kazi, lakini Mungu alituonyesha jinsi ya kufanya hivyo. “Ulihisije, Gary, kutoka kwa madeni?” Amani! Pumziko! Tafakari hili. Tulitoka katika hali mbaya ya kifedha hadi kutokuwa na madeni kabisa, kulipia magari yetu pesa taslimu, nyumba yetu,

na kila kitu kingine tulichohitaji. Kwa miaka tisa mirefu, nilikuwa chini ya shinikizo kubwa kila dakika kila siku. Sikuwa na raha. Haijalishi ilikuwa siku gani katika wiki, au kama ilikuwa likizo. Sikuwa na amani. Masuala yangu ya kifedha yalinifuata kila mahali nilipoenda. Nilivumilia aibu na fedheha mara kwa mara kutokana na hali yetu ya kifedha. Hofu ilikuwa rafiki yangu kila wakati, mashambulizi ya hofu na dawa za kupunguza mafadhaiko vilikuwa vitu vya kawaida katika maisha yangu ya kukata tamaa.

Kuwa na mabadiliko hayo yote ya kifedha, na bila shaka kuwa na vitu tulivyohitaji maishani, unaweza kufikiri kwamba tulikuwa tumepata ushindi katika eneo la kifedha. Ndio, hatimaye kuwa na vitu tulivyohitaji ulikuwa ushindi mkubwa, lakini msisimko wa kweli ulikuwa kuona Ufalme wa Mungu ukitenda kazi. Mimi na Drenda tulipoona utendaji wa Ufalme tena na tena, mara nyingi tulisema, “Je! Umeona hilo?” Kama vile kila kitu kinapokuwa dhahiri wakati kibonyezi cha taa kinapowashwa, kuwa na uwezo wa kuona baada ya kuwa kipofu na kuishi bila majibu ni jambo la ajabu. Kupata hazina yetu ya kweli ambayo ni Ufalme wa Mungu, kulistaajabisha sana. Kujaribu kukuambia jinsi nilivyohisi ni rahisi—kwa mara ya kwanza maishani mwangu, kulikuwa na pumziko!

Heka heka zilikoma! Hapo awali, gurudumu la gari letu lilipopasuka, ilikuwa shida kubwa kihisia. “Tutapata wapi pesa? Je, kuna fursa yoyote kwenye kadi?” Lakini leo, ikiwa kwa sababu moja au nyingine gari letu lingelipuka, nitamwuliza mke wangu, “Unataka gari rangi gani wakati huu?” Hakuna wasiwasi, hofu, madeni, bali pumziko tu. Sasa tunazingatia kazi ya utume wetu na kusudi letu. Hatuishi tena maisha ya manusuru, bali tunajishughulisha na MAISHA!

*Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Waangalieni ndege wa angani, ya kwamba hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi ghalani; na Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Ninyi je! Si bora kupita hao?*

— Mathayo 6:25-26

Katika miaka hii 36 iliyopita, nimeketi na maelfu ya watu mezani kwenye majikoni yao na kujadili kuhusu fedha zao kwa kiwango cha kibinafsi. Nimezungumza na umati wa maelfu ya watu duniani kote, na jambo moja ninalopata kila mahali ni kwamba kila mtu anatafuta pumziko!

Kila mtu anatazamia kwa hamu wikendi, likizo, au kustaafu—yaani kukoma na kupumzika.

Tafiti kadhaa za hivi majuzi nilizosoma zilisema karibu asilimia 70% ya Wamarekani hawapendi kazi zao, na asilimia 20% kati ya hiyo 70% hawazishughuliki na inajulikana kwamba hawapendi kazi zao. Kwa nini basi huwa wanaenda kufanya kazi wanayoichukia? Wanaishi chini ya shinikizo aina gani ili kustahimili maumivu mengi ya kihisia kila siku? Kusema kweli, wao ni watumwa. (Sote tulikuwa vivyo hivyo. Tumekulia katika ulimwengu ambapo njia pekee ya kustawi ni kuwa na pesa za kutosha ili kuwa na uwezo wa kuchagua mambo mbalimbali. Lakini kwa watu wengi sivyo.) Ndoto zao za kustawi hufifia polepole hadi kwa maisha ya manusuru huku wakijikuta katika kazi zisizo na matumaini katika miaka yao ya 30, 40, na hata 50.

Takwimu za hivi majuzi zinasema kwamba asilimia 69% ya wakazi wa Marekani hawana hata dola elfu moja katika akiba zao. Mashinikizo na viwewe vya kihisia vinavyokandamiza maisha ya watu wengi hudhoofisha hali yao ya kutijambua na kujithamini. Ndoto huwekwa kando ili kukidhi mahitaji ya haraka na kukata tamaa kunaanza kutawala, kisha furaha inatoweka.

Siku moja, nakumbuka nilizungumza na mchungaji fulani kuhusu fedha. Aliniambia kwamba alipenda huduma na watu, lakini kila siku aliamka na msisimko hadi alipokumbuka hali yake ya kifedha. Aliniambia ilikuwa kana kwamba wingu kubwa jeusi lilikatiza mwanga wa jua, huku mawazo ya kukatisha tamaa yakimwingia akilini na kumshika mateka katika mtazamo wa kuishi maisha ya manusuru, kutokuwa na matumaini kifedha, na utumwa usio na maono.

Maisha yamefanyika jambo la kutazama wengine wakishinda.

## **KUISHI MAISHA YENYE SHINIKIZO LA KIFEDHA SI...MPANGO WA MUNGU KWAKO LEO PIA.**

Hollywood imepata mabilioni ya dola kwa kuonyesha watu wengine wakishinda kwenye skrini kubwa. Watu wasioweza kujiona wakishinda kibinafsi hupata dakika chache za kutoroka kutoka kwa kazi zao ngumu na kuishi katika ndoto

zao kwa kutazama watu wakamilifu wakiishi maisha makamilifu kwenye skrini kubwa.

Leo michezo hupata mabilioni ya dola kwa mwaka kutoka kwa watazamaji kote ulimwenguni. Katika mwaka wa 2017, Ligi ya taifa ya mchezo wa mpira ilipata zaidi ya bilioni 7.8; mchezo maalum wa mpira unaoitwa *Super Bowl*, wastani wa bilioni 15.5; na huo ni mchezo mmoja tu!

Watu hupenda kuishangilia timu wanayoipenda hadi wanaposhinda.

Lakini kile tunachohitaji kuelewa ni kwamba sote tulikusudiwa na tumeumbwa kushinda—kuwa katika mapambano, kuwa mchezoni, na hatimaye kushinda. Kutokuwa na tumaini kifedha ni kawaida kwa watu wengi—kwa hivyo njia pekee ya kuepuka ni kuishi maisha ambayo sote tunayatamani kupitia kwa maisha ya wengine. Kinachovutia katika kushinda bahati nasibu ni nini? Kwa nini kipindi cha televisheni cha *Who Wants To Be A Millionaire* kilikuwa maarufu sana? Kwa nini leo watu bado hujaribiwa kuingia katika mipango ya kupata utajiri haraka? Jibu? PUMZIKO! Kila mtu amechoka kukimbia, kila mtu amechoka kuamka na uzito wa kuibiwa ndoto zao kwa kutafuta riziki. Lakini kuishi maisha yenye shinikizo la kifedha si jambo jipya; kwa kweli, kumekuwepo tangu mwanadamu aanze kuishi duniani. Hata hivyo, huo haukuwa mpango wa Mungu hapo mwanzo, na si mpango wa Mungu kwako leo pia.



## SURA YA 2

# HAKI ZA KISHERIA

Bila matumaini—hivi ndivyo ningeeleza maisha yetu kabla yetu kuelewa jinsi ya kupumzika. Miaka tisa ni muda mrefu wa kuishi katika vurugu na dhiki ya kifedha. Ninakumbuka tulikuwa tumekodisha shamba la ekari 85 kwa malipo ya \$300 kila mwezi, ambayo ilikuwa bei nafuu sana ingawa hatukuwa na uwezo wa kufanya malipo ilivyostahili, na mara nyingi nililitazama na kuwaza kama ningewahi kumiliki shamba kama hilo.

Mmiliki wa shamba hilo alikuwa na mpango wa kujenga uwanja wa gofu hapo na alitaka mtu wa kuishi na kumchungia mali yake kabla ya kuanza mradi wake, ambao walikadiria ungeanza baada ya miaka mitatu hadi mitano. Nyumba kuukuu iliyokuwa pale shambani ingekaa “vile vile,” na hawakutaka kulipia marekebisho yoyote wakati huo. Tuliichukua, na baada ya kuipiga rangi na kuisafisha kabisa, nyumba hiyo nzee ilipata sura ya kuvutia. Mpango wetu ulikuwa kwamba tuishi huko kwa miaka mitatu kisha tuondoke, lakini hata baada ya kuishi huko kwa miaka minane bado hatukuwa tumekaribia kumiliki chochote.

Baada ya Mungu kunena nami kuhusu Ufalme, kisha tukaanza kujifunza na kutumia kanuni na sheria za Ufalme, mambo yalianza kubadilika. Hapo mwanzoni fedha zetu zilipoanza kuboreka, tulifurahishwa sana na ushindi wowote mdogo. Nakumbuka wakati mmoja tulipokuwa katika nyumba hiyo kuukuu tulifurahi sana, hasa Drenda, niliponunua mashine ya kuosha vyombo! Ingawa wakati mwingine nilisaidia Drenda kuosha vyombo, nilikuwa pia na shughuli nyingi za kibiashara. Wakati huo, alikuwa akiosha vyombo kila mara kwa sababu alikuwa na watoto wanne wadogo nyumbani. Tuliponunua mashine hiyo, nakumbuka nikisema hivi,



“Je, unaweza kuamini kwamba tumelipia mashine mpya ya kuosha vyombo pesa taslimu?” Najua, unawaza, “Ala, kuna jambo gani kubwa katika kununua mashine ya kuosha vyombo?” Ili kukupa mtazamo sahihi, inabidi ujue ni vifaa gani tulivyokuwa navyo jikoni mwetu. Jiko letu na jokofu vilikuwa vya rangi ya kijani kibichi na vilikuwa na umri wa miaka 25. Kwa hiyo kwa kulinganisha, kununua mashine mpya ya kuosha vyombo ulikuwa ushindi mkubwa kwetu.

Katika sura iliyopita, nilishiriki jinsi Mungu alivyoniipa ndoto na mpango wa kuanzisha biashara ambayo ingekuwa jibu la janga letu la kifedha. Labda unawaza, “Laiti Mungu angeniambia jambo kama hilo.” Habari njema ni kwamba Yeye anatamani kufanya hivyo, lakini kuna baadhi ya mambo ambayo ni lazima uyajue kuhusu jinsi Ufalme unavyofanya kazi kabla ya kupata msaada wa aina hiyo. Mwelekezo niliopata siku ile katika ndoto ulitokea moja kwa moja kwa sababu ya yale Mungu alikuwa anatufundisha kuhusu Ufalme Wake na kwa kutumia yale ambayo alikuwa ametuonyesha. Ingawa nilizungumzia Ufalme kwa undani sana katika kitabu changu cha awali, ninahitaji kukirejelea tena hapa ili kukupa msingi sahihi.

Watu huniuliza ninamaanisha nini ninaposema Ufalme wa Mungu. Sikuujua Ufalme wa Mungu ingawa nilikuwa Mkristo. Nilijua nitaenda mbinguni nikifa, lakini sikuuelewa Ufalme wa Mungu na utendaji wake. Ili kuelewa dhana hii, unahitaji kuelewa maana ya neno *ufalme*. Maana yake halisi ni utawala wa mfalme. Ufalme haufanyi kazi ila tu kwa maneno ya mfalme. Maneno yake ndiyo sheria inayotawala ufalme wake na maisha ya raia wake. Dhana nyingine ni kwamba ufalme hauhitaji kuwa na watu milioni moja. Ufalme unamaanisha ipo serikali yenye sheria zinazomfanya kila raia halali wa ufalme huo kutii sheria za mfalme. Dhana hii ya kwamba Mungu ana Ufalme ulio na sheria ambazo zipo kwa ajili ya kila raia halali wa Ufalme Wake haijulikani katika sehemu kubwa ya Ukristo. Wakristo wengi wanaamini kwamba Mungu ndiye anayeamua ni maombi gani atakayojibu au ni nani atakayempendelea. Wanaamini kwamba ikiwa watafunga kwa muda mrefu sana au kumfanyia Mungu kazi zaidi ya kiroho, basi watapata kibali Naye. Rafiki yangu, tayari una kibali Naye.

*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.*

— Waefeso 2:19

Wewe si raia tu wa Ufalme Wake, lakini pia wewe ni mwanafamilia katika nyumba Yake, mwana au binti wa Mfalme. Wagalatia 4 inaweka wazi kabisa maana ya jambo hili kwako na kwangu.

*Lakini nasema ya kuwa mrithi, wakati wote awapo mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ni bwana wa yote; bali yu chini ya mawakili na watunzaji, hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. Kadhalika na sisi, tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomoe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Robo wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, "Aba," yaani, "Baba." Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.*

— Wagalatia 4:1-7

Wewe ni mrithi wa mali yote ya Mungu kama mwana au binti, na una haki za kisheria kama raia wa Ufalme Wake! Hebu hilo liingie ndani yako kwa muda mfupi—tayari una kila kitu. Hakuna kitu unachohitaji ambacho huna tayari. Kwa hivyo acha kumsihi na kumlilia Mungu. Huwezi kuomba kupewa kitu ulicho nacho tayari. Mungu huwa haangalii kila kesi na kufanya uamuzi kuhusu ni nani atasaidia au kutosaidia. Yeyote ambaye ni mwana au binti wa Mungu tayari ana msaada Wake.

Hebu nilinganishe hili na kuwa raia wa Marekani. Ikiwa wewe ni raia, basi tayari unaungwa mkono na serikali ya Marekani kutekeleza kile ambacho sheria inasema. Faida hiyo inajumuishwa na uraia wako. Kwa hivyo, huwezi kufunga na kuomba vya kutosha ili kupata msaada Wake; Yeye tayari amekupa bila malipo kupitia yale aliyoyafanya Yesu. Kwa hiyo furahia msaada Wake. Tayari unaumiliki!

*Akatufufua pamoja Naye, akatuketisha pamoja Naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhibirishwe wingi wa neema Yake upitao kiasi kwa wema Wake kwetu sisi katika Kristo Yesu.*

— Waefeso 2:6-7

Maneno, “*akatuketisha pamoja Naye katika ulimwengu wa roho*”

**HISIA NI NZURI, NA  
NINAPENDA KUHISI UWEPO  
WA MUNGU, LAKINI  
INAPOHUSU MASUALA YA  
KISHERIA, SIHITAJI KUHISI  
KWAMBA NIMEOKOKA ILI  
KUOKOLEWA. NI SUALA LA  
KISHERIA.**

yanazungumzia cheo chako cha kisheria katika Ufalme wa Mungu. Yesu ameketi mkono wa kuume wa Baba, nawe pia kwa kuwa wewe ni mwili wa Kristo. Hivyo wewe ni mrithi pamoja na Yesu wa yote aliyo nayo Mungu. Najua ni ajabu kufikiria hilo, lakini ni kweli. Una kila kitu; wewe ni mwanafamilia, na hii ni biashara ya familia! Lakini kwa sababu shetani amejaribu kuficha kila ulicho na kila ulicho nacho, watu wengi, hata Wakristo, wanaishi kama

wale ambao bado wamefungwa na mfumo wa laana ya dunia wa kuishi maisha ya kunusurika!

Jambo muhimu lililobadili maisha yangu ni wakati nilipotambua kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa na ni serikali yenye sheria, na mimi kama raia nina haki na manufaa zake za kisheria. Hisia ni nzuri, na ninapenda kuhisi uwepo wa Mungu, lakini inapohusu masuala ya kisheria, sihitaji kuhisi kwamba nimeokoka ili kuokolewa. Ni suala la kisheria. Sihitaji kujihisi kama raia wa Marekani ili kuwa mmoja wao. Tayari najua ni suala la kisheria linaloridhishwa na ukweli kwamba nilizaliwa Marekani. Unapokuwa katika msimamo sahihi mbele za Mungu, huku maisha yako yakiwa yameegemezwa kwa sheria badala ya jinsi unavyohisi, mambo hubadilika!

*Na huu ndio ujasiri tulio nao Kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*

— 1 Yohana 5:14-15

Tafakari Maandiko haya kwa muda mfupi; ni mojawapo ya yale ninayopenda sana. Nikiomba kitu sawasawa na mapenzi Yake, najua ananisikia! Hii haihusu sauti unayoisikia kwa masikio yako. Hii ni taarifa ya kisheria. Fikiria hakimu aliye katika chumba chake cha mahakama. Hakimu akiamua kusikiliza kesi maana yake amekubali kusuluhisha jambo hilo kwa kuzingatia sheria inavyosema. Kwa upande wetu, kwa kuwa

tumeomba kulingana na sheria za Mfalme, tunajua tayari Yeye atatekeleza sheria Yake mwenyewe. Hivyo, tuna uhakika katika matokeo; hakutakuwa na kubahatisha.

Kwa mfano, Marekani si ufalme kwa kuwa haina mfalme, lakini inaendeshwa kwa sheria zilizo sawa kwa kila raia halali. Vivyo hivyo, Ufalme wa Mungu pia unaongozwa na sheria zilizo sawa kwa kila raia bila ubaguzi. Hadithi tunazosoma katika Biblia hazipo kwa ajili ya kutusisimua tu bali ili kutuonyesha sheria hizo ili tuzijifunze na kuzitumia. Mara nyingi Yesu alitumia maneno haya, “Ufalme wa Mungu unafanana na,” alipokuwa akiwaeleza watu jinsi Ufalme unavyotenda kazi. Yesu alirejelea sheria za Ufalme aliposimulia hadithi, huku akitoa picha dhahiri ya jinsi sheria zinavyofanya kazi au kueleza kwa nini jambo fulani lilitukia. Tena, kwa sababu moja au nyingine, watu hawajui kwamba Ufalme wa Mungu una sheria zinazoongoza utendaji wake. Wengi hufikiri kwamba Mungu anaweza kufanya jambo lolote analotaka kufanya wakati anapotaka kwa sababu Yeye ni Mungu. Ninakubali kwamba Mungu ana uwezo wa kufanya chochote anachotaka kufanya; hata hivyo, amewekewa mipaka na sheria Zake Mwenyewe. Najua hili linaweza kusikika kuwa geni kwako, lakini ili kueleza hoja yangu, hebu tuangalie kwa haraka Marko 6.

*Yesu akawaambia, “Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake.” Wala hakuweza kufanya mwujiza wowote huko, isipokuwa aliweka mikono Yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao.*

— Marko 6:4-6

Uliposoma Maandiko haya, ulipaswa kuona mambo kadhaa ambayo yalikuwa ufahamu dhahiri wa jinsi Ufalme unavyotenda kazi.

### **Hakuweza kufanya mwujiza wowote...**

Kwanza kabisa, Wakristo wengi hawajaona Maandiko haya na watabishana nawe moja kwa moja kwamba umekosea ukisema kuna hali katika Biblia ambapo Yesu hakuweza kuponya. Lakini kama unavyoona, hakufaulu. Mara tu unapoelewa kwamba Ufalme unafanya kazi kupitia kwa sheria, basi unaanza kutazama hadithi hii kwa uangalifu zaidi. Mtazamo wa kawaida wa Wakristo wengi ni kwamba Yesu alichagua kutowaponya. Hilo

linaweza kuonekana kuwa kweli ikiwa huelewi uhalali wa Ufalme. Ukiwa na ufahamu kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kuponya lakini hakufanya hivyo, bila kuelewa mamlaka ya kisheria, bila shaka utakata kauli kwamba aliamua kutoponya. Sababu nyingine ingekuwa nini?

Huenda umesikia mtu akisema, “Mungu aliruhusu hili litendeke,” au “Mungu anajua zaidi,” au “Mungu anayo yote katika udhibiti Wake,” au maneno kama hayo anaporejlea tatizo au ugumu wake au wa rafiki yake. Kwa Mkristo wa kawaida, hapa ndipo anapotia tamati. Bila kujua sheria za Ufalme na ni nini hasa kilichomzuia Yesu, hitimisho lao la pekee ni kwamba haikuwa mapenzi ya Mungu kuwaponya. Rafiki yangu, Biblia haisemi kwamba alichagua kutoponya. Inasema hangeweza kuwaponya kwa sababu ya ukosefu wao wa imani. Mara utakapogundua kwamba kizuizi cha uponyaji katika hadithi hii haikuwa ukosefu wa Mungu wa kutaka kufanya hivyo, utatambua kwamba kulikuwa na sheria za kiroho za mamlaka zilizozuia nguvu za Mungu.

Sasa utanza kugundua katika hadithi zingine kwamba kulikuwa na sababu za kisheria zilizoruhusu mamlaka ya nguvu za Mungu kuleta mapenzi na shauku Yake katika hali fulani au la, kama ilivyo katika hadithi hii. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana kwako kujua jinsi sheria hizi za Ufalme zinavyofanya kazi. Siku moja utakapohitaji mguso kutoka mbinguni, hutataka nguvu za mbinguni zizuiliwe, bali utataka ziwe huru katika kuzalisha mapenzi ya Mungu maishani mwako. Na ndio maana niliandika kitabu hiki.

Ili kuanza safari yako kwa hakika, ningependekeza uanze na ufahamu mpya akilini mwako na utambue kwamba unahitaji kutupa sababu za zamani za kidini ambazo umesikia maisha yako yote kuhusu kwa nini Mungu hufanya au hafanyi jambo fulani. Natumai sasa unajua kwamba unahitaji kukataa maelezo ya kawaida yanayotolewa kuhusu mtoto wa fulani ambaye alikufa katika umri mdogo: “Mungu anajua zaidi, Yeye ndiye msimamizi wa yote,” nk. La, unahitaji KUJUA kwa nini Yesu hakumponya na sheria zinazoongoza mtiririko wa nguvu za Mungu ulimwenguni. Unahitaji kujua jibu kwa swali, “Kwa nini Yesu hakuweza kuponya?” Kwa watu wengi, ukweli kwamba nasema kuna jibu kwa swali hilo huwafanya waudhike. Lakini nakuambia tu kile Biblia inachosema, na hebu nirudie tena kwamba LAZIMA ujue jibu la swali hilo.

Jibu rahisi na fupi linaloeleza kwa nini Yesu hangeweza kuponya katika hadithi ile ni kwamba mbingu haikuwa na mamlaka ya kisheria kufanya hivyo. Mamlaka hayo hutolewa kwa imani na mwanadamu aliye ulimwenguni

ambaye amesadiki kikamilifu kuhusu yale mbingu inayoyasema. Hata ikiwa sisi sote tungekubali kwamba Yesu alikuwa na nguvu na shauku ya kuponya watu, hakuweza kufanya hivyo. Yesu, Mwenyewe alisema kwamba kushindwa Kwake kuponya hakukuwa kwa sababu ya udhaifu Wake bali ni kwa sababu watu hawakuwa na imani. Andika hilo! Kuna jambo muhimu hapo! Imani!

Katika kitabu changu cha awali, nilitumia muda mwingi kueleza maana ya imani, jinsi inavyofanya kazi, kwa nini tunahitaji imani, kwa nini Mungu anahitaji tuwe na imani, jinsi tunavyopata imani, na jinsi tunavyojua ikiwa tuko na imani. Kusema kwamba ufahamu kuhusu sheria hii ya kimsingi zaidi katika Ufalme ni muhimu ni dharau, maana ni uzima na kifo!

Hivi majuzi nilipokea jarida kutoka kwa huduma ya Kikristo inayojulikana sana. Kwa bahati mbaya, yaliyokuwa ndani yake ni mfano wa kile Wakristo wengi wanachoamini. Nitashiriki baadhi ya mambo hayo hapa.

Inaanza na neno nzuri kutoka **Kumbukumbu la Torati 31:6:**

*Iweni hodari na moyo wa ushujaa, msiogope wala msiwahofu; kwa maana Bwana, Mungu wako, Yeye ndiye anayekwenda pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha.*

Kisha inasema...

“Kwa nini Mungu hakomeshi ugaidi na kuteseka? Kwa nini anaruhusu watu wafe? Maswali ni mengi, na ukweli wa mambo ni kwamba hatujui majibu yote. Hatujui kwa nini Mungu anaruhusu mambo fulani kutokea. Kile tunachojua ni kwamba upendo wa Mungu ni mkamilifu. Njia Zake zi juu ya njia zetu. Tunapaswa kuamini ahadi Zake ambazo hazitumbii kwamba hatatupa zaidi ya uwezo wetu, lakini kwamba chochote anachotupa, atakuwa pamoja nasi katika kila hatua.

MAKOSA, MAKOSA, MAKOSA! Biblia inatumbia kinyume na hilo kabisa.

*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*

— 1 Wakorintho 10:13

Ahadi Zake zinatupatia ahadi ya uponyaji, urejesho, ongezeko la kifedha, na mengi zaidi—si ahadi tu ya kuwa na uwezo wa kustahimili magumu au maafa. Upendo mkamilifu hutoa masuluhisho. Ninaweza kuendelea, lakini cha kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo watu wengi wanavyoamini kumhusu Mungu. Jinsi mtu anavyoweza kuthubutu kufikiria kwamba Mungu, ambaye ni upendo mkamilifu, anaweza kumpa mtu ugonjwa wa saratani au kukataa kumponya wakati ana uwezo wa kufanya hivyo ni jambo linalopita ufahamu wangu. Walipoulizwa kuhusu hili, tena, jibu lao la kawaida ni kwamba njia Zake si njia zetu. Je, unafanya mzaha? Sisi hatuna upendo mkamilifu lakini hatuwezi kumfanyia mtoto wetu hivyo! Badala yake, Yeye amefanya njia Zake kuwa wazi mno katika Neno Lake.

Jarida hilo lilidokeza kwamba chochote anachotupa, atakuwa nasi katika kila hatua tunapoteseka. Je, Mungu atatupa kitu kibaya? La. Biblia inapotuambia kwamba yuko pamoja nasi na hatatuacha kamwe, inamaanisha kwamba Mungu yuko pamoja nasi ili kutimiza ahadi Zake! Rafiki yangu, mafundisho haya kwamba Mungu ni adui yetu hayatoki Kwake. Hayamwakilishi Mungu ninayemtumikia, na ninatumai hutayavumilia. Ikiwa kanisa lenu linafundisha upuzi kama huu, unapaswa kuondoka mara moja!

Mungu ni upendo na Neno linasema upendo haushindwi kamwe. Kinachoshindikana, hata hivyo, ni mamlaka ya Mungu, uwezo Wake wa kuingilia kati katika ulimwengu, jambo linalosababishwa na ukosefu wa imani. Kwa mara nyingine tena, hili ni suala la kisheria, wala si suala la kihisia, au kitu kingine chochote. Ni suala la kisheria unalopaswa kujua. Kwa kuwa mwanadamu ana mamlaka ulimwenguni, Mungu hawezi kufanya kile anachotaka, kama nilivyoshiriki awali. Ili kuipa mbingu mamlaka ya kuleta nguvu za Mungu na haki katika hali yako, makubaliano yako na imani yako vinahitajika. Rafiki, **lazima** ujue imani ni nini na kwa nini inahitajika katika kupokea kutoka kwa Mungu.

Iwapo hujasoma kitabu changu cha awali (*Mapinduzi Yako ya Fedha: Nguvu ya Kuwa Mwaminifu*), hebu nizungumzie kwa ufupi imani ni nini. Ingawa unaweza kudhani kwamba karibu kila Mkristo anayetumia neno imani anajua maana yake, labda utakuwa umekosea. Tunahitaji kuwa na

somo dogo la historia ili kuweza kuelewa dhana muhimu ya Ufalme kuhusu mamlaka ya kisheria.

Hebu tuangalie **Warumi 4:18-21**:

*Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyonenwa, “Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.” Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, alifikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), na hali ya kufa ya tumbo lake Sara. Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu; huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*

Ibrahimu anajulikana kama baba wa imani yetu. Alisadiki kabisa kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya yale aliyoahidi. Kusadiki kikamilifu, katika mapatano na Mungu, kunaitwa imani. Bila makubaliano hayo, Mungu hawezi kutenda chochote ulimwenguni. Kwa hivyo unaweza kuuliza, “Kwa nini Mungu anahitaji mtu afanye jambo ili apate ruhusa ya kufanya au kutofanya jambo lolote analotaka? Yeye ni Mungu.” Ili kujibu swali hilo, tunahitaji kutazama upesi hapo mwanzoni, wakati wa Adamu.

*Umemfanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono Yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*

— Waebrania 2:7-8

Maandiko haya yanarejelea Adamu na Hawa wakati wa uumbaji. Tafadhali tambua kwamba hakukuwa na kitu chochote duniani ambacho hakikuwa chini ya mamlaka yao kisheria. Adamu aliwekwa duniani kuitawala dunia akiwa na mamlaka aliyokabidhiwa kwa niaba ya Ufalme wa Mungu. Alitawala dunia nzima.

*Mungu akasema, “Na tumfanye mtu kwa mfano Wetu, kwa sura Yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa*



*kitambaacho juu ya nchi.”*

— Mwanzo 1:26

Hapo tena, tunaona kwamba Adamu alitawala dunia kupitia mamlaka iliyokabidhiwa na alivikwa taji ya utukufu (upako au nguvu) na heshima (cheo chenye mamlaka). Hakuna kitu ambacho hakikuwa chini ya utawala wake. Hakika unaposoma simulizi la uumbaji, Adamu aliwapa wanyama majina, maana alikuwa juu ya dunia yote. Kama tujuavyo sote, Adamu alipoteza mamlaka yake juu ya Shetani, ambaye alimdanganya Hawa na kumshawishi Adamu kufanya uasi dhidi ya serikali ya Mungu. Paulo anasema katika 2 Wakorintho 4:4 kwamba Shetani, kupitia kwa usaliti wa Adamu, alifanyika mungu wa dunia hii. Hakusema yeye ni mungu, bali mungu wa dunia hii, kumaanisha kwamba alikuwa na mamlaka ya kisheria ya kiroho hapa. Ingawa mwanadamu bado alikuwa akiishi duniani, mbele za Mungu alikuwa amekufa kiroho. Roho ya mwanadamu iliyoubwa ili kutembea katika muungano na Roho ya Mungu, sasa ilikuwa imetenganishwa naye. Mwanadamu alianza kuishi kulingana na hisi zake mwenyewe, akili yake, mapenzi yake, na hisia zake.

*Akamwandisha juu, akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, “Nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Basi, wewe ukisujudu mbele yangu yote yatakuwa yako.”*

— Luka 4:5-7

Utaona kwamba Shetani anasema kwamba cheo alichu nacho juu ya makao ya dunia “**alipewa**” yeye. Bila shaka, tunajua kwamba yule aliyempa ni yule aliyekimiliki kihalali hapo mwanzo, ambaye ni Adamu. Hii ni muhimu. Ikiwa hakika Shetani angejaribu kuingia katika ulimwengu kinyume na sheria, angetupwa nje mara moja na kwa lazima. Ikiwa unaweza kufikiria afisa wa polisi anayeitisha chelezo, utaelewa vyema kwa nini ninasema Shetani angelazimishwa kutoka. Beji anayoivaa afisa huyo ina maana kwamba nguvu na mamlaka yote ya serikali ya Marekani yapo ili kuunga mkono maneno yake.

Taji aliyovaa Adamu (cheo alichokuwa nacho), ili kutawala kwa niaba ya serikali ya Mungu, ilileta nguvu zote za Mungu kumpa msaada. Kwa sababu ya cheo cha Adamu duniani, Shetani hakuwa na mamlaka yoyote

katika ulimwengu. Alitawaliwa na Adamu na Hawa. Njia pekee ya Shetani kisheria ya kupata mamlaka duniani ingehitaji Adamu avue taji yake, jambo ambalo Shetani hakuwa na mamlaka ya kumlazimisha kufanya. Shetani alijua mtu pekee ambaye angeweza kuivua hiyo taji kutoka kwa kichwa cha Adamu alikuwa Adamu mwenyewe. Ndiyo sababu ilimbidi Shetani atumie mpango wake wa udanganyifu. Udanganyifu huo ulikuwa nini? Shetani alidokeza kwamba Mungu si wa kutegemewa na hakuwatakia mema. Alimsadikisha Hawa kwamba kulikuwa na faida katika kutomtii Mungu na kwamba sheria za Mungu zilikuwa zikimzuia yeye na Adamu wasipate jambo lenye manufaa.

### **Ilimbidi Shetani awafanye Adamu na Hawa wamwamini au wajipatanishe naye badala ya Mwenyezi Mungu.**

Kwa maneno rahisi, hii ni imani. Imani inaweza kufafanuliwa kuwa “kusadikishwa kikamilifu” kuhusu yale ambayo Mungu anasema. Adamu na Hawa waliacha kuona Neno la Mungu kama kitu cha kutegemewa na badala yake wakakubaliana na yale ambayo Shetani alisema. Kisha wakatenda kulingana na imani yao, jambo lililobatilisha msimamo wao wa haki katika Ufalme wa Mungu na kumpa Shetani nafasi ya kisheria juu ya mambo ya wanadamu. Matokeo? Adamu, ambaye alikuwa na mamlaka juu ya ulimwengu, alimfukuza Mungu kiroho alipojipatanisha na Shetani! Adamu aliacha taji yake, cheo chake cha mamlaka, na kumfuata Shetani. Kwa kufanya hivyo, kimsingi alimfukuza Mungu kutoka kwa maisha yake. Watu wengi wanaweza kusema, “La, haingewezekana; Adamu hangeweza kumfukuza Mungu kutoka duniani!” Lakini ukweli ni kwamba inapohusu masuala ya wanadamu, bila shaka alifanya hivyo. Hebu nikuthibitishie hilo. Tuangalie **Mwanzo 3:17-19** tena. Baada ya Adamu kufanya dhambi, Mungu alimwendea na kumwambia,

*Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

Tazama inasema, “*Ardhi [dunia] imelaaniwa kwa ajili yako.*”

Kulaaniwa kunamaanisha kutokuwepo kwa uwepo wa Mungu na baraka Zake. Adamu, ambaye alikuwa na mamlaka juu ya dunia, ndiye aliyekatiza mamlaka ya kisheria ya Mungu duniani. Kimsingi, Mungu anasema, “Ee, Adamu, kwa sababu yako, mikono Yangu imefungwa. Siwezi kukusaidia.” Kisha akamwambia Adamu kwamba kwanzia hapo yeye ndiye angejinusuru mwenyewe, kwa kufanya kazi nzito yenye dhiki. Ninaita jambo hili “mfumo wa laana ya dunia” wa kunusurika. Hapa ndipo sisi sote tulikulia—katika ufalme wa kunusurika na hofu. Tulijifunza kuwa na wasiwasi, na woga umetawala mawazo yetu tangu tulipozaliwa. Ninataka kurejea kwenye Maandiko haya baada ya muda mfupi ili kujadili zaidi kuhusu mfumo wa laana ya dunia, lakini kwa sasa, nataka kuhakikisha unaelewa jinsi Shetani alivyopata kiingilio ulimwenguni. Nirudie tena, ilimbidi atafute mwanadamu aliyeishi duniani ambaye alikuwa na mamlaka ya kisheria duniani kutoka kwa Mungu ili aweze kumfungulia mlango. Adamu ndiye aliyekuwa na ufunguo, na Shetani aliweza kumdanganya afungue mlango. Sasa, tuangalie Waebrania 2:7-8 tena.

*Umefanya mdogo punde kuliko malaika, umemvika taji ya utukufu na heshima, umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake. Kwa maana katika kuweka vitu vyote chini yake hakusaza kitu kisichowekwa chini yake. Lakini sasa bado hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake.*

— Waebrania 2:7-8

Tazama Maandiko haya yanasema kwamba Mungu hakuacha chochote kisicho chini yake. Ingawa Maandiko haya yanarejelea tukio la zamani, yanatumia neno *kisicho* ambalo liko katika wakati uliopo kuelezea hali ya sasa ya mwanadamu duniani. Ingawa mwanadamu alipoteza mamlaka yake ya kiroho katika ulimwengu kupitia kwa dhambi ya Adamu, hakupoteza makao yake kisheria hapa duniani, na hivyo kuhalalisha utumizi wa neno *kisicho*. Kwa sababu ya cheo cha mwanadamu duniani kisheria, na kwa sababu ya ngome ya kiroho Shetani aliyo nayo kisheria juu ya wanadamu, Mungu hawezi tu kuingilia kati ulimwenguni na kukiuka Neno Lake Mwenyewe au Shetani atadai kutofanyiwa haki.

Inabidi Mungu atumie mwanadamu katika ulimwengu ambaye atakubaliana Naye, jambo ambalo litafungua mlango wa kiroho kwa Ufalme wa Mungu kuwa na mamlaka ya kisheria hapa. Kama vile ilimbidi Shetani amtumie mlinzi wa mlango wa dunia, Adamu, Mungu sasa hana

budi kufanya kazi kupitia kwa wanadamu, ambao ni walinzi wa mlango wa dunia, ili kuleta mamlaka ya Ufalme hapa. Imani ni kusadiki kikamilifu moyoni na akilini mwako kuhusu kile mbingu inachosema. Lazima imani iwepo ili Ufalme wa Mungu uwe na mamlaka hapa. Sitachukua muda hapa kueleza jinsi ya kupata imani au jinsi ya kujua kama una imani. Haya yote yamezungumziwa katika kitabu changu cha kwanza cha mfululizo huu. Kwa madhumuni ya mjadala huu, nataka tu kuhakikisha unajua imani ni nini na kwa nini inahitajika kabla ya mbingu kuingilia kati katika ulimwengu.

Sasa, natumai umeelewa vyema zaidi wa kwa nini Yesu “hakuweza” kufanya miujiza mingi katika mji wake wa asili—watu huko hawakuwa na imani. Kwa hivyo, mbingu haikuwa na mamlaka ya kisheria. Hebu nimalizie mjadala huu na Andiko zuri linaloonyesha kile ninachosema.

Kila mtu amesikia kuhusu Warumi 10:10:

*Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*

Andiko hili ni sehemu ya kile ambacho Wakristo wanakiita njia ya Kirumi, sehemu ya Maandiko manne yanayotonyesha jinsi ya kuokolewa. Lakini je, umetenga muda mfupi kufikiria kuhusu mchakato ambao Warumi 10:10 inakuonyesha? Ni kupitia kwa moyo wako unaamini au kuingia katika makubaliano na mbingu. Moyo wako ukiwa katika mapatano na mbingu unaipa mbingu uhalali wa kuivamia dunia. Maandiko haya yanasema ukiamini, unahesabiwa haki. Haki ni utekelezaji wa sheria. Kwa hivyo kuamini moyoni mwako kunakupa haki ya kisheria mbele ya mbingu na ardhi ya kupokea kile mbingu inachosema kwa sababu hili linaipa mbingu uhalali katika ulimwengu. Lakini tazama, hakuna kinachotokea bado. Kuna sehemu ya pili ya Andiko hili: “...na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.” Wajua, ingawa moyo wako unaweza kukubaliana na mbingu, jambo ambalo linaipa mbingu uhalali wa kuivamia dunia, hakuna kitakachotokea mpaka wewe, mwanadamu uliye na mamlaka duniani, utakapoyaachilia hapa duniani. Kwa nini? Kwa sababu una mamlaka hapa; mbingu haiwezi bila wewe!

*Amin, nawaambieni, yoyote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yoyote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.*

— Mathayo 18:18

Kimsingi, andiko hili linasema kile ambacho nimezungumzia hivi punde. Lolote utakalolifunga duniani, mbingu zitakubali, na lolote utakalolifungua duniani, mbingu zitakubali. Mbingu haziwezi kufanya chochote bila wewe. Mbingu zinakungoja na haziwezi kutenda jambo isipokuwa mtu mwenye imani au mapatano na mbinguni aachilie mamlaka hayo katika ulimwengu.

Kuelewa jinsi ya kuachilia mamlaka na nguvu za mbinguni katika ulimwengu ndiko kunakoleta tofauti kubwa kabisa. Kulileta tofauti maishani mwangu na vile vile katika maisha ya mwenye kuandika barua pepe ifuatayo ambayo nilipokea.

“Habari! Mimi na mume wangu tunataka kushiriki nawe hadithi yetu ya ajabu ya ‘kuwinda kwa imani!’ Mnamo mwaka wa 2011, tulikuwa tukiishi katika ‘nyumba ya ndoto zetu,’ lakini tulikuwa tunaishi mshahara mmoja hadi mwingine na wakati mwingine tulitumia kadi zetu za mkopo kulipia mboga na [kupasha] nyumba yetu joto. Tulikuwa tunaishi lakini hatukuwa tukistawi. Nilikuwa kiongozi wa sifa na kuabudu katika kanisa letu, lakini hatukuelekeza imani yetu kwa fedha zetu. Nilitazama kipindi chako cha *Fixing the Money Thing* katika chaneli ya runinga ya Daystar, ambacho kilivutia umakini wangu, na nikaagiza kitabu, *Fixing the Money Thing*, pamoja na CD za Mapinduzi ya Kifedha. Tulisikiliza CD hizi kila wakati na kusomeana kitabu.

“Hatukujua hatukuwa na imani! Tulifahamu kwamba ili kuhifadhi nyumba hii ya ndoto zetu, tulihitaji majibu fulani kuhusu jinsi suala la fedha linavyoshughulikiwa katika Ufalme. Tulitoa matoleo ya \$200 kama mbegu kwenye huduma ya Faith Life Ministries (ambayo ingekuwa hata \$2,000. Lakini wakati huo, hizo zilikuwa pesa nyingi sana kwetu!) na tukakubaliana na Mungu atuonyeshe ni biashara gani ambayo ningeweza kufanya kutoka nyumbani.

“Mungu alitupatia wazo la biashara la kulea watoto wa mbwa aina ya *Goldendoodle* nyumbani kwetu. Tulinunua watoto wawili wa mbwa, Bella na Gracie, tukawafuga mpaka wakazaa watoto huku tukishirikiana na Mungu. Tulifahamu vyema kwamba hatungeweza kuumba watoto wa mbwa!! Mnamo mwaka wa 2014, mbwa wetu wawili walizaa watoto 13 ambao bei yao ya soko ilikuwa \$1200 kila mmoja. Mwaka huu, 2015, tumekuwa na watoto wa mbwa 63, WOTE wenye afya. Kutokana na kuuza watoto wetu wa mbwa, tumekuwa huru kutokana na madeni yetu yote isipokuwa nyumba yetu. Pia sasa tuna hazina ya dharura iliyofadhiliwa kikamilifu.

“Mama yetu alitushangaza pia alipotuomba ikiwa tungenda kuwafuga mbwa wake wawili aina ya *Goldendoodle* kwa kuwa yeye alikuwa anastaafu! Hivyo Mungu alitubariki na *doodle* wengine wawili bila malipo! Na mnamo Julai, mume wangu alipandishwa cheo na kuwa msimamizi katika shule yetu ya upili ya mtaani!! Katika mwaka mmoja, mapato yetu yaliongezeka maradufu hadi takwimu za sita!! KUWINDA KWA IMANI KUNAFANYA KAZI!! Tilitumia sheria za Ufalme wa Mungu. Sasa, tunatoa matoleo katika kila aina ya kazi ya Ufalme na huwa tunahudhuria kanisa lako mtandaoni kila Jumapili asubuhi kabla ya kwenda kuongoza sifa katika kanisa letu la mtaani! Asante kwa kutufundisha jinsi Ufalme unavyotenda kazi!”

—Karla

Wanandoa hawa walinitumia barua pepe nyingine wiki hii.

“Pasaka njema! Amefufuka! Tilitaka kushiriki sasisho kwa Mchungaji wetu wa mtandaoni Gary! Tafadhali mjulishe tulisherehekea kuzaliwa kwa Yesu huko Yerusalemu mwaka huu (tulilipia pesa taslimu). Tulibarikiwa pia kuwa na kijana wetu Carter aliyebatizwa katika Mto Jordan, na kuabudu pamoja na Hillsong Australia kando ya Bahari ya Galilaya jioni! Ajabu!!! Tunashukuru sana kwamba tumerekebisha mambo ya fedha!

Kufikia sasa tumekuwa na watoto 121 wa mbwa. Ilitubidi tuongeze bei ya mbwa hadi \$2,300 kwa sababu orodha ya watu waliokuwa wakingojea ilikuwa ndefu sana! Bwana asifiwe.”

—Karla

Huu ni mfano bora wa kile Ufalme unachoweza kufanya maishani mwako. Nilimpigia Karla simu wiki baada ya kupokea barua hii naye alifurahi SANA!!! Alisema nyumba yao ingelipwa mwaka huo huo. Ukiangalia barua pepe ya kwanza aliyotuma, alisema yafuatayo (ambayo yamenukuliwa kutoka kwa barua pepe iliyo hapo juu):

“Tulikuwa tunaishi mshahara mmoja hadi mwingine na wakati mwingine tilitumia kadi zetu za mkopo kulipia mboga na [kupasha] nyumba yetu joto. Tulikuwa tunaishi lakini hatukuwa tukistawi.”

Sasa, baada ya miaka michache tu, wangeilipia nyumba? Ufalme!



## SURA YA 3

# UFALME NDIO JIBU LAKO

Sasa kwa kuwa una ufahamu wa kimsingi kwamba Ufalme hufanya kazi kwa sheria na kanuni zisizobadilika kamwe, nataka kuanza kuangazia sheria ambazo kweli huathiri fedha na, hatimaye, pumziko.

Lakini kabla hatujaenda huko, nataka kufafanua kwa nini nilikiita kitabu hiki *Nguvu ya Kupumzika* na ninachomaanisha ninapotumia neno *kupumzika* katika muktadha wa fedha na Ufalme. Ajabu ni kwamba, si mimi niliyeanzisha dhana hii ya kuhusisha pumziko na fedha, bali ni Mungu.

*Basi mbingu na nchi zikaamalizika, na mwonekano wao wote mkubwa wa kuvutia. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi Yake yote aliyofanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyofanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyoiumba na kuifanya.*

— Mwanzo 2:1-3

Kwanza, acha niweke jambo hili wazi: Mungu hakupumzika siku ya saba kwa sababu alikuwa amechoka. Mungu hachoki. Alipumzika kwa sababu, kama andiko linavyosema, kila kitu kilikuwa kimekamilika naye alikuwa amemaliza kazi. Alimuumba mwanadamu mwishoni mwa siku ya sita ya uumbaji ili aishi katika siku ya saba. Siku ya saba haikuwa na mawazo ya woga, fikra za manusuru, ugonjwa, wala kazi yenye dhiki au kutokwa jasho ili kupata riziki. Badala yake, mawazo ya Adamu yangehusu Mungu, mke wake, kazi na kusudi lake. Kila kitu alichohitaji ili kutegemeza kazi



yake na maisha viliandaliwa na kupatikana; mpango wa Mungu ulikuwa umekamilika. Watu leo huota ndoto ya kuwa na kile Adamu alikuwa nacho, kuishi bila wasiwasi, kuwa na uwezo wa kuzingatia shauku zao na mahusiano bila kujali kuhusu riziki. Cha kusikitisha ni kwamba, Adamu alipoasi, alipoteza riziki ya Mungu, na tangu wakati huo mwanadamu alilazimika kukimbiza (kwa dhiki na jasho) vitu anavyohitaji ili kuishi.

*Kwa maana hayo yote Mataifa huyatafuta; kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji hayo yote. Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*

— Mathayo 6:32-33

Uzito wa kutafuta riziki ni mzigo mzito na hupotosha mtazamo wa maisha wa mwanadamu. Watu wanaota kuwa matajiri, na kuwa huru kutokana na matakwa ya kuishi yenye dhiki na kutokwa jasho. Kuwa milionea kunadhaniwa kuwa muhimu kwa kuwa na uwezo wa kupunguza dhiki na uzito wa kutafuta riziki, na hivyo kuturuhusu kuzingatia kusudi na kazi yetu. Bahati nasibu ni maarufu sana kwa sababu inaleta riziki bila kazi na kuepuka mfumo wa kifedha wa laana ya ardhi. Miradi ya utajiri wa haraka imeenea kwa kila namna na mara kwa mara hushambulia barua pepe zetu na machapisho yetu kwenye Facebook. Kwa hiyo katika muktadha kuhusu fedha zetu, tunahitaji kujibu swali: Je, kuna njia ya kurejea siku hiyo ya saba ambapo kila kitu kiko kamili na shwari na kinapatikana? Jibu ni NDIO kubwa! Kusudi la kitabu hiki ni kueleza jinsi hilo linavyoweza kutokea na kuleta ufahamu wa sheria za Ufalme zinazosababisha matokeo ya aina hiyo. Najua uzoefu wako maishani au hata kanisa na Wakristo wanaweza kubishana kwamba ninachosema si kweli, maana Wakristo wengi wamekumbatia theolojia inayosema “umaskini ni utakatifu.” Lakini ninakuhakikishia kwamba majibu yote unayohitaji ili kustawi na kudumu katika kazi yako, na kukupa fursa ya kugundua kusudi la kuumbwa kwako, yako katika Ufalme.

*Heri ninyi mlio maskini, kwa sababu Ufalme wa Mungu ni wenu.*

— Luka 6:20

Jibu la kuwa maskini liko katika Ufalme! Hili ndilo andiko la kwanza

ambalo Mungu alinionyesha alipoanza kunifundisha sheria za Ufalme kuhusu fedha. Bila shaka, ili kufahamu dhana hii, itabidi ufahamu maana ya dhana ya ufalme, ambayo tayari nimeshaitaja. Na ninafikiri lazima uwe na ufahamu dhahiri wa kile kilichotokea kwenye Bustani Adamu alipotenda dhambi. Kwa hivyo hebu nipitie hayo kwa muda mfupi.

Hapo mwanzoni, Adamu na Hawa hawakuwa na wasiwasi juu ya kitu chochote; hakuna ugonjwa au masuala ya riziki yaliyowasonga akilini mwao kila siku. Kila siku, kile walichopaswa kufikiria tu ni kazi yao, ambayo ilikuwa ni kumpenda Mungu, kupendana, na kutunza dunia na Bustani Mungu aliyowapa. Hofu haikuwepo kabisa maishani mwao. Lakini Adamu alipoasi, bila shaka kila kitu kilibadilika. Kama nilivyosema tayari, Shetani alifanyika mungu wa ulimwengu huu, mwanadamu alitengwa na Mungu, na mamlaka ya Mungu ya kisheria juu ya mwanadamu yalitupiliwa mbali. Adamu alishtushwa na ukweli mpya wa jinsi maisha yalivyoanza kufanya kazi. Kwa mara nyingine tena, haya ndiyo maneno ambayo Mungu alimletea Adamu baada ya kutenda dhambi.

*Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.*

— Mwanzo 3:17-19

Sasa mtazamo wa Adamu na Hawa ulifanyika wa manusuru wenye mawazo ya dhiki, kutokwa jasho, kujawa woga, na wasiwasi. Kusudi la kuumbwa kwao, ambalo lilikuwa mpango wa Mungu kwa ajili yao, sasa lilipotea katika mbio na vita vya kuwa hai. Kazi kuu ya Adamu na kusudi lake, sasa ilikomesha na mahangaiko ya maisha na hitaji la riziki. Alipoteza ufahamu wa yeye ni nani. Kusudi pekee aliloweza kuona sasa ni kuwa hai, jambo ambalo lilihitaji kazi ngumu na jasho kila wakati. Hakuna mengi yaliyobadilika tangu siku hiyo hadi leo.

Leo, mimi kama mchungaji, nimeona kwamba swali nyeti ambalo watu huniuliza ni, “Ninapaswa kufanya nini na maisha yangu?” Wanauliza kwa sababu katika ulimwengu tangu Adamu, kutafuta riziki ndio lengo ambalo kila kitu kingine kinapimwa. Maamuzi kawaida hufanywa kwa msingi wa pesa na sio kusudi. Pesa na uhitaji wake zinaweza kuwalazimisha watu kufanya kazi wanazochukia. Kwa kweli, watu wengi hawajui wao

ni nani hasa. Andika hili chini, “Mpaka umjue Mungu, hutawahi kujua mpango Wake kwa maisha yako. Yeye ndiye aliyekuumba.”

Watu wana njaa sana ya kujua wao ni nani. Katika ulimwengu wanaonekana kuwa idadi tu, lakini kwa Mungu wao ni kiumbe spesheli na cha kipekee chenye ujuzi na uwezo ambao hakuna mwingine anao. Lakini kwa sababu hawamjui Mungu na, hivyo, hawajitambui, wanatafuta thamani yao katika sehemu zisizofaa. Wanaruhusu utamaduni kuamua thamani yao kwa kukubali kile ambacho utamaduni unasema. Lakini taswira inayoonyeshwa na vyombo vya habari na utamaduni huo vyote ni vivuli vinavyobadilika-badilika. Wakati unafikiri unapiga hatua kulingana na kile kinachokubalika, utagundua kwamba utamaduni umebadilika na tayari uko nyuma.

Nakumbuka nikitembea barabarani na Drenda huko Paris. Paris bila shaka, inajulikana kwa mitindo ya mavazi; na mtindo wa mwaka huo ulikuwa wa mavazi yenye rangi ya kijivu na nyeusi. Kila dirisha la maduka yao lilionyesha mavazi yenye rangi hizo tu. Nilipotazama barabarani, pande zote mbili, niliona mamia ya watu wakitembea. Nilishtuka kwamba sikuona hata chembe ya rangi yoyote tofauti. Kila mtu alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya kijivu na nyeusi. Mamia na mamia ya watu walionekana sawa. Ni lini mara ya mwisho mtu alikuambia kwamba rangi aliyoipenda ni ya kijivu? Lakini siku hiyo, watu wengi walikuwa na uhakika kwamba rangi waliyoipenda ilikuwa ya kijivu au nyeusi.

Kwa sababu shinikizo la kutafuta riziki ni kubwa sana na linapotosha utambulisho wetu kwa chochote tunachofikiri kitatusaidia kuipata na kwamba tutakubalika, mimi na Drenda tulianzisha msembo ambao tumekuwa tukihubiri kwa miaka mingi: “Usiposuluhisha suala la fedha, kamwe hutagundua hatima yako!” Kuwa mtumwa wa kutafuta jinsi ya kuishi hakuruhusu wakati wa kutosha wa kuchunguza au kuunda njia zingine. Ukweli ni kwamba, kama nilivyoshiriki tayari, mara nyingi watu hufanya maamuzi yao wakiwa na lengo la kutafuta au kuhifadhi riziki. Wanatupilia mbali shauku yao kwa sababu ya kulipwa mshahara kila mwezi na maono yao kwa sababu ya kupata riziki. Ukweli ni kwamba tumeshinikizwa sana na hali yetu ya mawazo ya unusuru yenye dhiki na jasho jingi kiasi cha kuacha kuota. Hofu imeteka nyara ndoto zetu, na ukosefu wa riziki umetia ndoto zetu katika gereza la yale yasiyowezekana.

Nakumbuka wakati ndoto yangu ilikuwa kuwa na pesa za kutosha kununua mafuta ya gari ili kuweza kufika nyumbani, usihesabu kuwa na pesa za kutosha kushughulikia kitu muhimu maishani. Katika siku hizo,

hakukuwa na maono makuu mawazoni mwangu. Nilitumia mawazo yangu yote katika kulipa kodi ya nyumba kila mwezi. Ninakubali kwamba ni vigumu kuwa na mtazamo ila ule wa manusuru wakati umebanwa sana na ukosefu wa chakula au unaposhinikizwa na matatizo ya kifedha.

Adamu alipopoteza Ufalme, ulimwengu mpya kabisa wa kifo, hofu, unusuru, na kushambuliwa na woga uliteka maisha yake. Nina hakika sisi sote tunajua hisia ya hofu. Ninakumbuka hadithi nyingi maishani mwangu niliposhambuliwa na woga, aibu, na hofu kwa miaka tisa mirefu katika janga la kifedha, na hatimaye kuanza kunywa madawa ya kutuliza mashambulizi hayo. Kuishi katika mfumo wa laana ya dunia kumetuzoeza sisi sote kuwa na mtazamo mbaya kuhusu maisha. Watu wengine huushughulikia vyema zaidi kuliko wengine, lakini bila Kristo, mtazamo huu mbaya huendelea kutuambia sisi hatufai vya kutosha.

Je, umewahi kusikia mtu akisema, “Usiwe na matumaini mengi?” Nilipokuwa nikikua, ikiwa nilifurahia jambo ambalo babangu alifikiri ni la kipumbavu, alikuwa akisema, “Siku moja utakua.” Kwa sababu hiyo, kwa kawaida sikujiruhusu kuota chochote isipokuwa kile ambacho baba yangu aliona kilikuwa hitaji. Nafikiri babangu aliumizwa alipokuwa akikua katika nyumba ya walevi, na ndivyo alivyopaswa kufanya pia.

Kusema kweli, sisi sote tumekuwa wataalam katika kuwa na wasiwasi tangu kuzaliwa kwetu. Hofu ni lugha ya kawaida ya ulimwengu. Ikiwa utatulia na kutafakari juu yake, neno la limesukumwa ndani yetu tangu tulipozaliwa. “La, hutakuwa na hilo.” “La, rudisha hicho.” “La, hutaenda huko.” “La, huwezi kumudu hilo.” Hatimaye, tunaacha kusema “Ndio” kwa chochote isipokuwa mara kwa mara tunapotoroka ili kufanya shughuli inayopunguza mashinikizo katika akili zetu tusione hali zetu halisi, kama vile kula chakula chetu tunachopenda.

Uchunguzi mmoja unakadiria kwamba mtoto wa kawaida husikia neno *la* au *usifanye hivyo* zaidi ya mara 148,000 anapokua, lakini anasikia *ndio* mara elfu chache tu.

Hivi majuzi nilifanya kongamano letu la Utoaji wa Riziki wa kila mwaka, na kwenye jukwaa niliweka gari aina ya Ferrari ya 2017, ambalo ni gari la kupendeza hakika. Mmiliki wa gari hilo ni mshirika wa kanisa langu na alililipia pesa taslimu, ambayo ilikuwa karibu \$400,000. Watu wote waliohudhuria kongamano walipowasili, walishangaa na kulitazama gari lile, huku wakitaka kulitazama kwa ukaribu. Lakini ingawa wote walistaajabia gari hilo, jambo nililokuwa nikiweka dhahiri kwa kuliweka jukwaani halikuwa kuwachochea wawe na maisha yenye malengo ya

kujiwekea vitu, bali ni kuwafundisha somo. Watu wote walikusanyika karibu na gari, wote wakisema wangependa kuliendesha.

Nilijua mafundisho ya “la” waliyokuwa wamepokea katika mfumo wa laana ya dunia ya kazi nzito yenye dhiki na jasho jingi yalikuwa yakipiga kelele akilini mwao, “LA, hutawahi kumiliki gari kama hilo! La, kamwe hutaweza kumudu gari hilo; hata usifikirie juu yake.” Kwa sababu ya mafundisho ya “LA” waliyoyapata, na sote tumeyapata, wengi wao hawakuwahi hata kufikiria kumiliki Ferrari kwa sababu mtazamo wa “la” haungeweza kuiona au kuipokea. Lakini ikiwa ningendelea kubadilisha magari kila saa, kutoka ghali hadi ya bei nafuu, hatimaye, ningekuwa na gari kwenye jukwaa ambalo wangepfikiria na kusema, “Ninapenda gari hilo; ninapaswa kupata moja kama hiyo.”

Tofauti ilikuwa nini? Ilikuwa jinsi walivyojiona, uwezo wao, na gharama ya gari. Naam, huenda kulikuwa na wachache pale ambao walijiambia, “Nitamiliki gari hilo siku moja,” au pengine kulikuwa na watu waliokuwa na pesa na waliona gari hilo kwa njia tofauti. Lakini nina hakika kwamba kwa watu wengi, kumiliki gari kama hilo hakukuwa katika mawazo yao. Milionea aliyelipia gari hilo pesa taslimu ana Ferrari sita. Mtazamo wake ni kwamba hilo ni gari nzuri tu. Alipoona gari hilo, alifikiria kulimiliki na akaliagiza kutoka Italia, kisha likasafirishwa hadi nyumbani kwake Marekani. Haikuwa vigumu kwake kutenda kulingana na maono yake kwa sababu alikuwa na riziki. Hapa kuna kipengele muhimu kuhusu pumziko—riziki hutolewa kwa ajili ya kutekeleza maono.

## **Jambo Kuu Muhimu:**

### **Riziki Hutolewa kwa ajili ya Kutekeleza Maono**

Bila riziki huwezi kuwa na maono; bali utaishi tu. Mfumo wa laana ya dunia wa umaskini umeiba ndoto na hatma zetu. Najua Ferrari ilikuwa kielelezo kikubwa lakini ilitoa hoja yangu. Watu waliohudhuria kongamano hawakujiruhusu hata kuota kuwa na gari kama hilo kwa sababu waliliona kama jambo lisilowezekana. Ikiwa wangepjiruhusu hata kwa muda mfupi kuwa na ndoto ya kuimiliki, mafundisho yao ya mfumo wa laana ya dunia yangewapigia kelele na kuwaambia, “Hilo ni jambo la kutupa pesa!” Lakini vipi ikiwa ungekuwa na dola bilioni 25 pesa taslimu katika akaunti yako (ninatoa hoja tu)? Gari hilo lingonekana kuwa la bei nafuu sana hivi kwamba ungelinunua ili kulitumia wikendi tu. Hili ni suala la mtazamo tu,

na kwa kuwa Neno la Mungu linasema kila ahadi ya Mungu ni, “Ndio” na “Amina (na iwe hivyo),” mtazamo wako unahitaji kubadilika ili ufikiri jinsi Mungu anavyofikiri.

*Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika Yeye ni “Ndio;” tena kwa hiyo katika Yeye ni “Amin;” Mungu apate kutukuzwa kwa sisi.*

— 2 Wakorintho 1:20

Kulingana na kamusi, ufafanuzi wa mtazamo ni: nia au njia fulani kuhusu jambo; fikra, njia ya marejeleo, au kuelewa jambo. Kimsingi, mtazamo ni jinsi hasa unavyofikiri juu ya jambo fulani.

Hapa kuna dhana nataka utafakari. Adamu alikuwa mwana mfalme kabla ya kukubaliana na Shetani. Kwa hiyo baada ya kitendo hicho, ungemwona kama mtu masikini mwenye familia mbovu (Kaini, mwanawe, alimuua nduguye, Abeli), na kwa kweli usingempa nafasi ya kuwa mtu wa maana. Lakini kile ambacho hungiona ni kwamba alikuwa na ufalme katika mishipa yake. Ingawa hungemwona hivyo, alikuwa ameumbwa kutawala na kuwa na mamlaka maishani. Ukweli huu unakuhusu pia. Hupaswi kujiangalia mwenyewe kulingana na mahali unapoishi, kile ulicho nacho, na hali yako ya sasa, na kufanya uamuzi kuhusu uwezo wako. Lazima uangalie uwezo uliombwa nao.

Ninakumbuka nilipokuwa nikipitia hali ngumu, na kukabiliwa na masuala makubwa yaliyoonekana kuwa mazito kuniliko. Nilikabiliwa na maamuzi yaliyohitaji pesa nyingi zaidi kuliko zile nilizokuwa nazo mkononi. Nilihisi kwamba nilijua kile ambacho Mungu alikuwa akiniambia nifanye, lakini bado nilikuwa na woga kidogo kukitekeleza

## **MTAZAMO WAKO UNAHITAJI KUBADILIKA ILI UFIKIRI JINSI MUNGU ANAVYOFIKIRI.**

haraka. Bwana alinipa ndoto wakati huo. Nilikuwa nimepanda farasi juu ya kilima. Nilikuwa na upanga mkononi mwangu. Chini yangu katika kilima hicho kulikuwa na mamia, ikiwa si maelfu, ya askari-jeshi maadui waliokuwa juu ya farasi na panga zao zilikuwa zimeinuliwa dhidi yangu. Nilikuwa peke yangu katika kile kilima na hakika walikuwa wengi sana. Sauti katika ndoto yangu ilisema maneno haya, “Usijidharau, Gary!” Niliposikia hilo, niliinua upanga wangu na nikaanza mbio na farasi wangu kuelekea chini ya kilima kwa maadui wangu ambao sasa walipoona nikielekea kwao, walianza mbio pia kupanda

kilima kuelekea kwangu huku wakiwa wameinua panga zao. Nilipokuwa nikikimbia kuelekea kwao, nilisema kwa sauti kubwa, “THOR!”

Nilipoamka, nilijua Bwana alikuwa akizungumza nami kunitia moyo, lakini sikujua neno *Thor* lilimaanisha nini. Nina mshirika katika kanisa langu ambaye amekuwa mchungaji kwa miaka 30 na amesoma lugha nyingi. Nilimuuliza kama alifahamu maana yake naye akaniambia kwamba angefanya uchunguzi. Alinipigia simu siku iliyofuata na kusema kwamba *Thor* ilimaanisha mwana wa radi. Nilimshukuru na nikashangazwa na kile ambacho Bwana alikuwa akiniambia. Kwa adui, husikika kama radi! Isipokuwa nimwambie shetani kwamba mimi ni mdhaifu, ninapozungumza, kwake yeye ninasikika kama ngurumo (nguvu) la radi.

Nilisimulia hadithi hii nilipokuwa nikihubiri katika Kongamano letu la kwanza kabisa la Utoaji wa Riziki mwaka wa 2010. Niliposimulia hadithi hii, nilihitimisha kwa kile Bwana alichoniambia katika ndoto, “Gary, adui anapokuona ukija, huwa unasikika kama ngurumo la radi.” Kisha nikasema, “Inasikika kama ngurumo la radi,” makofi makubwa ya radi yalijaa hewani. Hakukuwa na mvua, hakukuwa ngurumo lolote lingine la awali, lakini hiyo ndiyo sauti pekee tuliyoisikia jioni nzima. Watu waliokuwa hapo jioni hiyo walishtuka. Lakini hakuna mtu aliyekuwa na furaha zaidi kuniliko mimi, maana nilijua ni Bwana aliyekuwa akiweka, “AMINA” Yake juu ya kile nilichokuwa nikisema kuhusu watoto Wake wote. Wala usitie shaka, kamera za runinga zilikuwa zikifanya kazi yao usiku huo, na ikiwa ungependa kuona tukio hilo unaweza kwenda kwa anwani ya mtandao ifuatayo: <https://youtu.be/rtx1XYJGIag>.

Kwa hivyo dhana unayohitaji kuelewa ni hii hapu.

## **Watumwa hawaoti ndoto kubwa!**

Watumwa huota kuhusu nini? Kukoma, ndivyo ilivyo. Wao hutazama saa zao alasiri nzima huku wakiota juu ya saa kumi na moja ya jioni, kwa kutaka kumaliza kazi na kuondoka. Wao huota kuhusu likizo, kustaafu, na kuwa na pesa ili waweze kuacha kazi. Watumwa huota ndoto ya kuacha kazi, wala si ya kuanzisha kazi nyingine! Mtazamo au mawazo ya utumwa huwa haubuni au kuanzisha kazi; unatafuta njia ya kutoka kwa kazi. Mtumwa tayari amezidiwa na haoni uwezekano wa mambo yanayopita karibu naye kila siku.

Ili kuwa kichwa na sio mkia, mtazamo wako wa akili lazima ubadilike kutoka kuwa mtumwa hadi kuwa mmiliki na muundaji. Lazima uanze

kuota tena. Unahitaji kuona kwamba wewe ni zaidi ya yale unayofikiria kujihusu, maana ingawa unaweza kuonekana mdhaifu machoni pako, kwa shetani unasikika kama ngurumo la radi. Una damu ya kifalme katika damu yako, na unahitaji kufikiri na kutenda kulingana na hilo.

Nina rafiki tajiri mwenye mamilioni mengi. Ana nyumba nyingi za kifahari kwenye mabahari au maziwani. Siku moja nilipokuwa nikimtembelea, tulikuwa tukitembea katikati ya mashua kwenye bandari. Tulipokuwa tukipita kila mashua, alinitajia jina la mwenyewe. Nitakupa mfano wa jinsi mazungumzo yalivyokuwa, lakini nitatumia majina mengine, kwa kuwa siyakumbuki. Kwa hivyo mazungumzo na rafiki yangu yalienda kama hivi: “Mashua hii ni ya Billy Smith, anayemiliki Huduma ya Matibabu ya Ohio. Mashua hii inayofuata inamilikiwa na John Rogers, ambaye anamiliki Rogers na Rogers, ambayo ni kampuni ya sheria. Mashua hii inayofuata ni ya Ralph Tidewell, ambaye ni mmiliki wa duka lile zuri la viatu lililoko katika barabara ya High Street.

Tulipotembea katikati ya mashua hizo, baada ya kupita karibu 20, niligundua kwamba kila moja yao ilikuwa ya mtu aliyemiliki biashara. Hakuna hata mashua moja iliyokuwa inamilikiwa na mtu wa kawaida ambaye alikuwa akifanya kazi saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni katika duka la aiskrimu. Sasa, sina shida na mtu anayefanya kazi katika duka la aiskrimu la eneo lake na sipingi kuwa mfanyakazi. Kile ninachokupa tu ni mfano wa aina ya watu walio na mali.

Tafadhali zingatia sana ninachosema. Hili halihusu pesa walizonazo; linahusu mtazamo wa akili walio nao. Usielewe mambo kwa mpangilio usio sawa. Watu wengi wanaweza kusema, “Laiti ningekuwa na pesa kama hizo.” Wanachopaswa kusema ni “Laiti ningefikiria kama wao!” Wana mtazamo tofauti kuhusu maisha na wao wenyewe.

Familia nyingi hazifikii mapato ambayo yanaweza kuonwa kuwa mapato mengi. Utafiti wa sasa unasema 51% ya wafanyakazi wa Marekani wanapata chini ya \$30,000 kwa mwaka. Zaidi ya nusu ya taifa letu hupata chini ya \$30,000 kwa mwaka?! Ikiwa uko katika miaka yako ya ishirini na ndio unianza au unafanya kazi mahali fulani kwa sababu unataka kuwa hapo, na pesa si muhimu sana kwako basi sawa, lakini najua hiyo sio kweli kwa zaidi ya nusu ya taifa. Najua watu wanahitaji pesa zaidi. Niamini, nimetembelea maelfu na maelfu ya familia kwa miaka yangu 36 katika sekta ya huduma za kifedha, na nimejionea.

Kwa hivyo kwa nini hawana mapato zaidi? Kabla hujaanza kupiga kelele jinsi maisha yasiyo ya haki au jinsi wewe ni mhasiriwa au upuuzi mwingine



wowote, nitawasilisha kwako kwamba ni kwa sababu mbili. Kwanza, wamenaswa chini ya mfumo wa laana ya dunia wa umaskini na hawajui Ufalme wa Mungu na kanuni Zake za kupata riziki. Pili, wana mawazo potofu kwa sababu ya mafunzo ya laana ya dunia ambayo wamekuwa nayo, na hawaoni njia ya kutokea, ingawa njia inaweza kuwa imesimama mbele yao. Kimsingi, watumwa wana mawazo ya utumwa, kama nimekuwa nikishiriki. Hawaoni fursa zilizo mbele yao wakati wanatafuta pumziko. Tuseme ukweli; watu hukata tamaa pasipo na majibu ya kweli.

Hebu nikupe mfano ninaoutumia kwenye semina zangu. Tuseme nikwambie kwamba ninaweza kutatua shida zako zote za pesa kwa sentensi moja rahisi. Tayarisha penseli na karatasi yako kwa sababu ninakuhakikishia kuwa hili litakuwa jibu lako. Tayari? Sawa, ndilo hili hapa: kuwa na mapato halisi ya dola milioni 5 mwaka huu. Ninaposema hivyo kwenye jukwaa, kila mtu huanza kucheka. Lakini kwa nini wao hucheka? Kwa sababu hawawezi kujiona wakipata pesa za aina hiyo, wala kufikiri kwamba wana uwezo wa kuwa na mapato halisi ya dola milioni 5 kwa mwaka.

Kisha huwa ninawaambia kwamba hawatamiliki kamwe wasichoweza kuona. Kisha ninarudia zoezi hilo, lakini wakati huu ninapunguza idadi kila mara: \$200,000, \$100,000, \$70,000, au \$40,000 kwa mwaka. Hatimaye, ninawaambia, “Nitafika kwa idadi ya pesa ambayo mtasema, “Sawa, rahisi. Naweza kufanya hivyo.”

Kisha huwa ninawaambia hadithi nyingine. Tuseme kwamba mimi ni mfanyabiashara tajiri katika biashara ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Ninataka kusafirisha mipira hadi Uchina, na ninahitaji usaidizi wa kuifunga ili isafirishwe. Ninawaambia nitawalipa \$500 kwa kila mpira watakaofunga. Tuseme wanaweza kufunga mipira 200 kwa siku, hiyo itawaletea takriban \$100,000 kwa siku. Pia tuseme ningependa kuwapa mkataba wa mwaka mmoja wa kufunga mipira kwa malipo hayo hayo. Sasa, ikiwa ningewaambia suluhu lao ni kutengeneza mapato halisi ya dola milioni 5 katika miezi 12, majibu yao yangekuwaje? “Rahisi, hakuna shida, mtu anaweza kupata dola milioni 5 kwa malipo kama hayo.”

Tofauti ni nini? Mpango, ni hilo tu. Mpango huleta tofauti kubwa. Mungu aliyekuumba anajua mpango huo, na kile unachohitaji tu ni kuusikia kutoka Kwake. Ndivyo ilivyo katika Ufalme wa Mungu. Wakati Mungu alinipa ndoto ya kuanzisha biashara na kisha kunionyesha jinsi ya kuifanya, mapato yangu yalikuwa bado hayajabadilika—lakini nilikuwa nikipaza sauti ndani yangu, “Hii ni rahisi! Shida zangu za pesa zimeisha; nina mpango!”

*“Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi,” asema Bwana, “ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.”*

— Yereimia 29:11

Mungu ana mipango ya kukufanikisha! Mara tu unapogundua kwamba Mungu ana mpango wa mafanikio yako, nusu ya vita vimekwisha! Sikiliza, kusuluhisha suala la pesa sio jambo gumu sana. Riziki hutolewa kwa ajili ya maono! Ni kweli ni rahisi sana. Suluhu la kutokuwa na mboga ni kuwa na mboga. Suluhu la hitaji la nyumba kubwa ni kuwa na nyumba kubwa zaidi. Suluhu la kuwa na gari la kuaminika ni kumiliki gari linaloaminika.

Najua maneno yangu yanaweza kusikika kana kwamba yana utata, lakini mimi niliendesha gari bovu kwa miaka mingi. Ungeweza kuniona nikija kutoka umbali wa maili moja kwa sababu gari langu lilifuatwa na moshi mahali popote nilipoenda. Ninajua jinsi matatizo ya gari yanavyoweza kuwa wakati unahitaji kufika mahali fulani. Pia najua jinsi unavyohisi unapoingia kwenye duka la kuuza magari na kulipia gari jipya pesa taslimu. Wajua nini? Hakuna dhiki wala wasiwasi tena. Kwa nini? Kwa sababu hitaji langu limetimizwa na nina amani. Ninaweza kuzingatia kile ninachopaswa kufanya badala ya kushughulikia shida ya gari.

Ukweli wa mambo ni kwamba watu wengi hulazimika kushughulikia suala la pesa halisi hadi wanakuwa chini ya shinikizo maishani mwao. Wanaweza kuwa wanafanya kazi kwa masaa mengi sana wakijaribu kujikimu kiasi cha kutoishi maisha jinsi inavyofaa. Rafiki, haya si mapenzi ya Mungu kwa maisha yako.

Kama nilivyosema awali, watu hutipilia mbali ndoto na shauku zao kwa mshahara wa kazi wanazodharau. Watumwa kwa kawaida si watu wenye furaha sana! Jambo la kusikitisha ni kwamba, hapa ndipo watu wengi hudumu, katika huzuni, chukizo, na bila matumaini na hali yao ya maisha.

**KAMA RAIWA WA UFALME,  
UNA HAKI ZA KISHERIA,  
NA KILA SHERIA NA  
KANUNI SASA ZIPO KWA  
AJILI YAKO.**

Lakini ukweli ni kwamba, wanahitaji mabadiliko madogo tu katika mtazamo wao ili kuwa huru au, kama nilivyoshiriki hapo awali, kuwa na mpango.

Hebu nikupe mfano wangu binafsi. Wengi wenu mnajua kwamba ninapenda kuwinda na kuvua samaki, kuendesha

pikipiki na kwenda milimani, chochote kinachohusu kwenda nje ya nyumba. Nililelewa Ohio katika jumuiya ndogo ya wakulima kwa eneo linalojulikana kama Plain Township. Uliitwa Mji wa Tambarare maana haukuwa na milima yoyote. Bila shaka, hilo lilikuwa jambo nzuri kwa wakulima, lakini haikuwa mandhari ya kuvutia hata kidogo. Nilijiandikisha kwa kila jarida la uwindaji na uvuvi ambalo ningeweza kama vile, *Outdoor Life, Sports Afield, Field & Stream*, na mengineyo. Nilikuwa nikisoma hadithi nzuri za uvuvi na uwindaji mwituni na milima ya kupendeza upande wa magharibi, na milima yenye rangi ya kijani kibichi iliyo katika Bonde la Appalachian lililo umbali wa saa moja tu upande wa mashariki kutoka kwetu. Hata hivyo sikuwa nimewahi kutembelea maeneo hayo. Nilikuwa na umri wa miaka 40 kabla ya kuona mlima wangu wa kwanza.

Kwa nini? Nilikuwa na pesa za kusafiri, nilikuwa na gari langu mwenyewe, barabara kuu ya I-70 inapita katikati ya mji wetu, na njia ya kuelekea upande wa magharibi inapitia Rocky Mountains. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba sikuwahi kufikiria hata mara moja kwenda huko au hata kujiruhusu kufikiria, “Nitaenda huko siku moja.” Nilistaajabia sehemu hizo kupitia kwa picha zilizong’aa kwenye majarida lakini sikufikiria kwenda huko. Kulingana na mimi haijalishi hata kama wangu kwa mwezi; hilo halikuwa jambo lililowezekana akilini mwangu. Nilipofika umri wa miaka 40 na hatimaye kusafiri kuelekea magharibi, sikuamini nilichokosa maisha yangu yote. Sasa, lazima nipande mlima angalau mara moja kwa mwaka. Rafiki, kuna mengi huko nje kuliko yale unayoyaona sasa hivi. Wewe una mengi ndani yako kuliko yale unayoyaona sasa hivi! Kuna mtazamo tofauti wa maisha ambao unahitaji kuona na kupata.

**Unapoanza kuelewa na kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi na yale ambayo Ufalme wa Mungu unasema tayari unayo, mtazamo wako utabadilika!**

*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani Mwake Mungu.*

— Waefeso 2:19

Kama raia wa Ufalme, una haki za kisheria, na kila sheria na kanuni sasa zipo kwa ajili yako. Hili hasa ndilo lililokuwa shida ya Drenda na mimi. Ingawa tulikuwa Wakristo na tulimpenda Mungu, tulikuwa raia wa Ufalme

wa Mungu wasio na ujuzi wowote kuhusu sheria na kanuni za Ufalme Wake. Kwa sababu ya mitazamo yetu midogo tuliyopewa na mfumo wa laana ya dunia, hatukuwa na ndoto. Lakini maarifa ni nguvu.

Kwa mfano, katika mahakama, mkataba wa kukodisha uliotiwa saina unathibitisha kuwa una haki ya kisheria ya kuishi katika nyumba yako. Una amani na faraja katika ufahamu kwamba una hati iliyotiwa saina na una haki kisheria kuishi katika nyumba yako. Vile vile, kujua yale ambayo Mungu anasema na yale yaliyopo katika Ufalme kwa ajili yako kunakupa uhakika wa kutwaa kila kitu kilicho chako kisheria. Kwa mfano, ustawi wa mkulima ni nini? Je, ni pesa? La. Je! ni mbegu anayopanda? La. Ni ujuzi alionao wa sheria za kupanda na kuvuna. Hata awe maskini kiasi gani, anajua jinsi ya kuwa tajiri. Yeye anapaswa tu kujiingiza katika sheria za ulimwengu ambazo Mungu ameweka. Mchakato wa kupanda mbegu na kuvuna unaweza kumzalishia mkulima tena na tena.

Mkulima anaelewa sheria za mavuno na ana imani kamili nazo. Yeye hupanda mbegu yenye thamani ya maelfu ya dola ardhini, wala haogopi. Huwezi kumpata mkulima akiwa ameketi karibu na trekta lake mara baada ya kupanda mbegu zake akilia juu ya pesa zote alizotupa ardhini. La, hawezi kulia juu ya gharama ya mbegu. Yeye ana uhakika na sheria za ulimwengu wa asili. Je, anaweza kukuambia jinsi mbegu inavyomea? Sidhani, lakini anaweza kukuambia kuwa anatafuta ardhi zaidi ya kulima. Ndivyo ilivyo kwako na mimi. Tusipojua sheria za Ufalme na kuzitumaini, hatuwezi kufurahia maisha ambayo Mungu amekusudia tuishi.

Mojawapo ya hadithi za kuisimua zaidi tuliyoshuhudia siku hizo za mwanzoni ilitukia nilipopigiwa simu na mtu nitakayemwita “Don,” ambaye alikuwa akikabili matatizo makubwa ya kifedha. Alikuwa amesikia kwamba nilisaidia watu na masuala ya fedha zao.

Nilipokutana na Don kwa mara ya kwanza, alikuwa amekuja ofisini kwangu akiwa amevunjika moyo sana na kusongwa na shinikizo la madeni. Hakuna kitu kilionekana kuwa sawa katika maisha yake wakati huo. Nilipoketi na kuzungumza naye, niligundua kwamba alikuwa nyuma kwa miezi mitatu hadi minne kwenye kodi yake ya nyumba na karibu kila bili aliyokuwa nayo. Kulikuwa na matatizo ya ndoa—mke wake alikuwa amechoshwa na hali yao ya kifedha na alikuwa ameanza kupoteza heshima kwa Don kwa kuwa hakuweza kumtunza yeye na watoto wao watano. Ukweli ni kwamba Don alikuwa ameacha kujiheshimu, na alikuwa na maswali mengi.

Kazi aliyokuwa nayo wakati huo ilihusisha kuuza bima ya afya katika

Jimbo lote la Ohio, lakini kutofaulu kwake kulimfanya aingie katika janga la kifedha.

Licha ya mambo yote kwenda kinyume na Don, niliona uwezo ndani yake. Alikuwa tayari kujifunza na kufanya kazi. Mambo hayo mawili yenye nguvu yalinivutia vya kutosha kumwajiri na kujiwekeza katika ustawi wa maisha yake ya baadaye. Mwishowe, uwekezaji huo ulileta faida kubwa kwetu sote.

Kampuni yangu changa ilikuwa imeshinda safari ya kwenda Hawaii kutoka kwa mmoja wa wachuuzi wetu, na nilihisi hii ingekuwa fursa nzuri ya kushiriki na Don kuhusu Ufalme wa Mungu. Ingawa Don alikuwa Mkristo, hakuwa na ufahamu kama wangu. Na ingawa nilijaribu mara kadhaa kushiriki naye kanuni za Mungu katika eneo hili, alionekana kutoamini nilichokuwa nikisema.

Niliendelea kutafuta njia ya kumvutia Don ambayo ingemsaidia kutambua kwamba yeye pia angeweza kufaulu kupitia kwa kujifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi. Lakini Don alikuwa na moyo uliovunjika sana kiasi kwamba ilikuwa vigumu kwake kujiamini na kuamini kwamba mabadiliko yanaweza kutokea kweli. Nilijua safari hii ya Hawaii ilikuwa fursa yangu.

Majuma machache kabla yetu kuondoka, mimi na Don tulizungumza kuhusu mambo ambayo tungeona na kufanya huko Hawaii. Nia moja maalum ilivutia umakini wa Don. Alitaka kukamata samaki aina ya *marlin* mwenye rangi ya samawati katika maji masafi ya Bahari ya Pasifiki. “Hawaii ndio mji mkuu wa *marlin* wa rangi ya samawati duniani,” Don aliniambia kwa furaha. “Sikuzote nimetamani kumkamata samaki huyo; imekuwa ndoto yangu.” Kwa mara ya kwanza baada ya majuma mengi, niliona mwangaza machoni pa Don. Jambo fulani lilimsisimua, na nilijua msisimko wake ungefungua mlango wa kujifunza jambo muhimu.

“Don,” nikasema, “je, unafahamu unaweza kuwa na uhakika, sio kutumaini, bali *kujua* kwamba utamkamata *marlin* huyo wa rangi ya samawati huko Hawaii kwa kuingia katika Ufalme wa Mungu?” Akiwa amechanganyikiwa lakini akiwa na shauku, Don alitaka kujua mengi zaidi, nami nikaendelea na maelezo yangu kuhusu Ufalme. Nilinukuu andiko la Marko 11:24 linalosema, “*Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*” Kwake Don, hili lilikuwa jambo zuri sana hakuamini. Nilichukua muda kumsaidia kuelewa Ufalme na jinsi ya kuachilia imani yake. Na hivyo, kabla ya kuondoka kwenda katika safari yetu, yeye na mke wake walisali

kwa makubaliano na kuamini kwamba walikuwa wamepokea samaki huyo wa rangi ya samawati. Pia walitoa matoleo kama mbegu ya kifedha katika Ufalme wa Mungu kwa ajili ya mavuno yao. Hili lilikuwa jambo ambalo Roho Mtakatifu alikuwa amenifundisha kufanya nilipoachilia imani yangu kwa ajili ya chochote nilichohitaji.

Tulipokuwa tuingoja kusafiri, Don alifanya kila alichojua kufanya ili kuhakikisha apate mavuno yake. Alifanya utafiti kuhusu mashua na malipo yaliyohitajika na hatimaye akachagua nahodha ambaye alijisikia vizuri naye. Kila kitu kilikuwa tayari, nasi sote tukafurahi sana kwenda Hawaii kwa maji ya rangi ya samawati.

Siku ya kuvua samaki ilifika, na tulipokuwa tukipanda mashua, tulimwambia nahodha kwa furaha kwamba siku hiyo tungemkamata *marlin* wa rangi ya samawati. Ingawa alitarajia tuwe na siku yenye mafanikio ya kuvua samaki wengine, alituhakikishia kwamba hakukuwa na uwezekano mzuri kwetu kumkamata *marlin* wa rangi ya samawati siku hiyo. Yeye kama mmiliki wa mashua mbili na wafanyikazi wake katika miezi minne ya uvuvi hawakuwa wamekamata zaidi ya *marlin* mmoja wa rangi ya samawati. Hii ilikuwa kwa sababu huo haukuwa msimu wa *marlin* maana samaki hao huhama kwenda kwa sehemu nyingine. Bila kukata tamaa, tulimwambia kwa heshima kwamba siku hiyo tungemkamata samaki huyo na tukaendelea kuandaa vifaa vyetu.

Baada ya saa sita za kuvua hatukukuwa na ishara hata moja kwamba tungemkamata samaki huyo, na nilianza kuwa na wasiwasi kwamba hilo lingedhoofisha imani ya Don. Katika wasiwasi yangu nilimrushia swali. “Don,” nikasema kwa sauti kubwa kutoka mahali nilikuwa nimeketi kwenye daraja lililokuwa juu yake, “hebu nikuulize swali. Ulipokea *marlin* wako wa rangi ya samawati lini? Itapojitokeza au tulipoomba?” Don alijibu kwa sauti ya kujiamini na nguvu, “Gary, hiyo ni rahisi. Nilimpokea nilipoomba.” Nilifurahi na kupata uhakikisho niliposikia jibu lake. Hapo ndipo nilipojua Don alikuwa ameyapa maagizo yangu uzito uliostahili na alikuwa amedhamiria kumkamata samaki huyo.

Baada ya dakika chache, kamba ya nyavu ya Don ilianza kutoa sauti huku ikiinama kuelekea baharini na wenzake walisema kwa sauti kubwa, “Samaki!”

“Usisimke sana,” nahodha alionya. “Ni samaki mkubwa sawa, lakini sio *marlin* wa rangi ya samawati. Samaki hao huja juu kabisa na kuruka angani kwa nguvu lakini samaki huyu amekaa ndani ya maji kabisa. Dakika zilizidi kuyoyoma huku Don akiendelea kupambana na yule samaki ambaye bado

hakuwa amekaribia juu ya maji ili kuweza kuonekana. Jinsi Don alivyokuwa amechoka, samaki pia alikuwa amechoka hata zaidi na punde tu aliacha kupigana. Don na mimi hatukustaajabu wakati alipomvuta marlin huyo mkubwa, wa kupendeza na wa rangi ya samawati ndani ya mashua, lakini kila mtu mwingine kwenye mashua alipigwa na butwaa.

Picha ya Don na samaki wake iko ofisini mwangu hadi leo kama ushuhuda kwa wengine na ukumbusho wa mara kwa mara kwangu kuhusu ukweli wa Ufalme. Kwa watu wengine, alikuwa samaki tu. Lakini kwa Don, samaki huyo alimaanisha mambo makuu zaidi. Ikiwa Ufalme ulifanya kazi ilipohusu *marlin*, bila shaka ungefanya kazi kwa kila kitu kingine alichohitaji maishani. Kwake Don, huo ulikuwa mwanzo tu wa kutambua matokeo ambayo Ufalme wa Mungu ungeweza kuwa nayo katika maisha yake.

Ninapenda hadithi hii, na ninapenda kuona watu wakiwa na mapitio halisi katika Ufalme wa Mungu. Hili ndilo ninalokutakia pia!

## SURA YA 4

# SAMAKI MKUBWA

Sote tuna funguo aina mbalimbali za nyumba zetu, magari yetu, na chochote tunachotaka kulinda. Ufunguo unatupa kiingilio kwa kile tunacholinda au mamlaka ya kutumia kitu, kama vile gari. Kule kuishi kama Mkristo kwa miaka tisa katika janga la kifedha na kukata tamaa, nilijua kwamba kulikuwa na ukosefu au shida fulani. Hakuna aliyehitaji kuniambia hivyo. Nilihitaji kujua shida ilikuwa wapi na jinsi ya kuitatua.

Bwana aliponena nami nilipomlilia anisaidie huku nikiwa nimelala juu ya kitanda changu katika lile nyumba kuukuu mashambani, aliniambia tatizo langu lilikuwa kwamba sikuwa nimewahi kujifunza jinsi Ufalme Wake unavyofanya kazi. Katika sentensi hiyo moja nilipata ufunguo, au niseme mahali pa kupata ufunguo au funguo nilizohitaji—Ufalme. Mungu alikuwa ananiambia kwamba jibu langu lilikuwa katika Ufalme Wake. Sikuwa nimechukua wakati kujifunza jinsi Ufalme Wake ulivyotenda kazi, lakini ikiwa ningefanya hivyo, ningepata jibu langu. Mungu aliponena nami siku hiyo kwamba sikuwa na ufahamu kuhusu Ufalme, kwa kweli sikujua alimaanisha nini. Lakini nilimsikia kwa udhahiri kabisa kwamba ikiwa ningejifunza jinsi Ufalme Wake unavyotenda, ningepata majibu niliyokuwa nikitafuta. Kwa hiyo kwangu, ufunguo mkuu ulikuwa katika taarifa hiyo ya jumla, “Hujapata kamwe wakati wa kujifunza jinsi Ufalme wangu unavyofanya kazi!” Bila shaka, kauli hiyo yenyewe ilisema mengi na ilikuwa ufunguo wangu wa kwanza wa kuona mabadiliko maishani mwangu.

*Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani Mwake;*



*naye ataitwa jina Lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi Yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme Wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo.*

— Isaya 9:6-7

Kuelewa kwamba Ufalme wa Mungu kwa kweli ni ufalme unaofanya kazi kwa misingi ya serikali na sheria kulifungua macho yangu kwa ufahamu wa Ufalme ambao sikuwa nimewahi kuujua hapo awali. Kufahamu kwamba Ufalme wa Mungu ulianzishwa na unaimarishwa na haki (utekelezaji wa sheria) na uadilifu wa Mungu (sheria Zake) kulinionyesha kwamba kila jambo linalotendeka katika Ufalme huo ni matokeo ya sheria au kanuni ya Ufalme Wake. Huenda nisiwe kisu chenye ncha kali zaidi kwenye kabati, lakini nilikuwa mwerevu vya kutosha kuelewa kwamba ikiwa Ufalme huendeshwa kwa msingi wa sheria basi ingefaa nijifunze sheria hizo na kuzitumia maishani mwangu. Mungu alipoanza kunifunulia na kunifundisha mimi na Drenda sheria Zake, nilianza kutambua kwamba kila hadithi katika Biblia ina funguo ninazohitaji kujua kuhusu jinsi Ufalme unavyofanya kazi. Nilianza kusoma kila hadithi katika Biblia kwa njia tofauti: “Kwa nini jambo fulani lilitokea? Kwa nini halikutokea?” Nilisoma kila hadithi kwa mtazamo wa, “Ni kanuni gani zimefunuliwa katika hadithi hii? Hilo lilifanyikaje?”

Nilianza kujitita mwanasayansi wa kiroho, na nilifurahia Roho Mtakatifu aliponifunulia sheria baada ya sheria. Nilifurahi hata zaidi kuona kwamba sheria nilizogundua zingefanya kazi maishani mwangu kama zilivyofanya katika Biblia. Watu huniuliza, “Gary, unamaanisha nini kuhusu sheria za Ufalme?” Kwa kawaida mimi huwakumbusha sheria zote tunazotumia hapa duniani—sheria ya mvuto wa ardhi, sheria za fizikia, na sheria zote za kiasili.

Mkulima hutumia sheria hizi wakati wowote anapotaka; halazimiki kuomba ili zifanye kazi. Zinafanya kazi kila wakati anapochagua kuzitumia. Ziko tayari kutumiwa na mtu yeyote anayetaka kuzitumia. Vivyo hivyo, Ufalme wa Mungu hufanya kazi kupitia kwa sheria ambazo tunaweza kujifunza. Kwa kuwa ni sheria, hazibadiliki kamwe, na tunaweza kujifunza kuzihusu na kuzitumia katika maisha ya Ufalme.

Hakika, mara tu unapokuja kwa Kristo, wewe ni raia wa Ufalme Wake,

na Ufalme wote ni wako. Unaweza pia kujifunza sheria hizi za Ufalme na kuzitumia.

“Sawa,” watu huniambia, “Nimeelewa hilo lakini nipe mfano wa sheria katika Ufalme.” Kuna sheria nyingi mno. Nimekwisha andika juu ya sheria chache, kama vile sheria ya mamlaka, sheria ya imani, na sheria ya mapatano, ingawa sikuziita hivyo katika sura za awali. Tena, kuna sheria nyingi, na sheria hizi zote zinaweza kugawanywa kulingana na kazi na jinsi zinavyotumika, jambo ambalo bila shaka tunahitaji kuzingatia. Hebu nikupe hadithi ili kusaidia kufafanua kile ninachosema.

Nina ndege aina ya Piper Mirage, ambayo huwa ninatumia ninaposafiri kwenda kwa mikutano, biashara na kukutana na wateja. Nilikuwa na safari ya kwenda Colorado kuhudhuria mkutano na nilikuwa nimepanga kwa uangalifu kwamba ndege ifanyiwe ukaguzi ili ifanyiwe marekebisho kama ilivyohitajika kisheria kila mwaka kabla ya safari hiyo. Ikiwa hujui, kila ndege inayosafiri nchini Marekani inahitajika kufanyiwa ukaguzi mara moja kila mwaka. Rubani wangu alifaa kwenda kuchukua ndege kisha aje kutupeleka kwa mkutano wetu. Lakini siku moja kabla ya kwenda kuichukua, waliokuwa wakiifanyia ukaguzi walipiga simu na kusema kwamba walikuwa wamevunja kioo cha mbele cha rubani-mwenza kimakosa. Walisema kwamba wangeibadilisha bila malipo, lakini mchakato huo ungeongeza siku tatu zaidi kabla ya ndege kusafiri. Hiyo ilimaanisha kwamba mimi na Drenda tungelazimika kusafiri kwa ndege nyingine hadi Colorado. Sina kusudi la kulalamika, lakini kila mara tunapendelea kusafiri kwa ndege yetu popote tunapoenda inapowezekana. Tulivunjika moyo kidogo lakini tulisafiri kwenda kwa mkutano. Lakini tulipanga kwamba rubani wetu aje kutuchukua katika safari yetu ya kurudi Ohio.

Baada ya siku mbili katika mkutano wetu, mvua ya mawe ya ghafla ilipiga eneo hilo. Mawe hayo yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba yaliharibu eneo lote. Katika maeneo mengine, vipande vikubwa vya barafu vilipitia paa za nyumba. Mamia ya magari yaliharibika yasingeweza kukarabatiwa. Majengo na paa ziliaribiwa. Rubani wangu alipokuja kutuchukua, aliegesha ndege mahali pale pale ambapo tungeiacha ikiwa tungesafiri nayo kwenda kwa mkutano. Tuliona jambo la kushangaza. Kila ndege iliyokuwa imeegeshwa mahali pale ilikuwa imevunjwawunjwa na mawe ya mvua. Ndege yangu, kwa neema ya Mungu, haikuwepo na hivyo haikuharibika. Hadithi ya kushangaza ajabu, lakini hilo lilifanyikaje? Je, ilikuwa bahati nzuri tu au ndege hiyo kutokuwepo ilikuwa ni matokeo ya sheria ya kiroho ambayo kwa jinsi fulani nilinufaika nayo?

Naam, najua kwa hakika kwamba ilikuwa ni matokeo ya sheria ya kiroho niliyokuwa nimetumia, ambayo nitashiriki nawe baada ya muda mfupi. Kuelewa sheria kunakupa fursa ya kuitumia tena katika hali yoyote unapoihitaji. Katika tukio hili, nilitumia sheria ambayo Mungu alikuwa amenifundisha zamani alipoanza kunipa uzoefu katika sheria na utendaji wa Ufalme Wake.

Hebu nikupe sheria ambayo Mungu alinipa, kisha nitakueleza jinsi nilivyoitumia. Kumbuka, kila hadithi katika Biblia ina jambo fulani kuhusu Ufalme na jinsi unavyofanya kazi. Mimi hujiita mwanasayansi wa kiroho. Kila ninaposoma Biblia, mimi hutafuta sheria zilizosababisha jambo fulani kutokea au kutotokea. Hadithi inayohusiana na somo hili inapatikana katika Marko 6.

*Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi wake walimwendea, wakasema, "Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula." Akajibu, akawaambia, "Wapeni ninyi chakula." Wakamwambia, "Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula?"*

*Akawaambia, "Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame."*

*Walipokwisha kujua wakasema, "Mitano, na samaki wawili." Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*

— Marko 6:35-44

Hii ni hadithi na kielelezo kizuri kinachoonyesha Ufalme wa Mungu ukifanya kazi. Mikate mitano na samaki wawili kulisha watu 20,000?! Lakini umesema Gary kwamba, "Biblia inasema kulikuwa na wanaume 5,000 tu huko." Naam, lakini lazima iwe kwamba kulikuwa na wanawake na watoto huko pia. Ndio sababu nafikiri kwamba labda kulikuwa na watu karibu 20,000 huko.

Wanafunzi walipokuja kwa Yesu kuhusu suala la chakula, Yesu alitaka kuwafundisha jambo fulani kuhusu Ufalme kwa hivyo alisema, “Ninyi wapeni chakula.” Naam, hilo liliwashtua sana. Wangepata wapi chakula kiasi hicho? Walimjibu kwa ufahamu wa chanzo pekee cha riziki walichokijua—kazi! Walisema, “Hilo lingechukua miezi minane ya ujira wa mtu!” Kwa mtazamo wao wa mapato ya masaa ya kawaida ya kazi chungu na mfumo wa laana ya dunia wa kutokwa jasho, ingekuwa vigumu kuwalisha.

Lakini katika Ufalme, sheria mbalimbali za utendaji hufanya mambo yote yawezekane. Yesu alitaka kuwasaidia watupilie mbali mfumo wa laana ya dunia na kujifunza uwezekano mpya kutoka kwa Ufalme wa Mungu. Kisha Yesu akawaambia waende kutazama ni kiasi gani cha chakula walichokuwa nacho ili kulisha umati. Walienda kuangalia kisha wakamjibu kwamba walipata mikate mitano na samaki wawili lakini walijua hiyo haingetosha kuwasaidia. Yesu aliwaomba mikate hiyo na samaki. Alishika chakula hicho mikononi Mwake, akakiombea na kukibariki. Kisha akakirudisha kwa wanafunzi Wake ili wawagawie umati. Bila shaka unajua mwisho wa hadithi; watu wote 20,000 walikula wakashiba na bado vikapu 12 vilibaki.

Maswali yangu ni: “Kwa nini Yesu aliomba aletewe chakula hicho kabla ya kuwaambia wakigawe? Kwa nini Yesu hakuwaambia wanafunzi wakigawe mara tu walipokipata? Je, ilibidi Yesu aibariki kwanza?” Jibu sahihi ni kwamba Yesu alipaswa kubariki mkate na samaki kwanza. Wajua, chakula hicho kilikuwa ulimwenguni chini ya mamlaka na utawala wa wanadamu wanafunzi Wake walipokipata mara ya kwanza. Kwa hivyo, Yesu hakuwa na mamlaka juu yake. Lakini kilipoletwa kwake kwa hiari, aliweza kukibariki. Neno *kubariki* linamaanisha kutakasa au kutenga. Sasa, sheria ya Ufalme iliyofunuliwa ndio hii hapa.

### **Yesu alipobariki mkate na samaki, chakula hicho kilibadili falme.**

Kimsingi, mamlaka juu ya mkate na samaki yalibadilika. Sasa Mungu alikuwa na haki ya kisheria ya kuzidisha mikate na samaki kwa ajili ya umati.

### **Ikiwa Yesu hangechukua chakula hicho na kukibariki, hakingeongezeka.**

Hii ndio sheria tunayotumia tunapobariki chakula chetu, ingawa nafikiri watu wengi hawatambui kile wanachofanya hasa wanapoombea chakula chao. Lakini kwa ufupi, tunapoombea chakula chetu, kinabadili

falme, na hivyo kumruhusu Mungu atulinde na kitu chochote chenye madhara tunapokila. Nahitaji kuongeza dokezo hapa. Tukiendelea kula kwa hiari vyakula visivyofaa na vitu ambavyo tunajua ni vibaya kwetu, tutavuna tunachopanda. Lakini tukila kitu hatari, tusichotambua kwamba kitatudhuru, Neno la Mungu hutulinda kama vile lilivyoilinda ndege yangu. Simaanishi maombi ya kitamaduni ambayo watu wengi huomba chakula chao. Bali kusali kwa imani, kumshukuru Mungu kwamba ameondoa magonjwa katikati yetu hutupa sisi fursa, kama raia wa Ufalme Wake mkuu, kufurahia ahadi Zake.

*Hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa.*

— Marko 16:18

Ili kupata pumziko katika ulimwengu wa leo, tunahitaji tumaini la ulinzi wa Mungu. Kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuiba amani yetu kila upande, ikiwa ni pamoja na chakula tunachokula. Niamini, fahamu kwa uhakika kwamba Shetani ana njama ya kuiba afya yako na uwezo wako wa kuwa na ufanisi dhidi yake katika ulimwengu kwa njia ya chakula!

Tunaweza kuona mfano mwingine kuhusu kuleta matatizo yetu, masuala, amani yetu ya akili, hakika kila kitu kilicho maishani mwetu chini ya mamlaka ya Ufalme katika Wafilipi 4:6-7.

*Msijisumbue kwa neno lolote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi moyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*

— Wafilipi 4:6-7

Tunaposali kuhusu jambo fulani, tunaleta tatizo au suala hilo chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu. Tusipoomba, mikono ya Mungu imefungwa. Hivyo Biblia inasema ombeni bila kukoma (1 Wathesalonike 5:17) na hamna kitu kwa kuwa hamwombi Mungu (Yakobo 4:2).

Niliponunua ndege yangu na kila ninaponunua kitu chochote, mimi hukiombea, huku nikiweka mikono yangu juu yake, na kukiweka chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu ili kutimiza yale yaliyokusudiwa kinapotumikia Ufalme wa Mungu na kazi yangu. Kwa sababu hii, Shetani na wafuasi wake hawaruhusiwi kugusa ndege yangu. Hakuna ubaya wowote utakaonipata nikiwa ndani ya ndege hiyo!

Takriban mwezi mmoja uliopita, nilikuwa nikiendesha ndege yangu kutoka Houston hadi Ohio baada ya kongamano. Ilikuwa jioni tulipokuwa tukipita sehemu zenye giza mashambani. Radi ilianguza anga kwa mbali upande wetu wa kulia na kushoto huku dhoruba ikiendelea kuzunguka nchi pia. Hilo lilitufanya tubadilishe njia yetu ili kuepuka dhoruba hiyo, na kwa sababu hiyo, tulitumia mafuta mengi kuliko tulivyokuwa tumepanga. Kwa hivyo ili kuhakikisha kwamba tumefika nyumbani salama na kutii kanuni za Shirika la Usafiri wa Anga kuhusu kuwa na akiba ya mafuta kwenye ndege, tuliama kusimama Louisville, Kentucky, ili kununua mafuta. Tuliua tukiwa na galoni zipatazo 30, lakini tulikuwa tumebakisha saa nzima kabla ya kufika nyumbani na hatukutaka kupungukiwa. Tuliingia kwenye sehemu ya kuegesha ndege kisha tukawaomba watuwekee mafuta galoni 20 kwa tanki mbili moja upande wa kulia na nyingine wa kushoto katika mabawa ya ndege. Jumla ya kiasi cha mafuta ingekuwa galoni 70, ambazo zilitosha kutupeleka hadi Ohio kwa kuwa ndege yangu hutumia takriban galoni 22 kwa saa.

Tulipokuwa tukiingia kwenye sehemu ya kuegesha ndege, msichana mmoja wa ofisi lao alituuiliza kama angepiga simu ili mafuta galoni 40 yaletwe. Aliposema hivyo, mtu anayesaidia ndege kupaa au kutua pale katika uwanja wa ndege alikuja na makaratasi kuhusu ununuzi wetu. Msichana huyo alichukua makaratasi hayo kutoka mikononi mwake, akayatazama, kisha akasema, “Kuna jambo lisilo sawa hapa. Hesabu hizi hazilingani.” Yule mtu akasema aliweka mafuta na kwamba angerekebisha hesabu baadaye. Msichana akajibu, “Sawa,” lakini akasema hadi wakati hesabu zingerekebisha, hangenipa risiti lakini angetutumia kupitia kwa barua pepe. Tukasema, “Sawa,” na tukatoka nje kuelekea kwenye ndege pamoja na yule mtu. Rubani wangu alimwomba yule mtu ahakikishe kwamba kweli alikuwa ameweka galoni 20 kila upande wa mabawa, naye akasema, “Ndio, nimeweka galoni 20 kila upande.”

Kwa hiyo tuliondoka kuelekea Ohio, na kama dakika 40 kwenye ndege, ghafula, tanki la kushoto liliisha mafuta. Tulishtuka; hilo lingewezekanaje? Baada ya dakika moja, tanki ya kulia liliisha mafuta pia. Ilikuwa ni usiku wa manane wenye giza kuu, na tulikuwa angani futi 15,000. Ni nini kilitokea? Tulikuwa tumeweka mafuta muda mfupi awali. Watu huniambia, “Je, ndege yako haina vifaa vya kupima kiasi cha mafuta?” Bila shaka, vipo lakini vipimo vya mafuta vya ndege yetu hupanda juu polepole tunapoongeza mafuta. Ikiwa umewahi kuendesha gari ya zamani aina ya *Suburban*, labda utaelewa ninachozungumzia. Vifaa vyake vya kupima mafuta hupanda

polepole mafuta yanapoongezwa.

Kwa hivyo rubani wangu alimuuliza yule mtu moja kwa moja kama alitia mafuta kwenye ndege na kiasi alichoweka. Sisi wenyewe tulimwona akiwa na lori la mafuta karibu na ndege huku akiweka mafuta. Rubani wangu alihakikisha alipoona lori la mafuta likiweka mafuta ndani ya ndege na akathibitishiwa kwa maneno mara mbili kwamba jumla ya galoni 40 ziliwekwa kwenye ndege. Kwa kawaida, mara tu tunapothibitisha kwamba mafuta yapo, huwa tunatumia kipimo cha dijitali kupima utumiaji wa mafuta yetu hadi asilimia kumi ya galoni inapobaki. Tulifikiri tumefanya kila tulichohitaji kufanya kwa upande wetu ili tuwe salama.

Tulitangazia uwanja wa ndege wa Greater Cincinnati kuhusu hali yetu ya dharura na tukalazimika kutua huko, jambo ambalo kwa kweli halikuwa tatizo maana tulikuwa juu ya uwanja huo tanki zilipokauka, lakini lilikuwa tukio la kusisimua kwa hakika. Tuligundua baadaye kwamba hii ilikuwa mara ya kwanza ya mtu yule kuongeza mafuta kwa ndege. Alikuwa ameweka galoni 2 kwenye kila tanki, wala sio 20. Hakujua kusoma mita. Kweli? Na hiyo ndiyo kazi pekee ambayo kampuni hiyo ya kitaifa hufanya—kujaza ndege mafuta—ajabu kweli!

Adui alichomaanisha kuwa dhara kwetu hakikuwa suala, lakini ingeweza kuwa dhara kubwa ikiwa mafuta yangekwisha tukiwa mahali pengine popote isipokuwa kwa futi 15,000. Lakini pia, adui hawezi kunidhuru mimi au ndege hiyo. Ili kuzuia tukio lingine la adui yetu, tangu wakati huo tulibadilisha baadhi ya taratibu zetu wakati wa kuongeza mafuta. Sasa hatumwachii mfanyikazi wa uwanja wa ndege kuongeza mafuta bila sisi kuwa pale naye, huwa tuko makini katika vituo vyote vya kuongeza mafuta. Tukio hilo lingekuwa baya ikiwa tungekuwa chini zaidi na kuendesha polepole kwenye njia ya ndege au katika hali mbaya ya hewa; lakini bila shaka, haikuwa hivyo maana nina agano la ulinzi.

Matukio haya yote mawili kuhusu usalama wa ndege yangu pamoja na mimi mwenyewe, yalikuwa ni matokeo ya agano langu, haki zangu za kisheria katika Ufalme. Bila shaka ninaweza kukuambia hadithi ya jinsi nilivyopata ndege hiyo hapo awali, lakini sitaweza sasa hivi. Nafikiri umeelewa—Mungu ni wa ajabu!

Kuna sheria za Ufalme unazopaswa kujifunza ili uwe na ufanisi,

usalama, na kupata riziki hapa ulimwenguni. Shetani anatuchukia, lakini hawezi kutuzuia, Mungu asifiwe. Ulinzi pia ni pumziko, hakuna wasiwasi wala hofu! Ni haki yako kisheria.

Sheria hii ambayo nimeielezea na kutumia ndiyo ninayoita sheria ya mamlaka, ikiwa hujui.

*Andiko lingine ambalo Mungu alinipa hapo mwanzo kuhusu  
Ufalme Wake ni*

— Luka 6:20.

Mara ya kwanza Bwana alipotuonyesha andiko hili, mimi na Drenda tulianza kujifunza kile Mungu alichomaanisha aliposema “ufalme wa Mungu.” Pia, alituonyesha kwamba Yeye ni mfalme wa ufalme unaotawaliwa na kufanya kazi kupitia kwa sheria. Kwa mfano, tuangalie mpaka wetu wa Kusini. Kila mwaka, maelfu ya watu hujaribu kuingia Marekani kisiri. Kwa nini? Je, ni kwa sababu hawana mandhari nzuri wanakoishi? La, bila shaka siyo. Wanajaribu kuja Marekani kwa sababu ya serikali hapa. Serikali yetu ina sheria zinazolinda haki za watu na kutoa uhuru mwingi usio katika mataifa mengine: umiliki wa mali, haki ya kumiliki biashara yako mwenyewe, haki ya kuabudu upendavyo, na uhuru wa kujieleza. Yote haya hayapatikani katika mataifa mengine mengi.

Tayari tumezungumza mengi kuhusu Ufalme wa Mungu, msingi wa funguo, kanuni, na sheria zote ambazo Mungu ametupa kama raia. Ujuzi wako au ukosefu wa ujuzi wa sheria hizi unaweza kusababisha uhai au mauti, ushindi au kushindwa. Baada ya kuteseka kwa miaka tisa katika hofu ya kifedha inayodhoofisha na sasa kuwa huru, siwezi kusesitiza vya kutosha jinsi ilivyo muhimu kujua maana ya kuwa raia wa Ufalme wa Mungu na umuhimu wa kujua sheria na kanuni zote zinazofanya kazi katika Ufalme Wake.

Dunia imekuwepo kwa maelfu ya miaka, lakini mambo mengi tunayofurahia leo hayaeleweki. Kwa mfano, nataka uwe na picha jinsi ilivyokuwa siku ya mkasha wa Krismasi mwaka wa 1906 huko Ocean Bluff-Brant Rock, Massachusetts. Jambo lilitokea ambalo lilibadilisha ulimwengu siku hiyo. Reginald Fessenden alichezea mashua zilizokuwa baharini kupitia kwa redio, wimbo unaoitwa Oh Holy Night kwa lugha ya Kimombo, na kuwasomea Luka sura ya pili. Huu ulikuwa utangazaji wa kwanza wa redio duniani. Sasa, tuna simu ya rununu na tunaweza kuzungumza na mtu yeyote duniani bila wasiwasi.



Au vipi kuhusu Januari, mwaka wa 1879? Thomas Edison alifanikiwa kuvumbua vioo vya taa, na sasa kila taifa duniani linatumia sheria za umeme na sheria zinazosimamia fizikia kuona usiku.

Au vipi kuhusu Desemba 17, mwaka wa 1903? Wale ndugu wa familia ya Wright walifanikiwa kuendesha ndege ya kwanza, na sasa tunaweza kupanda ndege ya kisasa na kusafiri kote ulimwenguni kwa masaa machache. Ndege aina ya A380, ambayo ni ndege kubwa zaidi ya kibiashara, yenye uzito wa pauni milioni 1.2, inaweza kubeba zaidi ya watu 800 kwa zaidi ya masaa 9 bila kujaza mafuta kwa takriban maili 600 kwa saa kote duniani. Ikiwa watu wangeona kitu kama hiki katika miaka ya 1800, wangezimia kwa kuona kitu kama hicho. Lakini sasa, ni kawaida kwetu kama vile kubonyeza swichi na kuwasha taa.

Hoja ninayotoa ni kwamba sheria hizi tayari zilikuwa hapa duniani, tangu mwanadamu alipoumbwa. Zilikuwepo ili zitumiwe na mwanadamu; wala hakuziona. Aliona ndege wakiruka, aliona radi, lakini bado hakuelewa.

Ndivyo ilivyo pia kuhusu Maandiko. Dini imeweka mipaka kuhusu maana ya Neno la Mungu. Wewe na mimi tumesikia, kwa miaka mingi, kwamba mambo hayo yote yamepita, Mungu hafanyi miujiza tena. Karama za Roho zilikuwa kwa ajili ya mitume tu, au mwiba wa Paulo ulikuwa ugonjwa. Ukweli ni kwamba, Neno ni rahisi sana. Linamaanisha kile linachosema hasa. Lakini msingi wa Ufalme ndio ufunguo mkuu wa kwanza ambao lazima uwe nao ili kufungua milango mingine yote.

## **Sasa Hapa kuna Ufunguo Mwingine Mkuu:**

### **Sheria hazibadiliki!**

Ukiangusha jiwe litaanguka. Litaanguka mara ngapi? Kila wakati unapoliangusha! Sheria ya mvuto itahakikisha kwamba utapata jibu sawa kila wakati. Ndivyo ilivyo kuhusu Ufalme wa Mungu.

## SURA YA 5

# KUSAFIRI KWA NDEGE NI BORA KULIKO KUTEMBEA

Kusafiri kwa ndege ni bora kuliko kutembea! Nilipokuwa nikiandika sura hii, nilikuwa katika ndege yangu nikurudi nyumbani kutoka kwa nyumba yetu ya likizo ya wakati wa kiangazi ambayo iko kule Canada. Nilikuwa nikisafiri mwendo wa maili 250 kwa saa, na tulikuwa futi 23,000 kutoka ardhini. Kwa miaka mingi, tulisafiri kwa gari hadi Canada kutoka nyumbani kwetu huko Ohio. Ilikuwa safari ndefu ya masaa 31 ya kuchosha kufika huko. Ilinibidi kuendesha gari usiku kucha ili kufika huko siku iliyofuata. Naam, kulikuwa na mara chache tulitumia siku mbili kufika huko, lakini unapokuwa na likizo ya wiki mbili na siku nne zinatumiwa kuendesha gari, unapoteza muda wako mwingi katika hilo. Lakini, kwa kawaida nilikuwa nikichoka sana tulipowasili huko, kisha ilinibidi nikabiliane na safari hiyo hiyo ya masaa 31 kurudi Ohio.

Maisha yangu yote nimependa ndege na nimekuwa na leseni yangu ya urubani tangu nilipokuwa na umri wa miaka 19, lakini sikuwahi kufikiria kumiliki ndege. Je, umeangalia bei ya ndege? Lakini kadiri nilivyokuwa nikijifunza kuhusu Ufalme, nilitambua kwamba mimi ndiye niliyekuwa ninazuia ndege hiyo kwa mawazo yangu ya, “La” na umaskini. Nina ndege mbili sasa, moja ambayo huwa ninaendesha wakati wa kujifurahisha, ambayo ni ile ndege yangu ya kwanza, kisha ile ninayotumia kusafiri. Kama nilivyotaja awali, “Mafunzo ya ‘La’” hayaruhusu ndoto au uwezekano wa jambo. Tunafunga mambo kabla hata hayajaanza.

Sikuwahi kufikiria kumiliki ndege hapo awali. Sikuona uwezekano

wa jambo hilo. Kwa miaka mingi, nilikodisha ndege nilizotumia kusafiri. Lakini nilipojifunza sheria za Ufalme na kuona matukio baada ya matukio maishani mwangu yaliyodhihirisha Ufalme, niliamua kwamba nitamwamini Mungu kwa ajili ya kupata ndege yangu. Sikuwa na pesa za kuinunua wakati huo, lakini nilichukua hundi, na katika sehemu ya kumbukumbu niliandika “kwa ajili ya ndege yangu.” Niliorodhesha aina kamili ya ndege niliyokuwa nikipokea. Mke wangu nami tulitoa hundi hiyo kama mbegu katika Ufalme kulingana na Marko 11:24, huku tukiamini kwamba tulipokea tuliposali. Hivi ndivyo Bwana alikuwa amenionyesha kufanya hapo mwanzoni kuhusu Ufalme. Nilikuwa nimeona utaratibu huu maishani mwangu mara nyingi sana.

Baada ya majuma machache, nilikuwa nikifanyiwa uchunguzi wa kawaida wa kimwili kisha daktari akaniambia ghafula, “Je, kuna uwezekano unamjua mtu yeyote ambaye angependa kununua ndege?” Nilishangaa sana, maana hakuna mtu aliyewahi kuniuliza hivyo hapo awali. “Ni ndege ya aina gani?” Nikauliza. Alinieleza aina ya ndege na akaniambia ilikuwa katika uwanja wa ndege wa mtaani ikiwa nilitaka kuiona. Ajabu, ilikuwa aina ile ile niliyokuwa nimefanyia matoleo! Nilipitia uwanja wa ndege na kuitazama, na ilikuwa katika hali nzuri. Nilijua hii ilikuwa ndege yangu. Lakini kulikuwa na tatizo moja; sikuwa na pesa za kuinunua. Nilimwambia daktari nilipendezwa sana nayo na kwamba ningemjibu.

Wiki kadhaa zilipita na nikapokea simu kutoka kwa kakangu ambaye alikuwa akifanya kazi kwenye mgahawa wa babangu karibu na jengo nililomiliki. Nilikuwa nimemiliki jengo hilo miezi michache awali mwishoni mwa vuli. Nilikuwa nimepanga kubadili jengo hilo kuwa ofisi ya kampuni yangu ya huduma za kifedha. Jengo hilo halikutimiza kanuni za majengo ya biashara kwa madhumuni niliyokuwa nayo, kwa hivyo nilijua ningelazimika kulijenga upya. Niliwasiliana na mjenzi ambaye aliandaa michoro, kisha tukasaini mkataba. Hata hivyo, tuliamaa kusubiri hadi majira ya kuchipua kabla ya kuanza mradi kwa sababu ya hali ya hewa. Marekebisho yangehusisha ujenzi upya wa jengo hilo.

Mmiliki wa awali wa jengo hilo aliniambia kwamba maji yalikuwa yamefungwa kwa sababu ya majira ya baridi, kwa hivyo sikuchunguza ili kuhakikisha hilo. Mwishoni mwa mwezi wa Februari, baada ya msimu wa joto kuanza kuyeyusha theluji ya msimu wa baridi, nilipigiwa simu na kakangu. Aliniambia jengo langu lilikuwa limeharibika kwa kuwa maji yalikuwa yanatiririka kutoka ndani yake hadi barabarani. Yeye na mimi tulijua hilo lilimaanisha nini—maji hayakuwa yamefungwa kama

mmiliki wa awali alivyokuwa amesema. Hakika, nilipochunguza uharibifu, mabomba ya bafu ya ghorofa ya juu, pamoja na bafu ya chini na mabomba ya jikoni, yalikuwa yamepasuka na maji yalijaa jengo hilo. Kuta zote za kadibodi zilikuwa zimeanguka chini.

Jambo hili linaweza kuonekana kama janga kubwa, lakini mipango yangu ya ukarabati ilihitaji kuta zote za kadibodi kuondolewa na vyumba vipya kusanidiwa. Upande wa nje pia ulipaswa kubadilishwa pia. Kwa hivyo, kwa kweli, maji hayakuumiza jengo hilo hata kidogo. Uharibifu wowote uliotokea ulifanyika katika sehemu zilizohitaji kujengwa upya. Hata hivyo, niliponunua jengo hilo, nilichukua bima juu yake. Uharibifu wote ulishughulikiwa na kampuni ya bima ambayo iliniandikia hundi—na ndivyo ulivyokisia—ililipia ndege yangu. Ndege hiyo, aina ya Piper Warrior, ni rahisi kuendesha, na mimi huiendesha mara kwa mara ili kufurahia. Kila ninapoiendesha, mimi hustaajabia jinsi inavyopendeza kuendesha ndege yangu ya pesa taslimu. Bado ninamiliki ndege hiyo hadi sasa, na imekuwa miaka 20.

Ingawa katika hadithi hii matukio yaliyotokea yalikuwa ya kushangaza sana, sitaki kukuacha na mtazamo mbaya wa jinsi mambo yanavyofanya kazi. Mambo huwa hayajitokezi ghafla kama katika hadithi hii. Mungu anaweza kukuelekeza kwa fursa itakayokupa pesa za kulipia ndege yako, au labda unaweza kuipata kwa bei nafuu sana. Mawazo unayotaka kuwa nayo unapotoa matoleo kama mbegu katika Ufalme ni kwamba Mungu atakuonyesha mavuno na jinsi ya kuyateka. Jambo la pili ni kukaa ndani ya imani na uwezo wako uliokuza. Nimekuwa na watu wanaofikiri kwamba maana Mungu amewaonyesha jinsi ya kulipia gari lao basi wanaweza kutoa matoleo ya kuvuna dola trilioni moja. Huna imani ya kuvuna dola trilioni! Anza mahali ulipo na anza kutumia sheria za Ufalme na kujenga imani yako katika sheria za Ufalme na uwezo wako wa kutwaa yale ambayo Mungu anakuonyesha.

Lakini hapa kuna jambo ambalo nataka uelewe. Nilikuwa rubani kwa zaidi ya miaka 20 kabla ya kununua ndege. Je, unafikiri sheria za Ufalme zilifanya kazi katika miaka hiyo ishirini? Bila shaka ndio. Kuelewa kwangu, au niseme ukosefu wangu wa ufahamu, haukuniruhusu kufikiria kumiliki ndege.

Mwanadamu amewatazama ndege wakiruka kwa maelfu ya miaka, sheria ya kupaa ilifanya kazi mchana kutwa kila siku ili watu wote waione, lakini hakuna aliyeiona. Je, ni kitu gani usichokiona? Tafakari hili.

Mojawapo ya Maandiko ambayo Mungu alinifundisha siku za mwanzo

kuhusu pumziko katika riziki ya Ufalme ni Mithali 10:22.

*Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo.*  
— Mithali 10:22

Andiko hili linarejelea Andiko na kanuni kutoka Mwanzo 3:17 ambayo nilishiriki hapo awali.

*Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako. Michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni. Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi.*

— Mwanzo 3:17-19

Adamu alipopoteza Ufalme, alipoteza riziki iliyotoka kwa Ufalme na aliachwa kujiokoa kupitia kwa bidii yake mwenyewe. Lakini kama mimi na wewe tumeshagundua, hatuwezi kukimbia haraka vya kutosha kupitia kwa mfumo wa dhiki na kutokwa jasho ili kufikia uhuru tunaotamani sana. Lakini sasa kuna habari njema!!!! Yesu alikuja kuwahubiria maskini habari njema!

*Robo ya Bwana MUNGU i juu Yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema.*

— Isaya 61:1

Yesu alitumwa kuhubiri habari njema kwa maskini. Je, habari njema kwa maskini ni ipi? Rahisi, hawapaswi kufungwa na ukosefu na umaskini katika mfumo wa riziki wa laana ya dunia. Niamini, baada ya kuishi—au niseme kunusurika—kwa miaka tisa bila chochote ila madeni na shinikizo, Andiko hili lilikuwa habari njema, lakini la kutatanisha. Je, kweli lilimaanisha lilichosema? Je, haingekuwa jambo jema ikiwa kweli lilimaanisha kile lilichosema, kwamba baraka ya Bwana kweli huleta utajiri maishani mwetu? Nilihitaaji sana kujua ikiwa hii ni kweli kisha jinsi ya kutumia ukweli huu. Jambo moja nililolewa, hata hivyo, ni kwamba laana ya kazi nzito na jasho huleta riziki katika kiwango cha manusuru tu—na kiwango hicho hakitoshi. Hakuna aliyetaka kuwa huru kutokana na laana hii kuniliko, lakini hata hivyo sikujua jinsi ya kusababisha hilo katika maisha yangu. Nafikiri hivi ndivyo Wakristo wengi wanavyoishi—wanasoma ahadi

za Mungu ilhali hawajui jinsi ya kuzitumia na kuzidhihirisha hapa katika maisha yao wenyewe.

Nilipoanza kujifunza na Bwana aliponiongoza katika ufahamu wangu kuhusu kanuni za Ufalme, nilisoma jinsi Ibrahimu alivyokuwa tajiri sana. Koma hapo! Vipi kuhusu mfumo wa laana ya dunia; alishindaje hilo?

*Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifugo, kwa fedha, na kwa dhahabu.*

— Mwanzo 13:2

Alikuwa tajiri—la, Biblia inasema alikuwa tajiri sana—lakini kwa jinsi gani? “Vema,” unaweza kusema, “ilikuwa ni kwa sababu alikuwa Ibrahimu.” La, sivyo, na hapa ndipo unapohitaji kupata ufahamu wako wa Ufalme kuhusu sheria. Sheria hazizingatii wewe ni nani. Haziwaheshimu watu. Ikiwa mtu fulani au mtu yeyote, angeruka kutoka kwenye jengo la *Empire State Building* bila kiangushio, haijalishi ni mtu mkuu au mdogo kiasi gani, kila mtu atajua matokeo. Sheria ya mvuto hufanya kazi kila wakati. Kwa hivyo Ibrahimu alifanikiwa vipi licha ya laana ya dunia? Je, tunaweza kupata vidokezo katika hadithi yake? Sehemu ya jibu inaweza kupatikana katika Mwanzo 12. Hapo, Mungu alimpa Abramu, ambaye baadaye aliitwa Ibrahimu, ahadi kuhusu maisha yake na uzao wake.

*Bwana akamwambia Abramu, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.*

— Mwanzo 12:1-3

Ahadi hiyo ilitegemea Ibrahimu kumwamini Mungu na kumtii, na ilihitaji imani kuu kuacha mahali alipofahamu na kutojua alikokuwa akienda.

*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.*

— Waebrania 11:8

Kwa hiyo tunaona kwamba Mungu alipata kiingilio cha kisheria katika

ulimwengu kupitia mtu ambaye alimwamini hata wakati hakumwelewa. Imani ya Ibrahimu ilimwezesha Mungu kumbariki kibinafsi. Lakini baadaye, kwa sababu ya imani ya Ibrahimu, Mungu pia alifanya agano naye kuhusu warithi wake. Usifikiri kwamba hili si jambo la kawaida. Kumbuka, hivi ndivyo Shetani mwenyewe alipata kuingia duniani hapo mwanzoni. Adamu, ambaye alikuwa na mamlaka ya kisheria juu ya dunia, kama ilivyoandikwa katika Waebrania 2:7-8, alichagua kumwamini Shetani badala ya Mungu.

Imani ya Ibrahimu, ambayo ilifungua mlango wa kisheria wa ushawishi wa kimbingu maishani mwake, ilimpa furs ya kusitawi sana. Ufanisi huu ulienea hadi kwa warithi wake wote. Nilipoendelea kujifunza hili zaidi, nilisoma kuhusu Yusufu, mjukuu wa Ibrahimu. Nilipata picha nzuri na ufahamu kuhusu Ufalme na jinsi unavyofanya kazi, na hasa, kile ambacho Mithali 10:22 inadokeza.

Ili kuweka msingi, ndugu za Yusufu walimchukia na kumuua utumwani kwa wafanyabiashara walionunua watumwa ambao walipita eneo lao mara kwa mara. Walimpeleka Yusufu Misri, ambako aliuzwa kwa Potifa, kapteni wa jeshi la Misri. Ni katika kifungu kifuatacho ambapo nilipata sehemu muhimu ya fumbo kuhusu uwezo wa Ibrahimu kufanikiwa kwa kiwango hicho.

*Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko. Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi; naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri. Bwana wake akaona ya kwamba Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote mkononi mwake. Yusufu akaona neema machoni pake, akamtumikia.*

*Naye akamweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na yote yaliyomo akayaweka mkononi mwake. Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivyomo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. MBARAKA WA BWANA UKAWA JUU YA VYOTE ALIVYOKUWA NAVYO KATIKA NYUMBA, NA KATIKA SHAMBA. Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu chochote chake, ila hicho chakula alichokula tu.*

— Mwanzo 39:1-6

Andiko lasema wazi kwamba ilikuwa ni Baraka ya Bwana iliyomletea Yusufu mafanikio. Lakini Baraka ya Bwana ilikuwa nini au ni nini? Nilitambua kwamba ilikuwa ni Baraka “kamilifu” ya Bwana, si baraka “jumla” ya Bwana. Sote tunaweza kusema kuhusu tukio fulani kubwa kwamba “ni baraka jumla.” Lakini andiko hili halirejelei jambo jema la jumla linalotokea. Linazungumzia juu ya “Baraka Kamilifu.”

Nilipata ufahamu kwamba Baraka kamilifu ya Bwana ilikuwa agano alilolifanya Mungu na Ibrahimu pamoja na warithi wake. Baraka hasa ilikuwa kwenye ahadi alizopewa Ibrahimu katika agano hilo. Makubaliano ya kisheria huwa na majukumu na wajibu wa pande zote mbili zinazohusika, lakini pia huorodhesha manufaa kwa kila mmoja. Katika hali hii, ahadi alizopewa Ibrahimu zilikuwa za kumletea yeye faida. Ili kufurahia manufaa hayo, aliwajibika kufuata amri na sheria za Bwana. Pia niliona wazi kwamba chochote Yusufu alichokileta chini ya mamlaka yake ya kisheria pia kilisitawi chini ya ahadi na kupata manufaa yale yale.

Kisha nikaelewa andiko la Mithali 10:22. Ahadi za Mungu alizopewa Ibrahimu kama makubaliano ya kisheria zilishinda mfumo wa umaskini wa laana ya dunia. Baraka aliyopewa Ibrahimu ilifanya iwe halali kwa Mungu kumbariki Ibrahimu na ukoo wake kwa ustawi na ushawishi ambao Mungu wakati mmoja alitaka mwanadamu awe nao. Hebu sasa tusome Mithali 10:22 huku tukiwa na ufahamu zaidi.

## Ufunguo Mkuu:

### **Baraka ya Bwana [Ahadi Alizopewa Ibrahimu] hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo.**

Maneno “*hachanganyi huzuni nayo*” yanarejelea mfumo wa laana wa dunia katika Mwanzo 3:17—kupitia kwa kazi yenye dhiki na jasho. Neno *huzuni* katika lugha ya Kiyahudi pia linamaanisha kazi ngumu! Je, unaona hili? Mwanadamu anaweza kuepuka mipaka ya laana ya dunia ya kazi yenye dhiki na jasho kupitia kwa ahadi alizopewa Ibrahimu. Doh, najua unachofikiria—“Ahadi hizo zilitolewa kwa Ibrahimu na uzao wake pekee.” Naam, lakini ninahitaji kukuonyesha Andiko lingine katika Wagalatia 3:13-14.

*Kristo alitukomboha katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa*



*kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba baraka [ahadi] ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani.*

— Wagalatia 3:13–14

Sasa kwa njia ya imani, sisi kama waumini katika Yesu Kristo tunashiriki katika baraka aliyopewa Ibrahimu. Basi ni baraka gani aliyopewa Ibrahimu? Tunaweza kupata orodha ya ahadi katika Kumbukumbu la Torati 28.

*Itakuwa utakaposikia sauti ya Bwana, Mungu wako, kwa bidii, kutunza kuyafanya maagizo yake yote nikuagizayo leo, ndipo Bwana, Mungu wako, atakapokutukua juu ya mataifa yote ya duniani; na baraka hizi zote zitakujilia na kukupata usikiapo sauti ya Bwana, Mungu wako.*

*Utabarikiwa mjini, utabarikiwa na mashambani. Utabarikiwa uzao wa tumbo lako, na uzao wa nchi yako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, maongeo ya ng'ombe wako, na wadogo wa kondoo zako.*

*Litabarikiwa kapu lako, na chombo chako cha kukandia unga.*

*Utabarikiwa uingiapo, utabarikiwa na utokapo.*

*Bwana atawafanya adui zako wainukao juu yako kupigwa mbele yako; watakutokea kwa njia moja, lakini watakimbia mbele yako kwa njia saba.*

*Bwana ataiamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako.*

*Bwana atakuweka uwe taifa takatifu kwake, kama alivyokuapia; utakaposhika maagizo ya Bwana, Mungu wako, na kutembea katika njia zake. Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako. Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa.*

*Atakufunulia Bwana hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo*

*ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya; msipokengeuka katika maneno niwaamuruyo leo kwa lolote, kwenda mkono wa kuume wala wa kushoto, kwa kuifuata miungu mingine na kuitumikia.*

— Kumbukumbu la Torati 28:1-14

Ahadi hizi zote, ingawa ziko katika Agano la Kale ni zako kufurahia. Tofauti ni kwamba katika Agano la Kale watu walizipata kupitia kile walichokifanya, lakini sisi tunazipata kupitia kwa imani yetu katika Yesu Kristo chini ya Agano Jipya. Wewe na mimi, kama watu wa Mataifa, tumeingizwa ndani; na sasa, kwa njia ya Yesu Kristo tunashiriki Baraka ya Ibrahimu. Lakini tuna zaidi ya baraka za kimwili za Ibrahimu kwa kuwa tuna baraka za kiroho za kuzaliwa upya. Kwa hivyo tuna baraka za kimwili, za kidunia kupitia kwa Ibrahimu, na pia tuna baraka za milele za mbinguni kupitia kwa Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu kama wana na binti za Mungu. Kumbuka, wana na binti pekee ndio wanaopata urithi; wala sio watumwa. Ingawa Ibrahimu alimpenda Mungu, Roho Mtakatifu hakuishi ndani yake, maana hakuwa amezaliwa upya, wala hangeweza kuingia mbinguni. Bila shaka, aliingia mbinguni baada ya Yesu kulipa deni la dhambi.

Sasa nilielewa maana halisi ya Mithali 10:22 inaposema kwamba baraka ya Bwana hutajirisha wala hachanganyi huzuni nayo. *Huzuni* katika lugha ya Kiyahudi inamaanisha kazi ngumu, ambayo sasa nilielewa ni mfumo wa laana ya dunia wa kazi nzito ya kutoa jasho. Nilielewa kwamba agano hili, baraka hii ya ahadi ya msaada wa Mungu na manufaa Yake, ilimwinua Ibrahimu juu ya laana ya dunia na kumfanya afanikiwe. Nilitambua kwamba manufaa ya baraka hiyo kama inavyofafanuliwa katika Kumbukumbu la Torati 28, ilinionyeshwa wazi kwamba nilipaswa kufanikiwa. Matokeo ya ahadi hizi ni kwamba mimi nilikuwa na hatma ya kuwa kichwa wala si mkia, mkopeshaji wala si mkopaji. Hii ni haki kisheria ya kila mtoto wa Mungu. Kama Yusufu, nina baraka za Mungu, na ninapaswa kufanikiwa. Pia nina urithi wa Ufalme wote wa Mungu. Kama mwana, yote tayari ni yangu kisheria.

Nilipotazama tena hadithi ya Yusufu katika Mwanzo 39, niliona wazi kwamba ni mafanikio dhahiri ya Yusufu yaliyomvutia Potifa, na pia kuvutia macho ya mataifa ya ulimwengu na kuwafanya waone tofauti katika watu wa Mungu.

*Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la Bwana, nao watakuwa na hofu kwako. Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupaa.*

— Kumbukumbu la Torati 28:10-11

Kuna kidokezo kingine kikubwa katika Mwanzo 39:6 ambacho niliona pia na nataka ukione. Likizungumza juu ya Potifa, andiko hili linasema, “Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu; wala hakujua habari za kitu chochote chake, ila hicho chakula alichokula tu.” Nilipata ufahamu! Hapa kuna mfano wa pumziko ambalo tunazungumzia. Potifa hakuhitaji kuwa na wasiwasi juu ya kitu chochote isipokuwa chakula alichokula. Hii ina maana kwamba mafanikio Yusufu aliyoleta kwa nyumba yake, Baraka ya Bwana, ilileta matokeo ambayo yalimruhusu Potifa kuzingatia kazi yake wala si kuishi!

Mimi na Drenda tuna msemo ambao tumeutumia kwa miaka mingi, “Hadi utakapotatua suala la pesa, kamwe hutagundua hatima yako,” na hutawahi kugundua wewe ni nani haswa. Hutafahamu utume wako, mahali pako pa shauku, wala kuridhika hata kidogo. Utakuwa ukifanya maamuzi yako yote kama nusuru, huku ukitafuta au kushikilia pesa, na kuwa kile usicho ili tu kulipwa mshahara. Hapa tunaona matokeo ya Baraka ya Bwana kwa Potifa, ambaye hata hakujua chochote kuhusu Ufalme wa Mungu. Kwa kuweka vitu vyake chini ya uangalizi wa Yusufu, mali yake, na kila kilichomhusu kiliamishwa na kuwekwa chini ya agano alilolibeba Yusufu. Unaweza kuona wazi wakati jambo hili lilitokea katika mstari wa 5 wa sura ya 39.

*Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivyomo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. Mbaraka wa Bwana ukawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba.*

— Mwanzo 39:5

Hapa tena tunaona kitu kilicho katika ulimwengu, yaani chini ya mfumo wa laana ya dunia, kikija chini ya mamlaka ya Ufalme wa Mungu na kuwa na mabadiliko makubwa. Tuseme ukweli: Ikiwa Mungu anakusaidia kwa hekima Yake, anakuongoza kufanya maamuzi sahihi, na kukuonya

juu ya mitego inayoweza kuwepo, hakuna mtu asiyeweza kufanikiwa! Je, unaona jambo hili? Baraka ya Bwana ni yako!

Nilipokuwa nikijifunza hili wakati Bwana alikuwa akinifunza kuhusu Ufalme, nilichanganyikiwa ni kwa nini Yusufu alikuwa na mafanikio makubwa kwa sababu ya baraka hii, lakini Wakristo wengi ninaowajua leo wanatatizika kulipa bili zao. Kuwa huru kabisa kifedha ni kitu ambacho wengi hufikiri kwamba hakiwezekani. Lakini tuna agano bora zaidi lenye ahadi bora kuliko zile za Agano la Kale. Ingawa nilielewa kwa udhahiri Baraka ya Bwana, bado sikujua hasa jinsi baraka ingelivyoleta majibu niliyohitaji—lakini nilikuwa nikijifunza na kufurahia uhuru zaidi na zaidi nilipoanza kujaribu kutumia kile Mungu alichokuwa amenifundisha.

Kisha nilielekeza mawazo yangu katika Agano Jipya na kumtazama Yesu na huduma Yake ili kujifunza zaidi kuhusu jinsi Ufalme wa Mungu ulivyokuwa ukibadilisha hali huko.

*Ikawa makutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, Yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka, wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni.*

*Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni, “Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki.” Simoni akajibu akamwambia, “Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu.”*

*Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama. Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, “Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana.” Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni.*

*Yesu akamwambia Simoni, “Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu.” Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao,*

*wakaacha vyote wakamfuata.*

— Luka 5:1–11

Hii ni hadithi ya jinsi Ufalme wa Mungu ulivyogeuzwa mfumo wa laana ya dunia katika maisha ya wavuvi watatu asubuhi moja. Unaposoma andiko hili, unaona kwamba Petro, Yakobo, na Yohana walikuwa wamevua samaki usiku kucha bila kupata kitu. Hawakufua dafu usiku mzima baada ya kufanya kazi hiyo yote, ambalo ni jambo la kawaida katika mfumo wa laana ya dunia ya kazi nzito na jasho. Lakini Yesu alipotumia Ufalme wa Mungu na kazi yake, wavuvi hao walivua samaki wengi sana kiasi cha kufanya mashua zao zikaribie kuzama!

Koma!!!! Hebu tutafakari yale ambayo tumesoma hivi punde. Kutokuwa na chochote, kutokuwa na samaki, ukosefu wa pesa, yote yaligeuka yakawa mavuno ambayo yalikuwa karibu kuzamisha mashua mbili? Watu huisoma na wameisoma hadithi hii kwa mamia ya miaka na hawaoni wala kufikiria kwamba hili linaweza kutokea kwao. Kwa nini? Jibu la kawaida ni kwamba Yesu alikuwepo na ndiye aliyefanya hivyo. Kumbuka hadithi niliyokuonyesha katika Marko 6 ambapo Yesu hakuweza kuponya watu kwa sababu watu hawakuwa na imani, na hivyo, Ufalme haukuwa na mamlaka? Ilibidi mtu aipe mbingu mamlaka kabla ya mbingu kuchukua hatua katika hali hii.

**Simoni akamjibu, “Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu.”**

Katika hadithi hii Petro alikubaliana na mbingu, kisha mbingu zikapata kiingilio kisheria. Hapa tena tunaona hali katika ulimwengu ikibadilishwa na Ufalme wa Mungu. Ajabu, siyo? Ni kama vile watu kwa maelfu ya miaka wameona ndege wakiruka angani lakini wamekosa kutambua kwamba wanaweza pia kupaa na hivyo kutolifuatilia jambo hili kamwe. Ndivyo walivyo Wakristo leo, wanakosa kutambua kwamba si lazima wavumilie nyavu zisizo na kitu bali wana kiingilio cha kupata nguvu za mbinguni ili kuwasaidia kufanikiwa maishani. Kile ninachotaka uone hapa ni kwamba wale wale waliokosa kupata chochote ndio wale wale waliokuwa na mashua mbili zilizojaa kiasi cha kuzama!

Rafiki yangu, tofauti ni Ufalme, sio watu. Unaweza kufikiria huna hatima, una upungufu fulani, wala hufaulu unapofanya chochote. Lakini kwa kweli, unachohitaji ni Ufalme ili kubadilisha maisha yako kuwa

hadithi ya mafanikio. Naam, una sehemu yako ya kutekeleza. Ilibidi waende kuvua samaki—ilibidi watunze nyavu zao, na kuziandaa kwa ajili ya kuvua samaki—lakini mtu yeyote anaweza kuvua samaki ikiwa Mungu atakuonyesha ziko wapi.

Sikiliza, mfumo wa laana ya dunia wa kwenda hapa na pale na kutokwa jasho hauwezi kukamilisha chochote. Huwezi kwenda kwa haraka au kwa muda mrefu vya kutosha ili kutimiza ndoto zako. Mungu kamwe hakukusudia usage meno na kujaribu kwa nguvu zako mwenyewe kutimiza mambo.

Kwa kutumia sheria na ahadi za Ufalme wa Mungu, tunaweza kupaa badala ya kutembea. Hebu niseme kwa maneno tofauti. Ingawa sheria ya mvuto wa sayari bado inafanya kazi, tunaweza kusafiri kwa ndege kwa kutumia sheria nyingine—sheria ya kuinuliwa—na kufurahia njia mpya kabisa ya kuishi.

**LAKINI KWA KWELI,  
UNACHOHITAJI NI UFALME  
ILI KUBADILISHA MAISHA  
YAKO KUWA HADITHI  
YA MAFANIKIO. NAAM,  
UNA SEHEMU YAKO YA  
KUTEKELEZA.**

Kumbuka, unapokuja kwa Kristo, wewe ni mshiriki wa Ufalme wa Mungu. Kama raia, una haki za kisheria; na kama mwana au binti, una haki ya kuwa mrithi. Haki na manufaa yako ya kisheria yamekuweka juu ya mfumo wa laana ya dunia wa umaskini, magonjwa, na kushindwa.

Hebu tafakari jinsi mstari huu ulivyosikika kwa Mwisraeli ambaye alikuwa mtumwa maisha yake yote. Kwa kweli, walichojua tu ni utumwa wa miaka mingi. Haya ndiyo maneno Musa aliyoliambia taifa la Israeli walipokuwa wakielekea kuingia katika nchi ya ahadi.

*Tena itakuwa atakapokwisha Bwana, Mungu wako, kukuleta katika nchi aliyowaapia babu zako, Ibrahimu na Isaka na Yakobo, ya kuwa atakupa; miji mikubwa mizuri USIYOIJENGA WEWE, na nyumba zimejaa vitu vyema vyote usizojaza wewe, na visima vimefukuliwa usivyofukua wewe, mashamba ya mizabibu na mizeituni usiyoiipanda wewe, nawe utakula na kushiba; ndipo ujitunze, usije ukamsahau Bwana aliyekutoa nchi ya Misri, nyumba ya UTUMWA.*

— Kumbukumbu la Torati 6:10-12

Kuzoea utumwa kuliwafanya wasijue njia nyingine ya kutekeleza jambo ila kupitia kwa kazi nzito na kudondoa jasho. Lakini hapa Mungu alikuwa akiwaambia kwamba kazi yao wenyewe haingetosheleza mahitaji yao. Hakuwa akiwaambia kwamba hawatajishughulisha tena na chochote, lakini kwamba hawangefungwa tena kwenye mfumo unaohitaji kazi nzito ili kuishi. Mungu alisema kwamba wangepanikiwa katika nchi aliyokuwa akiwaelekeza.

Hebu nimalize sura hii kwa kukusimulia hadithi nyingine moja inayofafanua zaidi kile ninachosema. Mimi na Drenda hatupendi magari sana. Kuna baadhi ya watu wanaoyapenda sana na wanaweza kukuhesabia magari yote wanayovutiwa nayo. Kwa sababu tusiyoiuia, mimi na Drenda hatujawahi kupenda magari. Sasa, usinielewe vibaya. Tunapenda vitu vizuri, lakini hatujawahi kusema kwamba lazima tuwe na gari fulani. Kawaida huwa tunanunua gari kisha tunaliendesha kwa miaka 10 au zaidi. Bila shaka, huwa tunatunza vyema magari yetu na kamwe hayafanani na magari makuukuu, lakini mradi tu yanaonekana vizuri na yanasafiri vyema, hatuna shida.

Lakini miaka michache iliyopita, kanisa letu lilikodisha magari kadhaa aina ya Escalade kwa ajili ya kongamano tulilokuwa nalo. Tuliyakodisha ili kusafirishia wageni wetu, na tulitaka kutumia magari mazuri kufanya hivyo. Sasa, hii haikuwa mara yetu ya kwanza kufanya hivyo. Huwa tunafanya hivyo kila wakati. Lakini ilikuwa mara yetu ya kwanza kuendesha gari aina hiyo yalipokuwa kanisani kwetu kwa ajili ya kongamano. Sina hakika ni kwa nini mimi na Drenda tuliendesha moja ya magari hayo wakati wa kongamano hilo, lakini tulienda nayo nyumbani kwetu hadi siku iliyofuata. Na wajua nini? Tuliipenda. Mimi na Drenda tulipenda jinsi ilivyokuwa tulipoiendesha na mwonekano wake.

Wakati huo, tulikuwa tukiendesha gari nzuri aina ya *Honda Pilot*, lakini hii *Escalade* bila shaka ilikuwa hatua moja juu ya gari letu. Ilikuwa ya rangi ya lulu nyeupe ya platinamu na ilikuwa na muundo mfupi. Ikiwa unajua mengi kuhusu magari haya, kuna yale yenye muundo mrefu na pia mfupi. Tulipenda lile fupi zaidi maana tulihisi ilikuwa rahisi zaidi kuliendesha na kuligeuza. Nilipokuwa nikiliendesha nikiwa na Drenda, alisema, “Wajua, napenda gari hili; nafikiri tunafaa kuwa na moja kama hili.” Nilikubali. “Tunapaswa kuwa na moja kama hili, lenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe.” Sote wawili tulikubali.

Ingawa hatukumwambia mtu yeyote kuhusu mazungumzo yetu, mwezi mmoja baadaye, nilipokuwa nikienda nje kuchukua jarida langu,

simu yangu ya rununu ililia. Niliitambua sauti ya aliyenipigia simu kama mshirika wa kanisa langu. Alisema, “Hujambo,” kisha akasema kwamba alitaka kuninunulia gari aina ya *Escalade*. Nilistaajabu kwa dakika moja lakini nikasema, “Vema!” Kisha akaniuliza ningependa rangi gani, nami nikamwambia kwamba tulilipenda lenye rangi ya lulu nyeupe. Akasema, “Nitakupigia simu tena nitakapolipata.” Hata hivyo, hakuniuliza ikiwa nilitaka lile fupi au ndefu. Mwezi ulipita nikadhani labda alikuwa amesahau kuhusu gari, lakini hakika, alipiga simu na kutuambia tupitie kwake, kwamba gari aina ya *Escalade* lilikuwa tayari kuchukuliwa.

Tulipokutana naye, tuliona *Escalade* yenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe ikiwa imeegeshwa hapo. Ilikuwa kamilifu kwa kila njia, na bila mkwaruzo. Tulimwambia tuliipenda. Kisha akaomba msamaha, akasema alisikitika ilichukua muda mrefu, kwamba ingawa alikuwa amejaribu kutafuta muundo mrefu, aliloweza kupata ni lile fupi tu. Tulicheka na kusema, “Lile fupi ndilo tulilotaka.” Tuliliendesha gari hilo hadi nyumbani na tulijihisi kama matajiri zaidi duniani kuliendesha. Lakini wajua nini? Magari haya aina ya *Escalade* yamekuwepo kwa muda mrefu. Sikuwa nimewahi kufikiria kuwa na moja kama hiyo! Ili kuelewa hadithi hii vyema, unahitaji kujua kwamba nimetoa magari nane, kwa hivyo nilikuwa na mbegu ardhini kuhusu magari lakini sikuwa nimesema ninataka gari.

Wazo la Ziada - Najua unachofikiria, kwamba mambo kama haya hutokea kwa wahubiri pekee. Naam, nimekuwa katika nyanja ya kifedha kwa miaka 36 na nimezungumza na wahubiri wengi. Kusema kweli, wengi wao hawana chochote cha ziada zaidi ya mahitaji yao ya kimsingi. La, mambo haya hayatutukii kwa sababu tunahubiri kuhusu Ufalme, bali kwa sababu tunaishi katika Ufalme na tunatumia sheria zake maishani mwetu. Nilikuwa nimeshatoka kwa madeni kabla ya kuanzisha kanisa langu. Sikuhitaji kuanzisha kanisa ili nipate kazi ya kulipa bili zangu. Nilianzisha kanisa langu ili kuwaambia watu kile ambacho mimi na Drenda tulikuwa tumegundua—habari njema ya Ufalme!





## SURA YA 6

# KUNA MENGI YA ZIADA MAISHANI KULIKO KULIPA BILI!

Ilionekana kama chemchemi ndogo ya maji katika maisha ya dhoruba niliyokuwa nikikabiliana nayo. Tulikuwa tumealika watu wapatao 50 katika ile nyumba yetu kuukuu mashambani mchana ili kufurahia pamoja kuota moto, kula na kuwa na ushirika. Huu ulikuwa wakati wa miaka yetu ya mafadhaiko na mahangaiko makubwa ya kuishi bila pesa. Nilikuwa nikitarajia mkutano huo maana nilikuwa nimechoka kihisia na nilihitaji kitu chanya cha kuzingatia kidogo. Jioni hiyo ilikuwa na mafanikio makubwa: chakula kilikuwa kizuri, marafiki zetu wengi walikuja na watoto wao, na wote walikuwa na wakati mzuri. Nyumba ilikuwa imejaa wakati mlango ulibishwa. Nilifikiri huenda ni mtu aliyekuwa amechelewa kufika kwa mkutano wetu, lakini nilipofungua mlango, nilisalimiwa na mfanyakazi wa kampuni ya umeme. Kwa upole alisema alikuwa amekuja kuzima umeme wangu kwa sababu ya bili ambayo haikuwa imelipwa. Niliogopa sana. Nyumba yangu ilikuwa imejaa wageni na nilihitaji umeme, na jamani hilo lingeniletea aibu sana.

Kwa haraka nilimwomba mfanyakazi huyo atoke nje ya nyumba hadi kwenye ua kwa dakika moja. Nilimuuliza ni nini kingehitajika ili umeme usizimwe naye akanipa kiasi cha fedha. “Hizo ni pesa nyingi sana,” niliwaza. “Unaweza kupunguza kidogo?” Alifikiria kwa dakika moja kisha akanipunguzia kiasi cha pesa. “Je, unaweza kushikilia hundi hadi Jumanne

kabla ya kuipeleka kwa benki?” Nikauliza. Akasema, “Hamna shida,” basi nikamwandikia hundi. Hakukuwa na pesa kwenye akaunti siku hiyo, na sikujua jinsi zingekuwepo kabla ya Jumanne pia, lakini angalau umeme ulikuwepo wikendi nzima. Sikumbuki nilifanya nini Jumanne ilipofika, lakini labda nilipata kitu cha kubadilishana ili kupata pesa.

Hii ilikuwa siku moja katika maisha yetu ya kuishi katika janga la kifedha. Sasa fikiria kuishi kwa njia hii kwa miaka tisa! Kuishi chini ya mafadhaiko aina hii huzuia maono yote na kuondoa kila chembe ya furaha ambayo siku inaweza kuleta. Kila wazo huzingatia jinsi ya kuishi, na mahali pa kupata pesa za kulipia bili inayokuja. Je, nilitumia pesa nyingi sana wiki iliyopita? Je, nichukue kikokotozi changu ninapoenda kununua mboga ili nisipitisha pesa? Daima nilifikiria jinsi ya kufanya mambo kwa njia ya bei nafuu. Rafiki, huku si kuishi! Angalia kile ambacho Mathayo 6:25 inasema.

*Kwa sababu hiyo nawaambieni, msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu, mvae nini. Maisha je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?*

— Mathayo 6:25

Yesu anasema kwamba vitu vilivyo maishani havina uzima! Kila kitu hapa maishani kinafaa kutusaidia katika maisha na kusudi letu. Lakini kwa kuwa Adamu alipoteza riziki ya Ufalme, maisha yalipinduka na sasa kila kitu kinachotegemeza uhai ni muhimu zaidi kuliko uhai wenyewe. Watu hawajui uzima halisi ni nini na kwa hakika hawajui wao ni nani hasa. Uliza mtu yeyote yeye ni nani naye atakuambia kile anachofanya. “Mimi ni daktari, mimi ni wakala wa mali,” nk. La, hiyo ni kazi unayoifanya wala sio utambulisho wako. Mwanadamu amepoteza ndoto zake. Ninachomaanisha ni kwamba mwanadamu sasa huota jinsi ya kupata pesa nyingi wala hana ndoto ya kusudi lake. Kwa maneno mengine, chochote kinacholipa pesa nyingi hufanyika ndoto yake. Walakini, kwa sababu kila mtu ameumbwa kwa njia ya kipekee na talanta na uwezo tofauti, wanajikuta katika kazi au majukumu yasiyo mapenzi yao. Maisha yanakuwa yenye majuma au muda mrefu ambayo yanangoja kuwa huru katika wikendi au wakati wa kustaafu.

Basi hebu nikuulize swali. Kama hungekuwa na hitaji la pesa katika maisha yako yote, je, ungefanya nini? Labda ungefanya kazi tofauti na ile unayofanya sasa hivi. Kama nilivyotaja hapo awali, najua kutokana na takwimu kwamba angalau 70% ya Wamarekani, walipoulizwa kama wanapenda kazi zao, walisema hawafanyi kile wanachopenda. Nataka

uelewe kwamba kukimbilia kupata mali, shinikizo la kufaulu, na wasiwasi wa mara kwa mara kuhusu siku za usoni, yote hayakuwa mpango wa Mungu hapo mwanzoni.

*Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, “Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi.”*

*Mungu akasema, “Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu; na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu.” Ikawa hivyo.*

*Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.*

— Mwanzo 1:27-31

Mwanadamu aliumbwa siku ya sita ya uumbaji—mwisho wa siku ya sita. Aliumbwa mwishoni mwa siku ya sita kwa sababu aliumbwa kukaa na Mungu siku ya saba, siku tunayojua kuwa ni siku ya mapumziko.

*Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi Lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi Yake yote aliyofanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyofanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi Yake yote aliyoiumba na kuifanya.*

— Mwanzo 2:1-3

Biblia inasema kwamba Mungu alipumzika siku ya saba. Hakuwa amechoka! Alikuwa amemaliza kazi. Kila kitu kilikuwa kimekamilika. Kila kitu ambacho mwanadamu angehitaji duniani kilikuwa tayari duniani wakati mwanadamu alipojitokeza. Amani! Mwanadamu alikuwa na riziki yote ambayo angehitaji. Hakuwa na wasiwasi juu ya kulipa bili, au kuwa mgonjwa. Alikuwa na mwili mkamilifu na mke mkamilifu. Jambo pekee

ambalo wangezingatia ni uhusiano wao mmoja kwa mwingine, Mungu, na kazi au kusudi lao. Adamu alikuwa mtawala wa dunia nzima; alitawala kikamilifu kwa mamlaka na nguvu za Ufalme wa Mungu. Lakini tunajua mwisho wa hadithi hiyo. Adamu na Hawa waliusaliti Ufalme wa Mungu na kupoteza mahali pao, riziki yao, na kusudi lao. Kusudi lao lilifanyika la unusuru. Wasiwasi na woga sasa ulitawala mawazo yao na mapambano ya kuishi. Kama vile Mwanzo 3:17 inavyosema, walipaswa kufanya kazi nzito yenye dhiki na kutokwa jasho.

## Adamu alipoteza siku ya saba!

Sasa hakukuwa na mapumziko wala amani. Giza la kutokuwa

**UTAJIRI HUTUVUTIA KAMA  
MAHALI PA KUTOROKEA  
ILI KUPATA PUMZIKO—  
MAHALI AMBAPO  
TUNaweza KUZINGATIA  
KILE TUNACHOTAKA  
KUFANYA, NA KUISHI  
MAISHA YALIYOJAA  
KUSUDI BADALA YA  
KUISHI TU.**

mkamilifu lilifunika maisha ya Adamu na ilimbidi kukimbia ili kukaa mbele ya utupu huo. Mwanadamu ameishi katika hali hii ya kutokamilika tangu wakati huo. Lakini kulikuwa na matumaini. Mwanadamu alipotenda dhambi, Mungu alimpa ukumbusho, ama tuseme picha, ya kile ambacho siku moja angerudisha katika uumbaji Wake. Iliitwa Sabato. Neno *sabato*

kihalisi linamaanisha pumziko. Siku ya saba ya juma ilitolewa kwa mwanadamu kama siku ya Sabato. Sharti la Sabato lilikuwa kutofanya kazi yoyote;

kutokwa jasho na kazi nzito zenye dhiki hazikuruhusiwa. Ilikuwa siku ambayo mwanadamu alipaswa kuacha kila kitu, kufurahia familia yake, na kumwabudu Mungu. Maandalizi yote ya Sabato yalipaswa kukamilishwa kabla ya Sabato kuanza. Hata mlo wa Sabato ulipaswa kutayarishwa usiku kabla ya Sabato. Ilikuwa ni siku ya mapumziko na riziki kamili na kila hitaji ambalo lingeweza kutokea lilikuwa limeshughulikiwa awali. Mwanadamu angeweza kuacha kila kitu na kufikiria jambo lingine wala si jinsi ya kuishi.

Siku ya Sabato ilikuwa ni siku tu. Lakini mwanadamu amekuwa akiota kuwa na maisha ya pumziko tangu wakati huo. Kutafuta mali kwa mwanadamu ni dalili ya hamu yake ya kuwa huru kutokana na kazi yenye dhiki na kutokwa jasho ambayo imemshikilia maisha yake yote. Utajiri hutuvutia kama mahali pa kutorokea ili kupata pumziko—mahali ambapo

tunaweza kuzingatia kile tunachotaka kufanya, na kuishi maisha yaliyojaa kusudi badala ya kuishi tu.

Leo, Sabato, siku ya saba, iwe unaiadhimisha Jumamosi au Jumapili, haionwi kama jambo la heshima kuu katika utamaduni wetu. Naam, watu wengi wanaohudhuria kanisa hufanya hivyo Jumapili asubuhi. Lakini ukiangalia utamaduni kwa ujumla, huwezi kuitofautisha Sabato na siku nyingine yoyote ya kazi. Nilipokuwa mtoto, Jumapili kila kitu kilifungwa. Hukuruhusiwa kwenda kununua chochote Jumapili; hata iwe ni mafuta ya gari. Babangu alihakikisha kwamba amenunua mafuta Jumamosi usiku ili kuwa na mafuta aliyohitaji Jumapili. Ikiwa unajua mengi kunihusu, unajua ninapenda kuwinda, lakini kama mwindaji, sikukubaliwa kuwinda Jumapili pia. Ilikuwa ni kinyume na sheria kuwinda siku ya Jumapili. Watu walivaa nguo zao bora na kula chakula cha jioni na familia zao siku ya Jumapili. Bila shaka hayo yote yamebadilika leo. Lakini maana ya kweli ya Sabato haijabadilika.

Lakini haijalishi jinsi maandalizi ya Sabato yalivyokuwa mazuri, au mlo wa familia kuwa mkubwa kiasi gani, Jumatatu ilikuwa inakuja. Nakumbuka maneno katika lugha ya Kimombo yalivyotumiwa kwa muda mrefu ni kama, “Hisia za Jumatatu asubuhi” ambayo yanamaanisha *hofu*. Mifano ya maneno yanayomaanisha Jumatatu asubuhi ni kama, “Lazima niende kazini” na “kurudi kwenye jiwe kuukuu la kusagia.” Na ukikoma na kutafakari jambo hili, lilionekana kama utumwa. Lakini asante Mungu kwa siku ya Ijumaa! Hata leo, wikendi na Sabato huleta mahali pafupi na kupumzika kwa watu wengi. Lakini ni muda mfupi na msongamano wa magari Jumatatu asubuhi unangoja.

Lakini vipi ikiwa kweli kungekuwa na njia ya kuishi daima katika Sabato. Ingekuwa jambo la kupendeza kama nini ikiwa kweli kungekuwa na njia ya kuishi maisha yasiyo na woga, yaliyojaa riziki, kusudi, na pumziko! Mimi na Drenda tuliishi maisha ya mateso, hofu, magonjwa, na ukosefu wa usalama kwa miaka tisa hadi tulipotambua kwamba tungeweza kuchagua pumziko la Sabato maishani mwetu. Ninamaanisha!

*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*

— Waebrania 4:9-11

Rafiki, hili ni Agano Jipya. Kuna raha ya Sabato iliyopo kwa ajili ya watu wa Mungu leo. Maandiko haya yanadokeza kwamba tunaweza kuingia katika pumziko la Mungu na kupumzika kutokana na kazi yetu. Kumbuka kile tulichojifunza hivi punde: Pumziko la Mungu linasema kila kitu ni kizima, kamili, na riziki inapatikana kwa urahisi. Kuna uhuru kutoka kwa mawazo ya unusuru, kufungwa na umaskini, na magonjwa na maradhi. Kuna njia mpya! Sabato haikuwa habari ya Agano la Kale tu, bali ipo kwa ajili yetu sisi leo pia. Lakini kabla hujafikiri ninazungumza kuhusu kuishi chini ya sheria na taratibu za Agano la Kale tena, hebu tuchunguze pumziko hili la Sabato katika kitabu cha Waebrania. Kwa sababu mimi na Drenda tumegundua, humo kuna ufunguo muhimu sana wa Ufalme wa Mungu unaofanya kazi na kuleta riziki maishani mwetu jinsi Mungu alivyokusudia.

## **JAMBO LA KUSHTUA: SABATO SI SIKU TENA!**

Natumai taarifa hii imekamata umakini wako. Kumekuwa na mjadala mkubwa katika mwili wa Kristo kuhusu jinsi Sabato inapaswa kuadhimishwa: Jumamosi, Jumapili, au kuanzia machweo ya jua Ijumaa usiku hadi machweo ya jua Jumamosi jioni. Kuna madhehebu ambayo yamejengwa juu ya msingi wa utafsiri wao wa Sabato. Tafadhali usichukizwe na kutupa kitabu hiki chumbani huku ukifikiri mimi ni mzushi, tafadhali nivumilie kwa muda mfupi, na tuangalie Wakolosai 2:16–17.

*Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au Sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo.*

— Wakolosai 2:16–17

Sikiliza kwa makini kile Paulo anachosema. Siku ya Sabato ilikuwa ni kivuli cha mambo yaliyokuwa yakija; ukweli, hata hivyo, unapatikana katika Kristo. Siku ya Sabato ilikuwa kivuli, haikuwa kitu halisi. Ikiwa Kristo ndiye kitu halisi, basi siku ya Sabato ilikuwa ni kivuli cha kututambulisha Kwake na yale aliyoyafanya. Acha niseme hivi: Hakuna uwezo katika siku ya Sabato kuondoa au kubadilisha mfumo wa laana ya dunia ya kazi nzito yenye dhiki na jasho ambayo Adamu aliileta katika ulimwengu. Ikiwa unaihesimu siku ya Sabato kidini, haina uwezo wa kukuweka huru. Bali ni kivuli, picha, ya kile utakachokipata ndani ya Kristo.

Nilipokuwa katika darasa la kwanza, mwalimu wetu alituagiza sote

tuchore michoro ya upande mmoja wa vichwa vyetu. Walichukua projekta na kutuketisha mbele yake, na ikaonyesha kivuli cha vichwa vyetu kwenye karatasi nyeupe. Halafu wakachora vivuli vyetu kwenye karatasi hizo nyeupe na kuvipiga rangi nyeusi. Kisha tukakata michoro hiyo na kuipeleka nyumbani kwa mama zetu kuadhimisha Siku kuu ya akina Mama. Kivuli kilinasa mfano wangu, lakini hakikunasa asili yangu, tabia au utu wangu. Lakini kilitoa habari fulani kunihusu.

Sabato ilifanya vivyo hivyo. Kivuli chake kilisema tusifanye kazi nzito yenye dhiki na kutokwa jasho. Ilikuwa ni kivuli tu, si kitu halisi. Sabato ilikuwa ikituelekeza kwa Yesu Kristo, ambaye, kwa kweli, ametuweka huru kutokana na laana ya sheria na mfumo wa laana ya dunia na kutuimarisha tena kama wana na binti za Mungu na raia wa Ufalme Wake mkuu! Tena, ilikuwa ni picha ya kile ambacho Yesu ataturudishia siku moja. Ni kazi iliyokamilika ambapo kila kitu tunachohitaji maishani kimerejeshwa kwetu. Walakini, kama kitabu cha Waebrania kinavyosema, tunaingia katika pumziko hili kwa imani. Kumbuka, imani inahitajika ili kuifanya mbingu kuwa na mamlaka hapa duniani. Yesu alipaza sauti msalabani akasema, “Yote yamekwisha!” kama vile Mungu alivyosema yote yamekamilika mwishoni mwa siku ya sita.

Sabato kwa watu wengi leo ni siku ya kidini. Watu huitazama Sabato kama siku ya Mungu, siku ambayo tuna deni kwa Mungu kwenda kanisani, kufanya mambo kwa ajili ya Mungu, na kufanya mambo mengine ya kidini. Ilimbidi Yesu awasahihishe wanafunzi wake, waliokuwa na mtazamo uleule.

*Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato.*

— Marko 2:27

Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya Sabato. Je! wajua watu wengi huhisi hatia wanapokosa kwenda kanisani? Kwa nini wao huwa na hisia hizo wakati wao ndio kanisa? Sisemi hata kidogo kwamba tusikusanyike pamoja katika ibada, lakini mtazamo wa mawazo yao unaonyesha kwamba wana maoni potovu kuhusu Sabato.

Najua bado unaweza kuwa umechanganyikiwa, kwa hivyo hebu niende kwa undani zaidi kwa kutazama maoni ya Yesu katika Yohana 11.

*Basi Yesu alipofika, alimkuta amekwisha kuwamo kaburini yapata siku nne. Na Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu, kadiri*



*ya maili mbili hivi; na watu wengi katika Wayahudi walikuwa wamekuja kwa Martha na Mariamu, ili kuwafariji kwa habari ya ndugu yao. Basi Martha aliposikia kwamba Yesu anakuja, alikwenda kumlaki; na Mariamu alikuwa akikaa nyumbani.*

*Basi Martha akamwambia Yesu, “Bwana, kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa. Lakini hata sasa najua ya kuwa yoyote utakayomwomba Mungu, Mungu atakupa.”*

*Yesu akamwambia, “Ndugu yako atafufuka.”*

*Martha akamwambia, “Najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.”*

*Yesu akamwambia, “Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniadini hata kufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?”*

*Akamwambia, “Naam, Bwana, mimi nimesadiki ya kwamba Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu, yule ajaye ulimwenguni.”*

— Yohana 11:17-27

Yesu alisema Yeye ndiye ufufuo; haikuwa siku tu. Siku ya Sabato ilikuwa kivuli cha kile Yesu alichofanya msalabani kwa ajili yetu. Yesu ndiye Sabato ya kweli na ndani Yake tunapata kiingilio katika Ufalme wa Mungu na yote uliyo nayo. Kwa hivyo, tunaweza kupumzika!

Sasa turejee kwenye Maandiko yetu ya Agano Jipya katika Waebrania.

*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu yeyote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi.*

— Waebrania 4:9-11

Kivuli cha siku ya Sabato kinasema haukubaliwi kufanya kazi na kutokwa na jasho kwa kile unachohitaji katika siku ya Sabato. Kilikuwa kinatuonyesha kile Yesu alichofanya, ambacho ni kutukomboza kutoka kwa mfumo wa laana ya dunia wa kulazimika kufanya kazi nzito yenye dhiki na jasho ili kuishi. Kwa maneno mengine, picha hiyo ilikuwa dhahiri katika Kristo. Ujumbe wa kwanza Yesu aliohubiri ulilenga siku ya Sabato. Katika Isaya 61, tunapata maneno ya kwanza kabisa aliyoyahubiri, ambayo yanapatikana katika Luka 4.

*Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema.*

— Isaya 61:1

Kwa kusema kwamba kulikuwa na njia ya kutoka katika umaskini, alikuwa akisema kulikuwa na njia ya kutoka katika mfumo wa laana ya dunia ya kazi nzito na jasho. Utumwa huu wa kutafuta riziki ndio uliowafunga watu ili wasiweze kupata pumziko. Lakini siku ya Sabato haikuwa picha pekee ambayo Mungu aliwapa watu Wake kuhusu kile ambacho siku moja kingerudishwa. Pia kulikuwa na mwaka wa Sabato!

*Kila miaka saba, mwisho wake, fanya maachilio. Na jinsi ya maachilio ni hii, kila mkopeshaji na akiache alichomkopesha mwenziwe, wala asimlipize mwenziwe wala nduguye; kwa kuwa imepigwa mbiu ya maachilio ya Bwana. Waweza kumtoza mgeni; lakini kila uwiacho kwa nduguyo mkono wako utamwachilia.*

*Lakini hawatakuwako maskini kwenu; (kwa kuwa Bwana atakubarikia kweli katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, uimiliki, iwe urithi wako;) kwamba utaisikiza tu kwa bidii sauti ya Bwana, Mungu wako, uyatunze maagizo haya yote nikuagizayo leo, kuyafanya. Kwani Bwana, Mungu wako, atakubarikia, kama alivyokuahidi; nawe utakopesha mataifa mengi, lakini hutakopa; tena utayatawala mataifa mengi, usitawaliwe na wao.*

— Kumbukumbu la Torati 15:1-6

Tazama kwamba walipaswa kufuta madeni yote kila baada ya miaka saba. Tena tunamwona Mungu akitumia nambari saba kuonyesha kwamba kila kitu kimekamilika. Hakuna ukosefu; Yeye ametoa kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya mwanadamu. Lakini watu waliposhuku hekima Yake katika kuwaambia wasamehe madeni, alisema, “**Lakini hawatakuwako maskini kwenu; kwa kuwa Bwana atakubarikia kweli katika nchi akupayo, Mungu wako, uimiliki, iwe urithi wako.**” Aliendelea kusema kuwa walitakiwa kubarikiwa sana wawe wakopeshaji na sio wakopaji. Tena tunaona hapa kwamba mfumo wa laana ya dunia wa kazi nzito na jasho ulibatilishwa na sheria mpya ya uzima ambayo ilituina kutoka kwa laana ya sheria ya dhambi na mauti.

Kama ilivyokuwa katika siku ya Sabato, hawakupaswa kufanya kazi nzito na kutokwa na jasho kwa mwaka mzima; hivyo, hawakuruhusiwa

kupanda mimea yao. Hapa basi mambo yalikuwa mazito zaidi. Sio tu kwamba walipaswa kusamehe madeni yote, bali pia hawakuruhusiwa kupanda mimea yao. Kufikia hapa mtu anaweza kusema, “Ninaweza kuishi siku moja na kile kilicho kwenye jokofu, lakini kuishi mwaka mzima bila kufanya kazi ni vigumu zaidi.”

Kwa hiyo hapa tena, kivuli kinatuambia tuwasamehe wale tunaowadai. Aliwaambia hawangepaswa kutumia malipo ya madeni kwa sababu wangekuwa na riziki nyingi, jambo ambalo lingewafanya wawe wakopeshaji wala sio wakopaji. Madeni ni mfumo unaotokana na kutotoshelezwa, kwa hivyo Mungu angewaruzuku kabisa kiasi cha kutohitaji kulipwa madeni. Kivuli kinasema, “Usipande mimea yako,” maana yake, kuna njia mpya ya kuishi nje ya mfumo wa laana ya dunia. Sasa, haya yote yanapatikana katika Yesu Kristo.

Lakini subiri, kuna mambo mengine—picha kubwa zaidi ya kuonyesha watu wa Mungu bado ilikuwa inakuja. Iliitwa Mwaka wa Yubile.

## SURA YA 7

# HILI HALIWEZEKANI

Kile utakachosoma sasa ni cha kushangaza. La, acha nitumie maneno mengine. Kwa kweli utafikiri hakiwezekani kabisa. Ninazungumza kuhusu Mwaka wa Yubile, picha muhimu zaidi ya kile Yesu anataka kufanya katika fedha zako kilichoandikwa katika Agano la Kale, lakini ni watu wachache hata wanaojua au kuelewa kile inachosema. Tayari tumezungumza kuhusu siku ya Sabato na mwaka wa Sabato, vyote ambavyo ni vivuli vya kile tulicho nacho katika Kristo, lakini sasa tutazungumzia jambo muhimu kabisa, ambalo ni Mwaka wa Yubile.

Jina pekee linaonyesha kwamba linahusu sherehe, sivyo? Hata hivyo, katika suala la fedha, watu wengi—na ninaposema watu wengi, jambo la kusikitisha ni kwamba, hii inajumuisha Wakristo wengi pia—hawana mengi ya kusherehekea. Kama nilivyoshiriki, nimekuwa nikifanya kazi katika nyanja ya kifedha kwa miaka 36 sasa. Nimemiliki kampuni nyingi na nimefanyia kazi makumi, ikiwa sio mamia, ya maelfu ya watu katika fedha zao za kibinafsi. Kwa hivyo ninaelewa jinsi mambo yalivyo. Na ninajua gari jipya linalong'aa au nyumba kubwa ya kupendeza inatoka wapi. Kwa kawaida ni madeni na mashinikizo mengi. Sisemi kuna shida katika kuwa na gari zuri au nyumba kubwa. Lakini inagharimu pesa nyingi kuishi katika nyakati zetu.

Na mfumo wa laana ya dunia ni mfumo wa kuishi ambao kwa kawaida hauwaweki watu huru. Kwa kweli, kati ya maelfu na maelfu ya watu ambao nimekutana nao, wengi wao si watu wabaya. Wanafanya kila wawezalo wenyewe, na hawajui kuhusu Ufalme wa Mungu au kile ninachoshiriki katika kitabu hiki pia. Bila shaka, unajua kwamba mimi na Drenda tuliishi katika shinikizo la kifedha kwa miaka tisa mirefu na migumu hadi

tulipojifunza kuhusu pumziko la Sabato. Baada ya kuishi kwa njia hiyo kwa muda mrefu, unapoteza uwezo wa kutambua ni shida ngapi unazovumilia na kufikiria ni kawaida.

Miaka kadhaa iliyopita, Mungu alizungumza nami kuhusu mawazo yangu madogo na kunijulisha kwamba nilipaswa kufurahia Yubile, sherehe,

## **UNAPOTEZA UWEZO WA KUTAMBUA NI SHIDA NGAPI UNAZOVUMILIA NA KUFIKIRIA NI KAWAIDA.**

lakini sikuwa nikifanya hivyo. Naam, nilikuwa nimetoka kwa madeni; nilikuwa nimeshuhudia mambo ya ajabu; na nilikuwa na furaha na kuridhika. Lakini nilikuwa nimeacha kuota na Mungu alifahamu hilo, na alitaka nijinyooshe tena, ili niendeleo kuunda na kuwa na

ndoto. Nilikuwa na furaha lakini sikuwa na moyo mwororo tena.

Kama nilivyosema, nina kampuni ya huduma za kifedha, nilikuwa nikialikwa kila mwaka, na mmoja wa wachuuzi wetu, kwenye hafla za kusherehekea mafanikio ya mwaka uliopita. Kwa kawaida mikutano hiyo ilihudhuriwa na takriban watu 250 ambao ni wakuu na watendaji wa makampuni. Ilikuwa safari iliyolipiwa gharama zote za kwenda mahali pa kifahari sana, lakini kwa wale waliofanya kazi bora kabisa, walitambuliwa kwa njia maalum kwa kupewa hundi kama bonasi. Kwa sababu nilikuwa na shughuli nyingi za kuchunga kanisa kubwa, kuhudumu katika vipindi vya runinga, na kuendesha kampuni yangu, kila mara nilihisi kwamba sikuwa na wakati wa kujiandaa inavyohitajika ili kufikia kiwango cha juu cha kutambuliwa.

Lakini mwaka mmoja nilipokaa katika mkutano na kutazama washirika 10 wakuu wakitambuliwa na kupokea hundi zao za bonasi za \$100,000, niliingiwa na hatia. Niliwaza, “Hebu subiri kidogo! Ninapaswa kuwa pale kwenye jukwaa nikitambuliwa pia. Mimi ni mtoto wa Mungu na Roho Mtakatifu ndiye Mshauri wangu. Ninapaswa kuwa pale juu nikishiriki na kudhihirisha wema wa Mungu!” Kwa hivyo mimi na Drenda tuliamua mara moja kwamba tutakuwa kwenye jukwaa hilo mwaka uliofuata. Vipi? Hatukujua jinsi hilo lingetendeka.

Kwa miaka 10 awali, kampuni yangu ilikuwa imezaa takriban dola milioni 3 hadi 4 kila mwaka, lakini uzalishaji uliohitajika ili kufikia kiwango cha juu kabisa ulipaswa kuwa takriban dola milioni 11. Sikujua jinsi ya kufika kiwango hicho na hata sikuwa na uhakika kwamba hilo lingewezekana kwa sababu ya ratiba yangu. Jambo moja nililokuwa nimejifunza hata hivyo ni kwamba singeweza kutimiza hilo kwa nguvu

zangu mwenyewe. Kwa hivyo mimi na Drenda tuliomba na kutambua lengo letu, tukatoa matoleo ya kifedha kama mbegu, na kuachilia imani yetu kwamba jambo hilo limetimilika.

Ili kufupisha hadithi ndefu, mnamo Januari ya mwaka uliofuata, mwaka mpya ulipokuwa ukianza tu, Mungu alinionyesha jinsi ya kufikia lengo langu katika ndoto. Alinionyesha kile nilichohitaji kufanya; na ilimradi nifanye alichonionyesha, ningekifikia lengo langu. Je! wajua kwamba lengo letu la dola milioni 11 lilitimia mwaka huo kupitia kwa kuuza bima moja tu! Ilikuwa furaha kama nini kuwa kwenye jukwaa lile katika kongamano lililofuata na kupokea bonasi ya \$100,000 pamoja na wale wengine 10 waliokuwa bora katika kampuni zao. Je! wataka kujua jinsi jambo hilo lilivyofurahisha? Ilikuwa sherehe kubwa zaidi. Sio tu kwamba tulifikia lengo letu la kupata bonasi, lakini pia mapato yetu yalikuwa yamepanda kwa mamia ya maelfu ya dola mwaka huo. Hiyo inaonekana kama sherehe kubwa kwangu!

Kwa hivyo ninapoanza kuzungumzia tukio fulani la Agano la Kale kama vile Mwaka wa Yubile, usisinzie na kufikiria ni jambo lisilosisimua maana siyoye. Kumbuka, maisha ni bora unapokuwa na karamu, kwa hivyo hebu tuangalie tukio/sherehe kubwa zaidi ambayo Israeli ilisherehekea ili ujifunze jinsi ya kuwa na yako.

## Mwaka wa Yubile

*Nawe utajihesabia Sabato saba za miaka, maana, miaka saba mara saba; zitakuwa ni siku za Sabato saba za miaka kwenu, maana miaka arobaini na kenda. Ndipo utakapoipeleka pande zote hiyo baragumu yenye sauti kuu, siku ya kumi ya mwezi wa saba; katika siku hiyo ya upatanisho mtaipeleka baragumu katika nchi yenu yote. Na mwaka wa hamsini mtautakasa, na kupiga mbiu ya kuachwa mahuru katika nchi yote kwa watu wote wanayokaa; itakuwa ni yubile kwenu, nanyi kila mtu atairudia milki yake mwenyewe, nanyi mtarejea kila mtu kwa jamaa yake. Mwaka huo wa hamsini utakuwa ni yubile kwenu; msipande mbegu, wala msivune kitu hicho kimeacho chenyewe, wala msizitunde zabibu za mizabibu isiyopelewa. Kwa kuwa ni yubile; utakuwa mwaka mtakatifu kwenu; mtakula maongoe yake yatokayo shambani. Mwaka huo wa yubile mtairudia kila mtu milki yake.*

— Mambo ya Walawi 25:8-13

Ninapoanza kuzungumza kuhusu Mwaka wa Yubile, hebu niweke msingi wa mambo ambayo unapaswa kuwa umeona tayari. Mwaka wa Yubile uliadhimishwa kila baada ya miaka 50, mara tu baada ya mwaka wa Sabato, mwaka wa arobaini na tisa. Nafikiri tayari unaweza kuona tatizo kubwa likijitokeza, sivyo? Katika mwaka wa Sabato, Waisraeli hawakuruhusiwa kupanda mimea yao. Vile vile mwaka wa Yubile ambao ulifuata mwaka huo ulikuwa na matakwa sawa ya kutopanda mimea. Kwa hiyo kimsingi, Israeli haikuwa na mavuno kwa miaka miwili mfululizo na hivyo ilibidi wangojee mimea yao ikomae kisha wavune katika mwaka wa tatu kabla ya kujaza maghala yao tena. Hili lingeweza kuwa tatizo kubwa kwa mtu yeyote aliyefurahia kula chakula kizuri au aliyekuwa akipata riziki kwa kuuza nafaka. Musa alipotoa maagizo kuhusu Mwaka wa Yubile, unaweza kuwazia jinsi watu walivyochanganyikiwa. Bila shaka, wazo la kupumzika kwa miaka mitatu lilikuwa ni wazo zuri, lakini ilibidi mtu alipe gharama yake. Kitu cha kwanza walichomuuliza Musa waliposikia kuhusu jambo hilo kilikuwa, “Je, hilo lawezekanaje?”

*Na kama mkisema, Je! Mwaka wa saba tutakula nini? Angalieni hatutapanda mbegu, wala kuvuna mimea yetu; ndipo nitawaamria baraka Yangu iwe juu yenu mwaka wa sita, nao utazaa matunda hesabu ya miaka mitatu. Na mwaka wa nane mtapanda mbegu, na kuyala yale matunda, akiba hiyo ya zamani, hata mwaka wa kenda, hata matunda yake yatakapoletwa ndani, mtakula hiyo akiba ya zamani.*

— Mambo ya Walawi 25:20–22

Mungu aliwapa jibu la kushangaza ambalo tutatumia muda mwingi kuchunguza katika sehemu ya kitabu hiki iliyosalia. Alisema kwamba Yeye angewaamria baraka kubwa katika mwaka wa sita kwamba ungezaa mavuno ya kutosha kudumu miaka hiyo mitatu hadi wakati wa kuvuna upya baada ya Mwaka wa Yubile. Kuna ulinganifu hapa na siku za uumbaji. Biblia inasema kwamba Mungu alimaliza kazi siku ya sita ya uumbaji kisha akapumzika. Ingawa alipumzika, hakuwa amechoka bali alikuwa amekamilisha kila jambo. Kila kitu mwanadamu alichohitaji kilikuwa kimeumbwa na kilikuwepo kwa manufaa yake.

Mungu sasa alikuwa akiwaonyesha Waisraeli picha ya kuwa na riziki zaidi ya kutosha, ambayo iko kinyume kabisa na mfumo wa laana ya dunia ya kazi nzito yenye dhiki na kutokwa jasho. Alitaka wamuone Yeye kama

yule aliyewapa riziki yao na kwamba Yeye hutoa riziki kubwa. Tena, ingawa hii ilikuwa picha kwao ya utoaji wa Mungu katika nyakati zao, haikuwa mpaka Yesu alipokuja ndipo tulipoona maana ya hicho kivuli cha Agano la Kale. Kiasili, hakukuwa na njia ya kuishi miaka hiyo mitatu bila kupanda mimea. Vivyo hivyo, katika hali ya asili ya kuishi chini ya mfumo wa laana ya dunia, hakuna njia ya kushinda kifedha bila kutokwa na jasho siku zako zote. Huwezi kukimbia haraka vya kutosha katika kutimiza lengo lako. Jaribu kuchukua likizo ya miaka mitatu kutoka kwa kazi yako wakati una majukumu yanayongojea kushughulikiwa, na utakuwa umechochea uhakika wa kufilisika. Lakini Mungu alikuwa akijaribu kuwaonyesha picha ya njia mpya, ambayo Yeye mtoa-riziki kwa watu Wake, kama vile Adamu alivyopokea kila kitu Mungu alichokuwa amemwaandalia wakati wa uumbaji.

Kuna mambo mawili zaidi ambayo Mwaka wa Yubile unatuonyesha ambayo tunahitaji kuona. Tena tunaona ardhi ikipumzika, hakukuwa na dhiki wala kutokwa jasho katika mwaka huo wa hamsini. Pia utaona kwamba ardhi yote ilipaswa kurudishwa kwa mmiliki wake wa kwanza. Waisraeli walipovuka Mto Yordani, kila kabila na familia ilipewa ardhi ambayo wangemiliki kwa ajili ya kuzalisha chakula na mapato waliyohitaji ili kuendelea kuishi. Kimsingi, ardhi ilikuwa utajiri wao. Juu yake walipanda mimea na kufuga mifugo yao. Kwa hivyo kurudisha ardhi yote kwa mmiliki wake wa asili ilikuwa kumrudishia uwezo wa kuwa na ustawi.

Tena, hiki ni kivuli cha kile Yesu alichotufanyia. Kivuli kinasema kwamba ufanisi ulipaswa kurudishwa kwa raia wa taifa la Israeli. Ni kweli kwetu vile vile kwamba ufanisi wetu umerudishwa kwetu, kwamba urithi wa Ufalme wa Mungu ni wetu tena.

Kuna jambo la tatu ambalo Mwaka wa Yubile unatuonyesha, nalo ni kwamba watumwa wote walipaswa kuwekwa huru na kurudishwa kwa familia zao. Hili lilikuwa jambo kubwa. Tena, kivuli kinasema kwamba wewe si mtumwa tena bali mwana au binti. Ukweli katika Kristo unasema kwamba wewe si mtumwa tena bali mwana au binti mwenye haki kamili ya urithi na ustawi katika nyumba ya Mungu.

Kwa hiyo fikiria juu ya yale ambayo umejifunza hivi punde. Yesu alitrudishia kile ambacho Adamu alipoteza. Yesu alituweka huru kutokana na utumwa, na kutufanya wana na binti za Mungu. Alituweka huru kutokana na mfumo wa laana ya dunia wa kazi yenye dhiki na kutokwa jasho, huku akimpa Mungu fursa ya kubariki kazi ya mikono yetu kwa njia kuu. Ingawa Yesu alilipia vitu hivi vyote, lazima tujue jinsi ya kujumuisha



## **MARA TU UTAKAPOJIFUNZA KILE AMBACHO SABATO INATUONYESHA, MABADILIKO MAKUBWA YA KIFEDHA YANAWEZA KUTOKEA MAISHANI MWAKO.**

faida hizi katika maisha yetu halisi hapa duniani. Hapa ndipo Wakristo wengi hukosea. Kwa kutojua kwamba Ufalme hutenda kulingana na sheria, na kutojua haki zao kisheria kama wana na binti na raia, wanaamini kwamba Mungu huchagua kiholela yule atakayembariki. Kwa hiyo, hawasomi sheria za Ufalme zinazoleta furaha

katika kutekeleza yale ambayo Biblia inasema ni yao. Nakwambia, mara tu utakapojifunza kile ambacho Sabato inatuonyesha, mabadiliko makubwa ya kifedha yanaweza kutokea maishani mwako.

Mtu mmoja katika kanisa langu alianza kunisikiliza nilipokuwa nikifanya mafundisho kuhusu imani na jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi. Yeye na familia yake walijifunza sheria hizi pamoja. Mwaka mpya ulipokaribia, waliamua kwamba wangetumia haki zao za kisheria na kuamini kulipia nyumba mbili za kukodisha ambazo walikuwa wamenunua mwaka huo. Ikiwa ninakumbuka vyema, nafikiri ilikuwa jumla ya takriban dola 400,000 zilizohitajika kulipia nyumba hizo mbili. Kwa hiyo waliomba na kutoa matoleo makubwa kama mbegu ya kifedha ili kutimiza lengo hili la kulipia nyumba zote mbili katika mwaka huo. Hili lilikuwa jambo zito kwao kifedha, lakini bwana huyu alifanya kazi katika nyanja ambapo ingewezekana kupata wateja wa kutosha na/au kandarasi kubwa za wateja ambazo zingeweza kufadhili uwezekano huo. Familia yote iliomba kwa pamoja na kukubaliana kuwa hili lingetokea. Kila wiki, familia hiyo ilirejelea mradi wao na kusoma tena Maandiko ambayo yaliwapa msingi wa kisheria wa kutarajia mavuno hayo. Bila shaka, bwana huyu alikuwa na ufahamu kwamba ilimbidi atekeleze sehemu yake.

Kadiri mwaka ulivyoendelea, hakika mikataba michache mikubwa ikawa inawezekana, lakini katika mashirika yote makubwa, mikataba ya mamilioni ya dola hayazalishi haraka. Karibu nusu ya mwaka, kampuni ya bwana huyu ilipata fursa ya kufanya mauzo makubwa, kiasi cha kuchangia karibu asilimia 40 ya uzalishaji wote wa kampuni yake kwa mwaka. Kupitia kwa kamisheni hiyo ya uuzaji, aliweza kulipia nyumba moja ya kukodisha. Kuelekea mwisho wa mwaka, shirika lingine lilionyesha kwamba kwa hakika lilitaka kutia saini kwa kandarasi za mamilioni ya dola ambazo rafiki yangu alikuwa akiwapa pia. Lakini tarehe ya kutekeleza hilo iliendelea

kuhairishwa. Mkataba ungetayarishwa, kisha tarehe ingesogezwa mbele na hivyo kuhitajika kufanywa upya, kisha tarehe ingesogezwa mbele tena. Sasa katika majira ya masika rafiki yangu aliarifiwa kwamba timu ya usimamizi aliyokuwa akifanya kazi nayo ilikuwa imebadilishwa na timu mpya ingeingia na kuchukua nafasi hiyo.

Rafiki yangu aliingiwa na fadhaha; alijua maana ya hilo. Timu ya usimamizi iliyoingia haikufahamu kuhusu mkataba ambao haukuwa umekamilika, na hivyo bila shaka ulikuwa umebatilishwa. Angelazimika kuanza mchakato wote upya na timu mpya. Alipokutana na timu mpya ya usimamizi, ilionekana kwamba walipendelea kuangalia mapendekezo ya kampuni yake. Walipoyaangalia mwishoni mwa mwezi wa Novemba, walisema walitaka kutia saini kwa mkataba huo. Lakini tena, mkataba ulichelewa na kuandikwa upya hadi siku mbili kabla ya mwaka mpya. Rafiki yangu alipigiwa simu kwamba walitaka kukutana naye na kutia saini, na wangelipa pesa taslimu ikiwa angeweza kukutana nao na kutia saini siku hiyo. Rafiki yangu alilipwa kamisheni ya kutosha kufikia lengo lake la kulipia nyumba zote mbili katika mwaka ambao yeye na familia yake walikuwa wameelekeza imani yao.

Ni kwa kujifunza kanuni za Ufalme tu kulikomchochea kuwazia mradi mkubwa kama huo, kwa kuwa hakuwa amewahi kupata mradi mkubwa kama huo hapo awali au kupata pesa nyingi hivyo katika mwaka wowote awali, ambazo zingeonyesha kwamba lengo lake lingeweza kutimizwa. Aliniambia kwamba walikuwa na karamu ya kusherehekea ushindi huo!

Hadithi nyingine, “hili kweli lilitokea” ilitokea na mmoja wa watoto wangu. Bila shaka, watoto wangu wote wametazama Ufalme ukitenda kazi maisha yao yote. Wote wametumia kanuni ninazozungumzia na wamemwona Mungu akifanya mambo ya ajabu. Ingawa wako katika miaka yao ya ishirini, wote wamelipia magari yao; na wengi wao nyumba zao zimelipiwa kikamilifu au wako karibu kumaliza kuzilipia. Mwanangu mkubwa, Tim, alitaka kununua nyumba kwa pesa taslimu. Kwa hiyo alitoka matoleo ya kifedha kama mbegu yake, huku akimwamini Mungu kupata nyumba nzuri kwa bei aliyokuwa akitaka. Yeye pia ni mjuzi sana katika ujenzi, kwa hivyo hakuogopa kununua nyumba lililohitaji kukarabatiwa.

Alitumia muda kuangalia nyumba kadhaa lakini hakupata ile hasa aliyoienda. Lakini siku moja, alikuwa akiendesha gari na akaona nyumba iliyokuwa ikiuzwa ambayo hakuwa ameiona hapo awali. Ilikuwa nyumba ambayo ilikuwa imechukuliwa kutoka kwa mweka rehani maana alikuwa ameshindwa kuendelea na malipo yake. Nyumba hiyo ilihitaji ukarabati

kiasi fulani, lakini haikuwa mbaya. Alimpigia simu wakala wa nyumba na kumtaka ampe bei ya nyumba hiyo. Hakuamini alichosikia—dola 37,000. “Lakini je, hiyo inawezekanaje?” aliwaza.

Wakala alifanya uchunguzi kuhusu nyumba hiyo kisha akasimulia hadithi ya kushangaza. Kwa kweli nyumba hiyo ilikuwa imechukuliwa kutoka kwa mweka rehani, na iliorodheshwa kulipiwa \$110,000 kama miezi sita awali. Hiyo ndiyo iliyokuwa bei wakati huo lakini ilikuwa imeuzwa kwa \$160,000 miaka michache awali. Ilionekana kwamba hakukuwa na mtu aliyependezwa nayo kwa muda wa miezi sita. Basi benki iliendelea kupunguza bei, bila kujua kwa nini hakukuwa na mtu aliyetaka kuinunua. Lakini Tim na wakala wake walipochunguza kwa kina, walitambua ni kwa nini nyumba hiyo haikupendwa na mtu yeyote. Ilikuwa imesajiliwa katika jiji na anwani tofauti kabisa, na hata nambari yake ya simu pia haikuwa sahihi. Kwa hivyo hakuna mtu aliyejua kwamba nyumba hiyo ilikuwepo! Nyumba hiyo, ambayo ilikuwa mashambani mwishoni mwa barabara ndogo haikupitiwa na magari mengi. Bei iliendelea kupunguzwa hadi siku ambayo Tim aliiona. Ajabu! Nilimwambia Tim kwamba nyumba hiyo ilikuwa imefichwa kwa ajili yake tu! Aliipaka rangi upya na kuifanyia ukarabati kidogo kisha akaiuza kwa \$160,000.

Binti yangu Amy ni kiongozi wa sifa katika Kanisa la *Faith Life*. Yeye na Jason walihitaji nyumba kubwa zaidi maana familia yao ilikuwa imeongezeka kutoka kuwa wanafamilia wanne hadi kuwa watano. Katika msimu wa joto wa mwaka wa 2017 hapa Ohio, bei za nyumba zilikuwa juu zaidi, na zile zilizokuwepo kwa kawaida ziliuzwa chini ya wiki moja. Matumaini yao ya kupata nyumba kubwa vya kutosha kwa bei nafuu ya \$250,000 hadi chini ya \$300,000, yenye ekari 5 hadi 10, ambayo walitamani iwe na maji, hayakufua dafu. Mashamba ya ekari 1 ya eneo hilo yalikuwa yakiuzwa kwa dola zaidi ya 200,000 katika msimu huo wa joto. Baada ya kwenda hapa na pale kutazama nyumba nyingi, waliacha kutafuta na wakaanza kuomba. Walitoa matoleo ya kifedha kama mbegu kwa ajili ya lengo lao, kisha wakamwambia Bwana, “Tuna shughuli nyingi sana hatuwezi kuendelea kutafuta hivi. Unajua nyumba yetu ilipo, na tunakuomba utuonyeshe kwa wakati unaofaa. Hatutaangalia mtandaoni, wala kuongea tena na wakala wetu wa nyumba kuhusu jambo hili!

Lakini usiku mmoja, jambo la ajabu lilitokea. Binti yao, mwenye umri wa miaka minne alisema walipokuwa wakiingia nyumbani mwao, “Mama, wakati wa kuhama umefika.” “Unamaanisha nini?” Amy akamuuliza mtoto. “Ni wakati wa kuhamia kwenye nyumba yenye ngazi kubwa inayopanda

kwenda kwa chumba changu,” mtoto wake akasema. “Nyumba gani? Ulikuwa na ndoto?” Amy akamuuliza. Binti yake akasema ndio, aliota ndoto. Usiku huo baada ya kuweka watoto wao wawili kitandani, Amy hangeweza kusahau mazungumzo hayo kisha akamwambia mumewe Jason kwamba labda walipaswa kutafuta mtandaoni.

Naam, kwa kweli kulikuwa na nyumba iliyokuwa imechukuliwa kutoka kwa mweka rehani pia na iliuwa na ghorofa mbili, na mto mbele yake, kwenye ekari 10. Bei, hata hivyo, ilikuwa \$26,000 juu ya bei ya \$300,000 ambayo walikuwa wametolea mbegu yao ya kifedha. Waliwaza kwamba wangeweza kuomba wapunguziwe gharama, kwa hiyo walimpigia simu wakala wao wa nyumba. Wakala wao alikuwa akiondoka kuelekea Florida siku iliyofuata lakini angeweza kuwaonyesha nyumba ikiwa wangependelea hivyo asubuhi mapema karibu saa tatu. Jason na Amy walisema wangekutana naye huko.

Wakala alichelewa kufika, lakini nyumba ilionekana kuwa nzuri. Pamoja na ukubwa wote wa nyumba, ekari 10 za shamba, na mto mbele ya nyumba, kila kitu kilionekana kuwa sawa. Bonasi ilikuwa kwamba kulikuwa na misitu iliyozunguka mali yote; lilikuwa shamba la kustaaajabisha. Walipokuwa wakiingia katika nyumba hiyo, binti yao alipiga kelele huku akikimbia kwenye ngazi kubwa yenye muundo wa mviringo moja kwa moja hadi chumbani kwake. Ili kufupisha hadithi ndefu, Jason na Amy walisema wangependa kuinunua. Wakala alipochunguza taarifa kuhusu nyumba hiyo, aligundua kwamba mnunuzi yeyote aliyependezwa nayo alipaswa kutoa ofa yake kabla ya saa sita siku hiyo. Walikuwa na chini ya saa moja kufanya hivyo! Ikiwa mtoto wao wa miaka minne hangewaambia ndoto hiyo, na kama wasingeanalia mtandaoni usiku huo, nyumba ingechukuliwa.

Ofa yao ya \$326,000 ilikubaliwa. Walifurahi sana. Walipokagua nyumba, ingawa paa ilikuwa sawa, mkaguzi alisema ingehitaji kubadilishwa baada ya miaka 5 au zaidi. Jason alipata wazo. Aliamua kuomba benki ipunguze bei kwa sababu paa ilihitaji kubadilishwa baada ya muda mfupi. Wakala wao aliwaambia wasijaribu kufanya hivyo, kwamba nyumba hiyo ilikuwa ikiuzwa “jinsi ilivyo” na hakuwa amewahi kuona benki ikipunguze bei kwa nyumba kama hiyo kwa sababu ya kasoro fulani. Lakini Jason na Amy walihisi mioyoni mwao kuandika barua na kuomba benki ipunguze bei. Naam umekisia vyema, benki iliwapa nyumba kwa \$296,000, chini ya zile \$300,000 walizokuwa wakiamini Mungu kulipa. Mungu alileta nyumba kama walivyomwomba afanye. Walipomuuliza mthamani thamani ya nyumba hiyo, aliwajibu, “\$500,000.” Rafiki yangu,

hiyo ndiyo sehemu maradufu!

Kama unavyoona, watoto wangu wote wamekuwa wakiyafurahia maisha ya Ufalme. Kitinda mimba wangu, Kirsten, hivi karibuni alilipia nyumba yake ya kwanza pesa taslimu mwaka huu akiwa na umri wa miaka 20. Kwa jinsi gani? Wote wanajua jinsi ya kutekeleza mambo kwa njia ya Ufalme!

## SURA YA 8

# SEHEMU MARADUFU

Sasa ninataka kushughulikia kwa kina zaidi jinsi pumziko la Sabato linavyofanya kazi na jinsi unavyoweza kulitumia katika maisha yako binafsi. Ninataka kurudi kwa hadithi yetu ya Mwaka wa Yubile na kutazama andiko letu. Hapo tutapata jibu la Mungu kwa Waisraeli walipouliza jinsi wangeishi kwa miaka mitatu bila mavuno. Hilo ni swali nzuri!

*Na kama mkisema, Je! Mwaka wa saba tutakula nini? Angalieni hatutapanda mbegu, wala kuvuna mimea yetu; ndipo nitawaamria baraka Yangu iwe juu yenu mwaka wa sita, nao utazaa matunda hesabu ya miaka mitatu. Na mwaka wa nane mtapanda mbegu, na kuyala yale matunda, akiba hiyo ya zamani, hata mwaka wa kenda, hata matunda yake yatakapoletwa ndani, mtakula hiyo akiba ya zamani.*

— Mambo ya Walawi 25:20–22

Tunaona katika kifungu hiki kwamba Mwaka wa Yubile, pamoja na mwaka wa Sabato uliotangulia, yote iliwezekana kwa sababu ya mavuno makubwa yaliyotokea katika mwaka wa sita, yaani mwaka wa arobaini na nane (kutoka Yubile ya mwisho). Bila mavuno hayo makubwa, pumziko la Sabato lisingewezekana. Hebu tuangalie kifungu kingine ambacho naamini kitafafanua hili zaidi.

*Kila asubuhi kila mtu alikusanya mana kadiri alivyohitaji, na jua lilipokuwa kali, iliyeyuka. Siku ya sita, kila mtu alikusanya pishi mbili, na viongozi wa jumuiya wakaja na kumpa Musa*

*habari hiyo. Akawaambia, “Hili ndilo agizo la Mwenyezi-Mungu: ‘Kesho ni siku ya kupumzika, Sabato takatifu kwa Yehova. Kwa hivyo oka kile mnachotaka kuoka na kuchemsha mnachotaka. Kisha mhifadhi chochote kitakachosalia mpaka asubuhi.’”*

*Kwa hiyo wakaiweka mana mpaka asubuhi, kama Musa alivyoamuru, nayo haikunuka wala kupata funza ndani yake. “Kuleni hivi leo,” Musa akasema, “kwa sababu leo ni Sabato kwa BWANA. Hamtapata joyote ardhini leo. Siku sita mtakusanya, lakini siku ya saba, yaani, Sabato, hapatakuwapo.*

*Hata hivyo, baadhi ya watu walitoka siku ya saba kuokota, lakini hawakuipata. Kisha Mwenyezi-Mungu akamwambia Musa, “Mtakataa kushika amri Zangu na maagizo Zangu mpaka lini? Kumbukeni ya kuwa Bwana amewapa ninyi Sabato; ndiyo maana siku ya sita anawapa mkate wa siku mbili. Kila mtu atabaki pale alipo siku ya saba; hakuna mtu atakayekwenda kutafuta chakula.” Basi watu wakapumzika siku ya saba.*

— Kutoka 16:21-30 (Tafsiri ya ‘Manna’)

Kifungu hiki, bila shaka, kinazungumzia juu ya mana iliyoanguka kutoka mbinguni kila siku ili kuwalisha watu na kinaeleza kwamba isingonekana siku ya saba, yaani Sabato. Hawangeihifadhi siku hadi siku, kwa sababu ingeoza haraka sana. Siku ya sita tu ndio wangeweza kuikusanya na kuiweka usiku kucha bila kuharibika. Neno la ziada la kushangaza kuhusu sababu mana iliharibika haraka sana kila siku linapatikana katika **Kumbukumbu la Torati 8:16.**

*Aliyekulisha jangwani kwa mana, wasiyojua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako.*

Mungu alikuwa akilifundisha taifa kumtegemea kila siku kwa ajili ya chakula chao, bila shaka, lakini pia katika kila kitu maishani mwao. Mungu alifahamu walikuwa wakielekea katika hali ya kuhitaji mambo mengine zaidi ya chakula; hivi punde wangekabili miji yenye kuta na majitu. Ilikuwa muhimu zaidi kwamba wamtegemea kwa uthabiti katika hali hiyo maana hilo lingemaanisha kuwa na uzima au kifo.

Hebu turejee katika Kutoka 16:29. Hapa, unaweza kuona wazi kwamba pumziko la Sabato liliwezekana tu kutokana na sehemu maradufu

ambayo walipewa siku ya sita.

*Bwana amewapa ninyi hiyo Sabato, kwa sababu hii huwapa siku ya sita chakula cha siku mbili; kaeni kila mtu mahali pake, mtu awaye yote asiondoke mahali pake kwa siku ya saba.*

Je, waona hili? Pumziko la Sabato liliwezekana tu kwa sababu ya sehemu maradufu. Hili ni jambo muhimu sana nitakuomba uliandike.

## **PUMZIKO LA SABATO HALIWEZEKANI BILA SEHEMU MARADUFU!**

Acha niseme kwa maneno mengine. Isipokuwa una zaidi ya kutosha, hutawahi kupumzika kutokana na mbio na kutokwa jasho kwa mfumo wa laana ya dunia. Kama vile mimi na Drenda tunavyowaambia watu kila mahali tunapoenda, “Usipotatua suala la pesa, kamwe hutawahi kugundua hatima yako!” Kwa nini? Kwa sababu bila kuwa na ya ziada, hutakuwa na njia nyingine na utakuwa mtumwa wa unusuru maisha yako yote. Kumbuka tuliposoma awali kuhusu faida za Baraka ya Ibrahimu katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 28:11-13. Hapo tuliona wazi kwamba kuishi maisha ya unusuru sio hatima yako! Iwapo umesahau, hebu tuirejeele kwa mara nyingine.

*Bwana atakufanya uwe na wingi wa uheri, katika uzao wa tumbo lako, na uzao wa wanyama wako wa mifugo, na uzao wa nchi yako, katika nchi Bwana aliyowaapia baba zako kwamba atakupa.*

*Atakufunulia Bwana hazina yake nzuri, nayo ni mbingu, kwa kutoa mvua ya nchi yako kwa wakati wake, na kwa kubarikia kazi yote ya mkono wako; nawe utakopesha mataifa mengi, wala hutakopa wewe. Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu, wala huwi chini; utakapoyasikiza maagizo ya Bwana, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kufanya.*

— Kumbukumbu la Torati 28:11-13

Umaskini, unusuru, na kufilisika sio hatima yako. Unapaswa kuwa mkopeshaji wala sio mkopaji, kichwa wala sio mkia! Huu ndio utele wa



Ufalme wa Mungu. Hii ndiyo raha ya Sabato, kuwa na zaidi ya kutosha, yaani sehemu maradufu!

Ninajua unachofikiria, “Jamani, hilo linaweza kuwa jambo zuri, Gary, lakini maisha yangu hayaonekani hivyo hata kidogo.” Hiyo ni sawa, hatuungalii nyuma, lakini tunatazamia kile ambacho Mungu anasema na kutarajia kile Ufalme unasema kutuhusu. Bila picha sahihi, na ufahamu kwamba maisha yetu yanapaswa kuwaje, tutaanguka kwa hila na mitego na mawazo potovu ya mfumo wa laana ya dunia. Imani ni kudumu katika makubaliano na kile ambacho Mungu anasema, wala sio hali zetu.

Kabla sijashiriki nawe jinsi Mungu alivyonifundisha mimi na Drenda juu ya sehemu maradufu, nataka kukusimulia hadithi ambayo naamini ni hadithi nzuri kuhusu jambo hili katika Agano Jipya.

## **IMANI NI KUDUMU KATIKA MAKUBALIANO NA KILE AMBACHO MUNGU ANASEMA, WALA SIO HALI ZETU.**

Nafikiri umewahi kusikia hadithi ninayotaka kushiriki nawe mara nyingi hapo awali, lakini pengine si katika muktadha wa sehemu maradufu au ufahamu wa Ufalme ulio nao sasa. Tunaipata katika Luka 15, hadithi ya Mwana Mpotevu. Tena, kaa nami hapa. Najua umeisoma hapo awali, lakini

hebu tuisome pamoja tukiwa na maarifa mapya.

*Akasema, “mtu mmoja alikuwa na wana wawili; yule mdogo akamwambia babaye, ‘Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia.’ Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati. Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu.*

*Alipozingatia moyoni mwake, alisema, ‘Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, ‘Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako.’ Akaondoka, akaenda kwa babaye.*

*Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. Yule mwana akamwambia, 'Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistabili kuitwa mwana wako tena.'*

*Lakini baba aliwaambia watumwa wake, 'Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.'* Wakaanza kushangilia.

*Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, 'Mambo haya, maana yake nini?' Akamwambia, 'Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima.'*

*Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake, akasema, 'Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wo wote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinja yeye ndama aliyenona.'*

*Akamwambia, 'Mwanangu, weve u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.'"*

— Luka 15:11-32

Katika hadithi hii, tunaona kwamba yule mwana mdogo aliondoka nyumbani na sehemu yake ya mali. Haya ni maelezo muhimu ya hadithi kwani yanarejelea sehemu yake ya urithi. Kwa hiyo kumbuka kwamba huyu mwana mdogo alikwisha kupokea sehemu yake ya urithi; hangefanya madai yoyote tena kuhusu mali hiyo.

*Yule mdogo akamwambia babaye, "Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia." Akawagawia vitu vyake.*

— Mwanzo 39:1-6

Kisha, hadithi inatuambia mahali ambapo mtoto huyu mdogo alienda:

katika nchi ya mbali. Ni muhimu uelewe kwamba mtoto huyu aliondoka nyumbani kwa babake, ambayo inamaanisha kwamba aliacha riziki yake, ulinzi wake, na sheria za taifa alimoishi babake. Alienda katika taifa la mbali, lenye sheria tofauti na njia tofauti ya maisha. Nina hakika kwamba mwana huyu mchanga hakujuu alichokuwa akifanya. Alifurahia manufaa ya kuwa mwana alipokuwa akiishi katika nyumba ya babake. Yote ambayo babake alikuwa nayo yalikuwa yake alipokuwa nyumbani. Lakini kwa sababu isiyojulikana, alihisi ukosefu wa kitu fulani, labda kwamba hakuwa na fursa fulani zilizokuwa mahali pengine.

Ikiwa haujaelewa tayari, Yesu alikuwa akisimulia hadithi ya wanadamu, hadithi ya Adamu. Adamu ndiye mwana mdogo aliyeondoka kwa nyumba ya Baba yake katika hadithi. Adamu ndiye aliyehisi kwamba alikuwa na hatima nzuri mahali pengine kuliko kuendelea kumtumikia Mungu, Baba yake. Ninajua unachofikiria, “Basi, ikiwa Adamu ndiye mwana mdogo, ni nani mwana mkubwa katika hadithi iliyobaki?” Nitashughulikia swali hilo mwishoni mwa mjadala huu, lakini kwa sasa, kumbuka tu kwamba Adamu ndiye mwana mdogo aliyeondoka.

Ingawa walikuwa na kila kitu, Adamu na Hawa walidanganywa na kuamini kwamba kulikuwa na mahali pengine pazuri zaidi kuliko kukaa katika nyumba ya Baba yao. Adamu alipoasi nyumba ya babake na kuchagua kuondoka, alikuja chini ya serikali mpya, na ufalme mpya wenye sheria mpya za utendaji. Biblia inauita ufalme wa giza unaotawaliwa na Shetani. Nina hakika kwamba Adamu alishtushwa na umaskini na kutokuwa na tumaini kwa ufalme huu mpya. Mwanzoni, kila kitu kilionekana kuwa kizuri. Mradi alikuwa na pesa zake, maisha yalikuwa sherehe kubwa! Lakini alipogundua kwamba alifanya makosa, muda ulikuwa umekwisha. Kisha, alijikuta katika fadhaha maana urithi wake ulikuwa umepotea. Akili yake, ambayo wakati mmoja ilikuwa imejaa maono, sasa ilizingatia maisha ya kila siku ya unusuru. Hakukuwa na kesho tena. Daima ingekuwa leo na leo haina ahadi.

*Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote, akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati.*

Mwana mdogo sasa alijikuta katika ufalme ambao umefilisika kabisa, ufalme uliokuwa katika hali ndefu ya njaa kali. Mwana alijaribu kuelewa kile alichokiona—watu walikuwa wakifa njaa. Maana alikuwa akitoka

kwenye nyumba yenye utele, akili yake ilikuwa na wakati mgumu kutafakari alichokiona. Lakini maumivu ya njaa tumboni mwake yalimkumbusha kwamba alichokiona ni kweli. Ili kuishi, sasa ilimlazimu kuomba barabarani. Katika ufalme wa giza, dunia hutoa miiba na michongoma tu, na ili kupata mazao yoyote, lazima kazi yenye dhiki na jasho ifanywe. Hitaji lake kubwa lilimfanya mwana huyo kuomba watu wamsaidie. Lakini kila mtu alikuwa na shida ile ile. Hakuna mtu aliyemsaidia pakubwa kwa sababu wote walikumbana na njaa ile ile kali aliyokuwa nayo.

Wakati muafaka wa mabadiliko ulitokea hapa kwa mwana mdogo, mabadiliko ambayo yametathiri mimi na wewe na wanadamu wote. Kwa mara ya kwanza katika maisha yake yote, mwana mdogo aliomba kulipwa kama mtumwa, mfanyakazi wa kibarua, kufanya kazi nzito ya mikono. Huu ni upotoshaji kamili wa utambulisho wake wa kweli wa yeye ni nani haswa. Yeye hakuwa tena mwana wa mtu tajiri mwenye heshima na mali, bali alikuwa mlinzi, au mchinjaji, au wakala wa mali, au mjumbe wa kubeba barua, na orodha inaweza kuendelea na kuendelea. Sasa alijulikana kwa kazi aliyofanya wala sio utambulisho wake wa asili! Alipoteza utambulisho wake! Ili kusisitiza kupotea kwa utambulisho wake hata zaidi, Yesu alisema kwamba alikata tamaa sana kiasi cha kuchukua kazi ya kulisha nguruwe. Nguruwe walionwa kuwa wanyama wachafu kwa Wayahudi, na Yesu aliuambia umati kwamba mwana huyo mchanga sasa alikata tamaa sana kiasi cha kupoteza uwezo wa kuwa na kusudi lolote maishani mwake. Sasa aliishi maisha ya aibu na fedheha. Mrahaba aliokuwa akiufurahia wakati mmoja sasa ulikuwa kumbukumbu ya mbali.

*Alipokuwa amekwisha tumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wa nchi ile; naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wala hapana mtu aliyempa kitu.*

Natumai unaona ulinganifu kati ya hadithi hii na wanadamu leo. Wanaume wawili wanapokutana mara ya kwanza, wao husema nini? “Je, unafanya kazi gani?” au “Je, unafanya kazi wapi?” au “Je, wewe hufanya nini?” Unapomuuliza mtu yeye ni nani, kwa kawaida atakuambia kazi anayoifanya. Kwa nini? Kwa sababu katika mfumo wa laana ya dunia, sote tumepoteza utambulisho wetu, na tunajaribu kwa bidii kuupata tena. Huwa tunaiga mtu yeyote anayevutia na anayeonekana kuwa na umuhimu.

Haya yote yalitokana na uamuzi wa Adamu kuondoka katika nyumba ya Baba yake. Katika mawazo yetu ya unusuru, tumepoteza utambulisho wetu. Lakini jipe moyo, huyu mwana mdogo katika hadithi yetu hakudumu kwenye zizi; na tunapoendelea kusoma hadithi hii, natumai utagundua kwamba hauhitaji kudumu hapo pia.

Biblia inasema siku moja mwana huyu mchanga alirudiwa na fahamu na akakumbuka nyumba ya babake ambako hata watumishi walikuwa na chakula cha ziada. Nafikiri katika hali yake ya njaa kali alikuwa na kumbukumbu za milo yote ya ajabu aliyowahi kufurahia hapo awali. Mjomba wangu Harold alikuwa mwelekezaji wa redio ya ndege aina ya B-17, za kuangusha makombora katika Vita vya Pili vya Dunia. Alitoka katika jamii na familia ya wakulima. Kila Jumapili, mamake alikuwa akiandaa mlo mkubwa wa kuku wa kukaanga, viazi vilivyopondwa, mkate wa kujitengenezea nyumbani, maharagwe, na mboga nyingine nyingi tamu. Kwa kweli, kila wakati kulikuwa na mkate wa nyumbani au keki. Najua mwenyewe jinsi milo hiyo ilivyokuwa ya kupendeza kwa sababu mamake alikuwa nyanyangu.

Ndege ya mjomba wangu iliangukwa katika nchi ya Ujerumani wakati wa vita, na alikaa miezi mingi katika kambi ya gereza ya Ujerumani. Chakula kilikuwa haba sana. Siku moja, nilimuuliza mjomba wangu jinsi alivyoweza kunusurika siku hizo, naye akaniambia kwamba alichofikiria tu ni jinsi ya kufika nyumbani kula kuku wa kukaanga na viazi vya kupondwa vya mamake. Nina hakika kwamba mwana huyu mdogo alipitia jambo kama hilo na alitambua kile alichokuwa akikosa. Lakini hakuwa na madai zaidi juu ya mali ya babake, kwa sababu tayari alikuwa amepokea kila kitu alichowiwa kutoka kwa mali ya babake. Kwa hivyo alifanya mpango. Angeenda nyumbani na kumwomba babake amwajiri kama mtumwa. Akilini mwake, kufanya kazi kama mwajiriwa au mtu wa kibarua, ndio jambo lililokuwa limebaki pekee.

*Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistabili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Akaondoka, akaenda kwa babaye.*

Kwa hiyo alirudi nyumbani na mpango wake na kumsihi babake

apate nafasi ya kufanya kazi ili angalau apate mahali pa kulala na chakula. Lakini Biblia inaeleza tukio la kushangaza katika hadithi hii. Alipokaribia nyumbani kwao, baba yake alimwona kwa mbali na akatoka mbio kumlaki na kumkumbatia sana. Kuanzia wakati huu na kuendelea, hadithi hii inapaswa kuitwa hadithi ya upendo wa Baba kwa sababu baba huyo alimkumbatia ingawa alikuwa amefunikwa na samadi ya nguruwe. Kwa kufanya hivyo, wasikilizaji Wayahudi wa Yesu walifahamu kwamba kumkumbatia kungemfanya baba huyo kuwa mchafu kiroho. Lakini baba huyu alijitolea kuwa najisi kwa niaba ya mwanawe. Kisha akaitisha vazi bora zaidi lililokuwepo na akamvisha mwanawe ili kuficha uchafu wake. Alichukua pete ya muhuri iliyowakilisha mamlaka yake mwenyewe na kuirejesha kwenye kidole cha mwanawe. Alimpa viatu vya kuvaa, jambo lililomaanisha kwamba alipata mali yote tena. Lakini kitu cha mwisho ambacho babake alimpa kilimkasirisha mwana mkubwa. Baba aliitisha ndama mnono auawe na kuliwa kwa sababu ya kurudi kwa mwanawe. Mwana mdogo, ingawa hakustahili, alirudishiwa cheo na manufaa ya kuwa mwana aliyeheshimiwa waziwazi na kuwa uhuru kama mwana, na kurudishwa kikamilifu katika cheo chake cha awali kama mwana nyumbani.

Sawa, haya yote yana uhusiano gani na sehemu maradufu? Yana uhusiano mwingi mno. Yesu alitumia hadithi ya mwana mdogo kuondoka na kurudi kwa sababu wasikilizaji Wake, katika utamaduni wa Kiyahudi, wangeelewa maana ya hadithi hiyo na kile nitakachokuambia sasa. Katika utamaduni wa Kiyahudi, mwana mkubwa alipokea moja kwa moja sehemu maradufu. Ikiwa unakumbuka, mwana mkubwa hakuondoka nyumbani, bali ni mtoto mdogo aliyondoka na kurudi. Pia utakumbuka kwamba alipoondoka, alichukua sehemu yake halali ya urithi, sehemu yake ya kisheria. Sasa hakuwa na madai zaidi juu ya mali ya babake au kitu chochote kilichokuwemo. Lakini mwana mdogo aliporudi na baba akamrudisha kama mwana na, kumpa ndama mnono ili kusherehekea kurudi kwake, mwana mkubwa alikasirika. Katika mawazo ya mwana mkubwa, ndama huyo alikuwa wake kwa sababu ilikuwa sehemu ya urithi wake.

Hivyo jambo hapa ni hili. Ingawa ndugu mdogo tayari alikuwa amepata sehemu yake ya urithi, alifanywa mwana tena na sasa angefurahia sehemu maradufu. Hii ilimaanisha kwamba alipokea sehemu maradufu ya mali. Kwa mtazamo wa kaka mkubwa, hii haikuwa sawa, na kwa hasira, alimwambia babake hivyo. Alidai kuwa alikuwa mwaminifu kumfanyia kazi miaka yote hiyo na kwamba kaka huyu mdogo hakuwa amefanya lolote ila kuidhalilisha familia yao. Kwa nini basi alipewa sehemu maradufu?

Je, hii ilikuwa haki? Kwa mtazamo wa mfumo wa laana ya dunia wa kazi chungu na jasho, sote tunaweza kusema haikuwa haki. Labda tungemuunga mkono mwana mkubwa ambaye alikuwa amefanya kazi kwa uaminifu, kwamba alipaswa kudai ukosefu wa haki kwa sababu ya yale yote aliyokuwa amemfanyia babake.

Lakini tungefanya uamuzi wa kile kilicho haki kwa msingi upi? Je! si baba ndiye aliyepaswa kuhukumu na kuamua ni nani angetaka kuonyesha upendeleo wake? Mafunzo ya mfumo wa laana ya dunia ambayo sote tunayo yangemaanisha kwamba ikiwa baba alimpa mwana mdogo sehemu nyingine ya mali, basi mwana mkubwa angepata mali kidogo. Lakini sivyo. Baba alikuwa tajiri sana hata watumwa walikuwa na ya ziada. Vipi ilipohusu wana?

Shetani hataki ujue jinsi Mungu wetu alivyo mkuu au wewe ni nani hasa. Amekuwa akieneza uongo juu ya Baba yetu tangu mwanzo. Sera za bima zimekuwa zikidai kwamba majanga yanapotokea ni kitendo cha Mungu. Mashirika ya kidini hudai kwamba Mungu anapendezwa na nadhiri ya kuwa maskini. Watu hudai kwamba Mungu huwafanyia watu wema mambo mabaya. Shetani anataka uwe kipofu wa jinsi ulivyo na jinsi Baba yako alivyo mkuu ili usije ukapata fahamu zako na kumrudia kwa moyo wako wote. Ninakuhakikishia kwamba unapomgeukia, unapata mapokezi yaleyale ya mwana huyu mdogo katika hadithi hii.

Unaweza kuwa unauliza, “Mwana mkubwa ni nani?” Hebu tuone kama unaweza kumtambua.

*Basi, yule mwanawe mkubwa alikuwako shamba na alipokuwa akija na kuikaribia nyumba, alisikia sauti ya nyimbo na machezo. Akaita mtumishi mmoja, akamwuliza, Mambo haya, maana yake nini? Akamwambia, “Ndugu yako amekuja, na baba yako amemchinja ndama aliyenona, kwa sababu amempata tena, yu mzima.”*

*Akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi babaye alitoka nje, akamsihi. Akamjibu baba yake, akasema, “Tazama, mimi nimekutumikia miaka mingapi hii, wala sijakosa amri yako wakati wowote, lakini hujanipa mimi mwana-mbuzi, nifanye furaha na rafiki zangu; lakini, alipokuja huyu mwana wako aliyekula vitu vyako pamoja na makahaba, umemchinjia yeye ndama aliyenona.”*

*Akamwambia, “Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na vyote nilivyo navyo ni vyako. Tena, kufanya furaha na shangwe*

*ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana.”*

**SHETANI HATAKI UJUE  
JINSI MUNGU WETU  
ALIVYO MKUU AU WEWE  
NI NANI HASA.**

Mwana mkubwa alisema kwamba kwa miaka yote hiyo alikuwa amemtumikia babake, lakini kwa muda wote huo, hata siku moja babake hakuwa amempa hata mwana-mbuzi mmoja ili aweze kusherehekea na marafiki zake. Hebu nitafsiri alichokuwa akisema. “Baba, huna haki!” Lakini tazama kile baba alichomjibu. “Mwanangu, wewe u pamoja nami sikuzote, na VYOTE NILIVYO NAVYO ni vyako.”

Koma hapo!!!!

Sasa, unaweza kutambua mwana mkubwa ni nani? Mwana mkubwa alikuwa na shughuli nyingi sana za kumtumikia babake huku akiwa na maoni potofu ya kujiona kuwa mwadilifu ili kuweza kufurahia wema wa babake. Kila kitu ambacho baba alikuwa nacho kilikuwa chake wakati huo wote.

Umesema vyema, mwana mkubwa anawakilisha sheria ya agano la kale. Mwana wa kwanza hangeweza kamwe kufurahia manufaa ya nyumba ya babake kwa sababu alikuwa na shughuli nyingi sana ili kupata kibali cha babake. Ingawa mwana mkubwa alikuwa na haki ya kupata sehemu maradufu, ni mwana mdogo tu aliyeifurahia.

Wewe ndiye mwana mdogo!

Una sehemu maradufu. Wewe ni mwana asiyepokelewa kwa msingi wa kile unachofanya bali kulingana na jinsi ulivyo ndani ya Kristo—mwana au binti wa Mungu, anayefurahia urithi ambao haukulazimika kuufanyia kazi bali kuupokea bure kutoka kwa Baba yako.





## SURA YA 9

# ZAIDI YA KUTOSHA

Ninaelewa kwamba unaweza kuwa na mashaka na kichwa cha sura hii, lakini hapa ndipo unapoelekea, katika mahali pa zaidi ya kutosha. Si kwa sababu ninakuonyesha mpango wa hivi punde wa kupata pesa bali kwa sababu kama mtoto wa Mungu ni haki yako ya kisheria kufurahia wema

**DHANA YA SEHEMU  
MARADUFU, YAANI KUWA  
NA ZAIDI YA KUTOSHA,  
INAWEZA KUONEKANA  
KWAMBA SI WAZO  
UNALOWEZA KUFIKIRIA  
SASA LINAPOLINGANISHWA  
NA MAHALI UNAPOJIONA  
WAKATI HUU MAISHANI  
MWAKO. LAKINI HAPU NDIPO  
UNAPOHITAJI KUANZIA  
SAFARI YAKO YA KUWA HURU  
KATIKA MAWAZO YAKO.**

na ustawi wa nyumba ya Baba yako. Dhana ya sehemu maradufu, yaani kuwa na zaidi ya kutosha, inaweza kuonekana kwamba si wazo unaloweza kufikiria sasa linapolinganishwa na mahali unapojiona wakati huu maishani mwako. Lakini hapo ndipo unapohitaji kuanzia safari yako ya kuwa huru—katika mawazo yako. Mawazo yako yasipokubaliana na Neno la Mungu, kamwe hutafurahia faida Zake. Kwa hiyo inua macho yako kutoka kwenye kile unachokiona sasa na uyaweke kwenye kile ambacho Mungu anasema ni chako katika Ufalme Wake. Acha kubishana na kile Mungu anachosema maana hukioni maishani mwako. Badala yake, anza

kubishana na hali yako kupitia kwa Neno la Mungu, ukiamini kwamba lazima iambatane na yale yote Mungu anayosema ni yako. Mimi ni mtu kama wewe na ninakuambia ufanye jinsi nilivyofanya. Amini anachosema

Mungu! Neno la Mungu haliwezi kushindwa na litaleta mabadiliko katika hali yoyote. Kwa mfano, hapa kuna barua pepe niliyopokea kutoka kwa msikilizaji aliyekuwa na mashaka, maana alikuwa amesikia yote, au hakuwa amesikia yote?

“Nitajaribu kuweka miaka 22 ya shida katika sentensi chache izezekanavyo. Mimi na mume wangu tulikulua katika familia za Kikristo na tulihudhuria kanisa mara kwa mara. Tulihusika katika kikundi cha vijana, mafundisho ya Jumapili asubuhi, n.k. Tulipooana, mwaka wetu wa kwanza kifedha ulikuwa mzuri ... hiyo ilikuwa zaidi ya miaka 22 iliyopita. Tangu wakati huo, “suala la pesa” lilikuwa chanzo cha maumivu na mapambano daima, na imani yangu ilikuwa ikiyumba-yumba sikuzote kwa sababu sikuweza kuelewa ni kwa nini yale ambayo Maandiko yalisema yalipaswa kutukia hayakufanyika. Ikiwa Neno la Mungu linadumu na ni la milele na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, basi shida ilikuwa wapi? Ama alikuwa mtu aliyejitoa mhanga kwa sababu ya imani yake, mwongo, au kichaa!

“Songa mbele hadi Januari 28, 2013 ... nilimwambia mume wangu, ‘Mungu asipojitokeza nitaondoka.’ ... nilikuwa nimemalizana na kanisa na Mungu. Nilipotoka nyumbani kwenda kufanya shughuli chache, mume wangu hatimaye aliitikia kusihwa kwa Roho Mtakatifu na akampigia simu rafiki yetu mpendwa ili kuzungumza naye. Baada ya kumaliza mazungumzo, rafiki yetu alisema kwamba alikuwa na mafundisho fulani aliyotaka tusikilize—mafundisho ya Gary Keese. Alishiriki ushuhuda wake kuhusu kile kilichomfanyikia. Kwa hiyo, nilipofika nyumbani mume wangu aliniambia kile rafiki yetu alichokuwa amesema na kwamba angeenda kuchukua mafundisho hayo siku iliyofuata.

“Sijui kilichotokea (kwa sababu nilikuwa nimesikia vya kutosha kutoka kwa wachungaji na walimu kuhusu “mambo yote ya kiroho”), lakini nilimpigia simu, na nikamuuliza ikiwa angepatikana jioni hiyo. Katika usiku wenye theluji nyingi, nilifanikiwa kufika nyumbani kwake. Nilipokuwa nikiendesha gari, nilimwambia Mungu, ‘Afadhali hili liwe jibu letu!’

“Siku iliyofuata, tulianza kusikiliza mafundisho, na sote wawili tulistaajabishwa zaidi. Tulianza kuelewa mambo yote. Maandiko hayo yote kuhusu: imani, kushikilia sana yale tuliyoyakiri. Vipande vyote vya fumbo hatimaye vilikuwa vimeingia mahali pao. Tulikuwa tumesikia kuhusu Ufalme miaka michache awali, LAKINI hakuna aliyejishughulisha kufundisha MCHAKATO ... jinsi ya kufika mahali pa kusema ‘NDILO

HILO!’ jinsi ulivyofundisha.

“Kwa hivyo mara moja, tulitekeleza yale tuliyojifunza ... tulihitaji pesa za kulipa rehani yetu. Ilikuwa Alhamisi, na mume wangu alikuwa amemaliza kazi ndogo ndogo katika nyumba ya wazazi wangu... waliniuliza kila wakati kiasi cha pesa za kumlipa mume wangu (walijua mambo yalikuwa magumu). Nami niliwaambia, ‘Chochote walichotaka.’ Hazikutosha kulipa malipo ya rehani ... LAKINI ilikuwa bado Alhamisi tu.

“Ijumaa, tulikuwa tumepanga kuonana na rafiki aliyetuazima zile CD za mafundisho. Kulikuwa na dhoruba kubwa ya theluji, lakini mimi na mume wangu tulitaka kuketi na kuzungumza naye kuhusu Ufalme na jinsi unavyotenda kazi.

“Kabla yetu kuondoka, alitaka kuomba, kisha akatupa hundi ... Bwana alikuwa amesisitiza moyoni mwake apande mbegu ya kifedha katika maisha yetu. Hilo lilitushtua kabisa. Tulipoangalia hundi ... ilikuwa ZAIDI YA KUTOSHA kulipa rehani na bili zingine ndogo!

“Nilimwambia mume wangu hili tu ndilo nililohitaji! Nilipiga picha ya hundi hiyo ili kunikumbusha uaminifu wa Mungu. Naam, adui hakupenda kile alichokiona na mara moja (yaani ninamaanisha mara moja !!!!) alijaribu kuiba mbegu yetu. Tulikuwa tumeamua huu ulikuwa ukweli, na hatungezungumza chochote ambacho kingeharibu maisha yetu ya baadaye. Shetani hakukata tamaa ... lakini tulisimama kidete, huku ngao yetu ikiwa juu.

“Sasa kabla sijaendelea, ninataka ufahamu kwamba nilikuwa Muitaliano mwenye kichwa ngumu ambaye alikuwa amechoshwa na ‘mafundisho ya ustawi’ niliyokuwa nimesikia ... na mume wangu alijua hili. Muujiza wa kweli ni kwamba nilipata ufahamu kikamilifu na niliushikilia ... wakati mwingine mume wangu hunitazama na kujiuliza ni nini kilifanyika!

Kwa imani tulitoa matoleo ya kifedha kama mbegu ya kupokea kandarasi ya \$150,000 ya papo hapo kwa kampuni yetu ya ujenzi mnamo 3/13 ili kulipa bili zetu tulizokuwa tumechelewa kulipa, ushuru, n.k. Mnamo Aprili 5/13, tulipokea kandarasi mbili za jumla ya \$450,000 kwa SIKU MOJA!!!! Hii ilikuwa baada ya miezi miwili tu tangu tuanze kutumia kanuni za Ufalme.

Tulihusisha watoto wetu nao wakaona matokeo yao wenyewe. Sasa, wamejitengenezea orodha zao wenyewe, nao hutoa matoleo ya kifedha kama mbegu kutoka kwa pesa zao ndogo ili kupata kile wanachotaka. Tuna maandiko katika kila chumba, na mtoto wetu wa miaka mitano huyasoma na kutangaza, ‘Ninaamini nimepokea.’

Tunashukuru sana kwamba sasa tuna pesa nyingi zaidi za kutoa na kwamba tunakaribia kutoka kwa madeni na kuweza kukamilisha miito yetu!

Asante, Mchungaji Gary, kwa kuchukua muda kujibu barua pepe ambazo nilikuwa nikikutumia. Tunaelewa kwamba huna wakati mwingi, na kuchukua wakati kufanya hivyo kunaonyesha jinsi unavyotaka kushiriki ujumbe huu wa ajabu wa Ufalme mkuu wa Mungu.”

Huwa ninapokea barua pepe kama hizi kila siku. Watu kama wewe na mimi wanagundua ukweli kuhusu utambulisho wao katika Kristo, wanajifunza jinsi Ufalme wa Mungu unavyofanya kazi, na kufurahia manufaa yake. Kwa hivyo mimi na Drenda tuligundua je kanuni ya sehemu maradufu? Nitakuambia katika sura hii na jua kwamba hadithi zetu zitakutia moyo.

Mimi na Drenda tulipoanza kujifunza sheria na kanuni za Ufalme wa Mungu, maisha yetu yalibadilika sana, kama nilivyowaambia katika sehemu ya kwanza ya kitabu hiki. Tuliacha kuishi maisha ya siku hadi siku kifedha, kukabiliana na mashambulizi ya hofu, kutumia dawa za kupunguza wasiwasi, na kutokuwa na tumaini lolote na kuanza kuishi maisha yenye kusudi na riziki. Tuliona mambo yaliyotokea tena na tena ambayo yalitufanya tutulie na kusema, “Je! Uliiona hilo? Ajabu!” Mara kwa mara tuliona Ufalme wa Mungu ukifanya kazi kama vile Biblia inavyosema, na kujiuliza maswali kama, “Kwa nini au ni kwa jinsi gani jambo hilo lilitendeka? au “Je, tulitumia kanuni gani?” Ingawa tulikuwa tukifurahia kuwa na zaidi ya kutosha, kwa kweli hatukuwa na sehemu maradufu moja kwa moja kama vile hadithi nitakazokusimulia zinavyoonyesha. Tulikuwa tukifurahia sehemu maradufu, hata hivyo, hatukujua kile tulichokuwa tukiona kiliitwa sehemu maradufu hadi Mungu alipoendelea kuongeza ufahamu wetu juu yake. Kabla sijaeleza jinsi Mungu alivyotusaidia kuelewa zaidi kuhusu sehemu maradufu, nataka kusoma Maandiko yetu muhimu tena kwa dakika moja. (Maneno kwenye mabano ni maandishi yangu, si sehemu ya Maandiko halisi.)

*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha Yake [imani] amestarehe mwenyewe katika kazi [mfumo wa laana ya dunia wenye kazi nzito yenye uchungu, jasho, na unusuru] kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake [maana alikuwa amekamilisha uumbaji].*

— Waebrania 4:9-10

Kufikia sasa unajua kwamba pumziko hili la Sabato ni ahadi kwa kila mwamini wa Agano Jipya katika Kristo wala si jambo la Agano la Kale tu. Pia unafahamu sasa kwamba Sabato haiwezekani bila kuwa na zaidi ya kutosha, au kama tulivyoona katika Kutoka 16, sehemu maradufu. Tafadhali usichanganyikiwe na kufikiri kwamba kuwa na sehemu maradufu kunamaanisha kwamba katika kila hali utakuwa na pesa nyingi za ziada wakati Mungu anapotaka utekeleze mradi fulani.

Kumekuwa na nyakati katika maisha yangu ambapo Yesu ameniambia nitekeleze mradi fulani wala sikuwa na pesa kwenye benki. Nilitambua baadaye kwamba Mungu hakuhofu kamwe kuhusu ukosefu huo maana alifahamu zingetoka wapi. Ndio maana hakuruhusu zije mapema, adui asije akajaribu kutuibia kabla hazijahitajika. Acha nikuonye, fanya uamuzi wa kufanya hivyo ikiwa una uhakika kwamba umesikia kutoka kwa Roho Mtakatifu. Tena, Yesu asipokuambia utekeleze mradi bila fedha, usiendeleze mbele. Subiri hadi wakati wa Mungu na riziki itakapopatikana.

Kijumla, sisi kama waumini tumeitwa tuishi maisha ya utele kifedha. Sisi si masikini bali tunaweza kuwa wakarimu kila mara jinsi Baba yetu alivyo. Ninataja hilo kwa sababu nimepokea barua pepe nyingi ambapo watu walikimbilia kutenda jambo na wakakosa wakati wa Mungu. Sikiliza, kwa sababu Mungu amekuonyesha jambo fulani haimaanishi kwamba ni wakati wa kulitekeleza. Mara nyingi, anakupa mwelekeo na wakati wa kujiandaa. Katika uzoefu wangu, wakati wa Mungu ni muhimu kama vile kusikia mwelekeo kutoka Kwake.

Yesu alipoanza huduma Yake katika mji Wake wa asili, baada ya kubatizwa katika mto Yordani na Yohana Mbatizaji na baada ya siku 40 mchana na usiku katika jangwa, aliingia katika sinagogi la mtaa wao kisha akachukua kitabu cha Isaya na kufungua sura ya sitini na moja na kusoma. Tukio hili limeandikwa katika Luka 4:18–21.

*Roho wa Bwana yu juu Yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa, na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.*

*Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, “Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.”*

Bila shaka, walimkasirikia kwa kudokeza kwamba Yeye ndiye andiko hilo lilikuwa likirejelea. Lakini zingatia sana mahali ambapo Yesu aliacha kusoma. Mstari wa kwanza hadi wa pili wa Isaya 61 unasema,

*Amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu.*

Tazama kwamba Yesu alikoma katikati ya sentensi. Hokusoma, “na siku ya kisasi cha Mungu wetu.” Kwa nini? Kwa sababu alitaka kumalizia katika sehemu ya kwanza ya sentensi hiyo, “mwaka wa Bwana uliokubaliwa.” Mwaka wa Bwana uliokubaliwa ni upi? Ni Mwaka wa Yubile! Kimsingi Yesu alikuwa akitangaza kwamba kila kitu kivuli cha Siku ya Sabato, Mwaka wa Sabato, na Mwaka wa Yubile kilikuwa kikutuonyesha sasa kilikuwa kimetimizwa sasa kwa sababu alikuwa amekuja. Sura nzima ya Isaya 61 inatuambia kile Yesu ametufanyia. Kuhusu sehemu maradufu, angalia mstari wa saba hadi wa tisa.

*Badala ya aibu yenu mtapata maradufu, na badala ya fedheha wataifurahia sehemu yao; basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele. Maana mimi, Bwana, naipenda hukumu ya haki, nauchukia wivi na uovu; nami nitawalipa malipo katika kweli, nitaagana nao agano la milele. Na kizazi chao kitajulikana katika mataifa, na uzao wao katika kabila za watu; wote wawaonao watakiri ya kuwa wao ni kizazi kilichobarikiwa na Bwana.*

— Isaya 61:7-9

Hakika ninaelewa kuwa na aibu kwa sababu ya shida za kifedha. Mara nyingi nilijikuta nimefedheheshwa na kuaibishwa juu ya hali yetu ya kifedha. Nakumbuka wakati mmoja nilikuwa nimekusanya marafiki zetu wapatao 20 kula chakula cha jioni katika mkahawa wa mtaa wetu. Sikumbuki tukio la kipekee tulilokuwa tukisherehekea, lakini nilikuwa nimekubali kulipia sherehe hiyo. Nakumbuka nilikuwa na wasiwasi nyingi wakati wa kula kwa sababu sikuwa na pesa za kulipia hafla kama hiyo. Pesa nilizotarajia kupata kutoka kwa biashara niliyokuwa nikifanya zilikuwa zimechelewa.

Kadi pekee ya mkopo niliyokuwa nayo haikuwa imeghairiwa, lakini ilikuwa imefika mwisho na sikuwa na uhakika kama ningeitumia hata mara moja tu au la. Kwa hakika, tulipomaliza kula chakula kadi ilikataliwa. Ilinibidi niombe kwa unyenyekevu na aibu kubwa, mmoja wa wageni wangu alipie sherehe hiyo.

Doh! Nina hadithi nyingi kama hizo, lakini sina uhakika kuwa una vitambaa vya kupanguza machozi vya kutosha karibu nawe ili kusikiliza hadithi kama hizo. Lakini Mungu asifiwe, kupitia kwa Yesu, wote wanaotuona sasa hukiri kwamba tumebarikiwa na Bwana!

Sehemu maradufu ni yako, Yesu ndiye raha yako ya Sabato, naye ndiye sehemu yako maradufu! Ikiwa umesoma kitabu changu chochote cha awali, unajua kwamba Bwana alinifundisha mengi kuhusu Ufalme kupitia kwa kuwinda kulungu. Kwa kweli, kuwinda kulungu ndiko Mungu alikotumia kuvutia umakini wangu wa kwanza kuhusu Ufalme. Nilikuwa nimewinda kulungu kwa miaka kadhaa bila mafanikio. Ingawa nilikuwa nikitumia wakati na pesa katika juhudi zangu, niliishia bila mawindo. Kusema kweli, sikupiga hata risasi moja. Kulikuwa na mwaka nilikuwa nikifikiria kuhusu msimu wa kuwinda kulungu uliokuwa ukija, na Mungu akanena nami na kusema, “Kwa nini usiniruhusu nikusaidie na uwindaji wako wa kulungu mwaka huu?!” Bila shaka, sikujua hilo lilimaanisha nini, lakini aliniambia nichukue hundi na niandike, “Kwa ajili ya kulungu wangu wa 1987” kwenye sehemu ya kumbukumbu, kisha nichukue kiasi fulani cha pesa na kuzituma kwa huduma fulani. Pia aliniambia nimwambie Drenda nami tuweke mikono yetu juu ya hundi hiyo na kudai Marko 11:24 huku tukiombea.

**Marko 11:24** inasema,

*Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*

Ili kufupisha hadithi ndefu, nilienda kwenye eneo ambalo sikufahamu kabisa mwaka huo na nikapata kulungu wangu kwa takriban dakika 40. Mimi na Drenda tumefuata hatua hizi kwa miaka 30 iliyopita, na daima nimevuna kulungu wangu kwa dakika 30 hadi 40 kila mwaka tangu wakati huo. Kwa miaka mingi, nimekwona Mungu akifanya mambo ya ajabu sana nikiwa mawindoni, na nimejifunza mambo machache kuhusu sheria za Ufalme kupitia hilo pia. (Hadithi hizo zote za awali zimeandikwa katika kitabu changu *Faith Hunt*.)



Kawaida mimi hupendelea kuwinda nikitumia upinde na mshale wakati wa msimu wa joto kisha tena wakati wa msimu wa baridi nikitumia bunduki hapa Ohio. Kisheria, idadi ya kulungu unayoweza kuwinda karimu sana hapa Ohio. Kwa mwaka idadi ya mawindo inayokubalika ni kulungu sita. Sijawahi kuwinda kulungu wengi hivyo kulisha familia yangu. Jokofu langu kawaida huwa limejaa kulungu wawili au watatu kwa mwaka. Ili uweze kuelewa kile nitakachokuambia, unahitaji kufahamu kwamba miaka hiyo yote ya uwindaji wangu sikuwa nimewahi kuua kulungu wawili nikiwa nimeketi kwa mti mmoja iwe asubuhi au jioni. Ikiwa wewe si mwindaji, naam, huwa tunawinda tukiwa tumeketi kwa mti. Kwa kawaida, nilipoua kulungu mmoja, niliondoka msituni na kurudi siku nyingine ili kuwinda mwingine. Lakini Bwana alitaka kunifundisha jambo fulani jioni moja nilipokuwa nikiwinda.

Ilikuwa ni mojawapo ya siku nzuri za uwindaji wa majira ya vuli, wingu dogo na mvua nyepesi iliyolowesha ardhi mara kwa mara. Ilikuwa Jumapili jioni, nilikuwa nimechoka kidogo kutokana na kuongoza ibada kadhaa kanisani asubuhi hiyo, na nilikuwa nikitarajia kwenda msituni. Drenda alikuwa anaenda kununua vitu vichache, na mimi na yeye tulikubaliana kwamba huo ungekuwa usiku mzuri wa kuweka mawindo kwenye jokofu. Nilikuwa nikivaa vazi langu la kujisitiri huku nikikusanya vitu vyangu na kutoka kuelekea kwa gari. Nilipotoka nje alikuwa akiwasha gari ili kuondoka. Baada ya kuwasha gari, aliteremsha dirisha chini na kuniambia, “Sehemu maradufu.” Sikujua kwa nini alisema hivyo, ingawa baadaye alisema kwamba alimsikia Bwana akimwambia hivyo wakati huo na alihisi aliongozwa kuniambia hivyo.

Mwaka huo tulikuwa tumetoa matoleo ya kifedha kwa ajili ya kulungu watatu, na hiyo ilikuwa siku ya kwanza ya kuwinda katika msimu huo. Nikampiga busu la haraka kisha nikamwambia nimekubali, na nikatoka kuelekea kwa msitu wetu. Huwa ninawinda katika shamba langu mwenyewe, kwa hiyo nilifahamu sana mahali pa kwenda. Nilipoketi juu ya mti wangu, nilitoa sauti yangu ya kuguna mara kadhaa. Katika dakika 15, kulungu mkubwa mwenye pembe 8 alikuja mbio, nilimpiga risasi kwa umbali wa karibu mita 36, na kulungu wangu akaanguka chini. Hilo lilikuwa jambo la ajabu! Nilishuka chini na kwenda kulungu wangu dume, lakini nikakumbuka kile Drenda alichosema, sehemu maradufu, kwa hivyo nilimwacha pale alipokuwa ameanguka na kurudi kwa mti wangu.

Nilifikiri kwamba kelele niliyofanya nilipokuwa nikishuka, na kutembea huku na huku, kisha kurudi kwa mti wangu, usitaje harufu yangu

iliyokuwa imetawanyika kote, kwamba kwa kawaida singempata kulungu mwingine rahisi katika dakika chache zilizokuwa zimebaki za kuwinda kihalali jioni hiyo. Lakini katika dakika 15 za kuwa mtini, kulungu dume mwenye pembe ndogo alitembea moja kwa moja chini ya mti wangu, na nikamwangusha kwa pigo kamili la risasi. Ajabu, risasi mbili na kulungu wawili mfululizo kutoka kwa mti mmoja. Sikuwa nimewahi kufanya hivyo hapo awali. Hilo lilinivutia na nikajua ni sehemu maradufu ambayo Drenda alikuwa amezungumzia.

Katika miaka mitano iliyofuata, ilikuwa vivyo hivyo. Kila wakati nilipoenda kuwinda nikitumia upinde nilipata kulungu wawili kutoka kwa mti uleule kwa dakika chache. Nilijua hilo halikuwa jambo la kawaida, na nikaanza kukazia mawazo katika dhana ya sehemu maradufu, kisha nikatambua kwamba kwa mara nyingine tena Mungu alikuwa akinifundisha somo lingine kuhusu Ufalme Wake.

Tangu zamani nimependa bunduki na, bila shaka, napenda kuwinda. Nilikuwa na kusanyiko langu mwenyewe la bunduki nilizotumia kuwinda, na nilifurahia sana bunduki nilizomiliki. Mimi na Drenda tuna ekari 60 zenye ardhi na takriban ekari 25 za misitu na ekari zingine 15 zilizo na kinamasi. Katika misimu yoyote ya vuli, kinamasi hicho huwa kikavu au hujaa maji, kulingana na kiasi cha mvua iliyonyesha wakati wa majira ya joto.

Kulikuwa na mwaka ambao tulikuwa na mvua nyingi wakati wa majira ya joto, na hivyo kinamasi kilikuwa kimejaa maji wakati msimu wa vuli wa kuwinda bata ulikuwa ukiingia. Kila mara bata walikuja kwa kinamasi mwaka wowote kulipokuwa na maji, lakini sikujali sana. Lakini mwaka huo kulikuwa na makundi makubwa ya bata waliokuja kwenye kinamasi huku maji yakiwa juu sana, na sikuweza kujizuia. Ingawa sikuwa nimewahi kuwawinda hapo awali, nilifikiri kuteremka kwenda kwa kinamasi ili kujaribu kuwawinda. Naam, uwindaji ulikuwa mzuri. Kulikuwa na bata kila mahali, na tulikula bata kadhaa katika chakula cha jioni mwaka huo.

Nilipokuwa nikiwinda bata mwaka huo, niligundua kwamba mara nyingi bata walikuwa wakipita nje ya safu ya risasi. Nilikuwa nikitumia bunduki yangu ya kila siku, ya kuwinda sungura na ndege, lakini bata hao waliporuka nje ya safu ya risasi kidogo, nilikumbuka kwamba nilisikia kuhusu aina mpya ya bunduki ambayo ilikuwa imeundwa kwa ajili ya kuwinda bata pekee. Ilikuwa na rangi ya kuisitiri na ingeweza kuua bata wengi maana ilikuwa na nafasi ya kuweka risasi nyingi, jambo ambalo liliwezesha mtu kuifyatua mara nyingi. Nakumbuka niliwaza kwamba nilipaswa kwenda kiutafuta wakati fulani.

Basi ilitokea kwamba nilikuwa katika duka la mtaani la bidhaa za michezo mwezi mmoja baada ya msimu wa bata kuisha wakati niliona bunduki zilizokuwa zimeandikwa *waterfowl guns*. Niliziangalia kidogo, lakini bei ilikuwa \$2,000 na kwa kuwa sikuhitaji bunduki kwa kipindi cha miezi 10 hadi msimu wa bata ulipoanza tena, niliamua kusubiri na kutonunua. Lakini ghafula bila kutarajia nilisema kwa sauti, “Bwana, ningependa bunduki hii.” Sikufikiria sana kuhusu hilo nilipoondoka dukani, lakini baada ya wiki chache nilikuwa mnenaji katika mkutano wa mauzo ya kampuni fulani, si mkutano wa kanisa, bali mkutano wa mauzo ya kampuni. Mwishoni mwa mazungumzo yangu, Mkurugenzi Mtendaji alinishukuru kwa kuwazungumzia kisha akasema, “Tulitaka kukushukuru kwa kuzungumza usiku wa leo na zawadi.” Nilipigwa na butwaa alipotoa bunduki kama ile niliyoiona dukani wiki chache awali. Maneno yangu, “Bwana, ningependa bunduki hii,” na ukweli kwamba nilikuwa nimewapa watu kadhaa bunduki hapo awali ulileta mavuno hayo.

Katika kitabu cha kwanza cha mfululizo huu, *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa Mwaminifu*, nimezungumzia kanuni iliyosababisha bunduki hiyo kujitokeza. Ninaiita kanuni ya mundu, na inapatikana katika Marko 4:26–29. Ningependekeza upate nakala ya kitabu hicho ikiwa bado hujakisoma. Bunduki hiyo iliyojitokeza ilikuwa ya kushangaza kwa hakika, lakini sio hadithi hiyo ninayotaka kuzingatia bali ni kile ilichochochea ninataka kukuambia.

Baada ya bunduki hiyo kujitokeza, na nikatambua kile nilichofanya ili kusababisha mavuno hayo, nilifikiria kidogo kuhusu bunduki zingine ambazo ningependa kumiliki siku moja. Kwa kweli, nilikuwa nimetoa makumi ya bunduki, kwa hiyo niliwaza nijaribu kutumia sheria za Ufalme. Bunduki pekee ambayo sikuwa nayo ilikuwa bunduki yenye shimo mbili za risasi, moja juu nyingine chini. Ni bunduki nzuri, na kwa kawaida ni ghali sana. Kwa hivyo nikasema, “Bwana, ningependa kuwa na bunduki moja kama hiyo!”

Baada ya mwezi mmoja hivi, nilipigiwa simu na mshiriki mwenza wa huduma yetu, naye akasema kwamba alitaka kuninunulia bunduki aina ya hiyo. Nilifurahi sana kisha akasema angeituma kwangu. Naam, baada ya siku chache nilipokea bunduki mbili za kupendeza zenye shimo mbili, juu na chini! Tazama kwamba nilipokea bunduki mbili. “Ajabu,” niliwaza. Nilimpigia simu mwenzangu na kumshukuru kwa kunitumia bunduki hizo nzuri. Baada ya siku chache alituma zingine mbili. Nilipopiga simu ili kumshukuru tena, alisema, “Nilivutiwa sana kwamba ulinipigia simu

kunishukuru, nilitaka kukutumia mbili zaidi.” Nilishangazwa na zawadi, lakini nilianza kuona jambo fulani katika hilo. Bunduki mbili kila wakati? Ilisikika kama kuwa na sehemu maradufu.

Karibu miezi miwili iliyopita, nilikuwa nikifundisha asubuhi kanisani kisha nilifaa kufundisha katika kanisa tofauti jioni hiyo. Baada ya ibada ya asubuhi, mtu mmoja alinikaribia na kusema, “Nitakutumia bunduki nzuri aina ya *Browning* niliyo nayo.” Tena, nilisisimka. Ajabu ni kwamba katika ibada ya jioni katika kanisa lile lingine, mtu alikuja akasema, “Nimekuletea bunduki mpya kabisa ambayo ingali ndani ya kisanduku chake.” Ilikuwa bunduki nzuri aina ya Marlin 30/30, ambayo mara nyingi nilikuwa nimeitamani lakini sikuwa nimewahi kuimiliki. Tena, nilishangaa lakini nilianza kuelewa nilikuwa nikipata—sehemu maradufu.

Tena, majuma machache baada ya hilo, jambo lile lile lilitukia—nilipewa bunduki mbili kwa siku moja. Kweli, ninachoweza kusema ni kwamba bila shaka mimi nimebarikiwa na bunduki nzuri. Lakini kama kila hadithi ninayosimulia, mimi huuliza kila mara, “Hilo lilifanyikaje?” Bila shaka, tayari nimekuambia kwamba nimetoa bunduki nyingi hapo awali lakini sikuwa nimesema, “Bwana ningependa bunduki hii,” hadi wakati huo. Tena, hii ndiyo kanuni ya mundu unayohitaji kufahamu. Lakini zaidi ya kanuni ya mundu, nilikuwa nikipata sehemu maradufu kwa njia dhahiri sana na nilitaka kujua hasa jinsi nilivyoweza kufanya hivyo. Ninaamini Bwana alinionesha kwamba wengi wetu tumekosa kipengele hiki muhimu sana cha kuvuna kutoka kwa Ufalme, na nitatumia muda katika sura inayofuata kushughulikia mada hiyo. Lakini kabla sijafanya hivyo, lazima nishirikiki nawe jinsi mwaka huo ulivyoendelea.

Baada ya kupatiwa bunduki, tukio lingine lilitukia—na ni hadithi ya kushangaza ambayo imetokea kuhusiana na kuona sehemu maradufu wazi, kwa udhahiri, bila maswali. Hadithi hii inahusu na magari yangu, haswa gari langu aina ya Cadillac Escalade yenye rangi ya lulu nyeupe niliyopewa ambayo nilitaja katika sura chache zilizopita. Kama nilivyosema awali, mimi na Drenda si watu wa kupenda magari sana. Kwa kawaida huwa tunaziendesha hadi zinapoacha kufanya kazi au kuonekana vizuri.

Na tena katika hadithi hii, ninahitaji kutaja kwamba mimi na Drenda tulitoa magari kadhaa hapo awali na hatukuwa tumeweke mahitaji wazi juu ya imani yetu kuhusu kile tulichokuwa tunaamini kuvuna kutokana na utoaji huo. Lakini kama unakumbuka hadithi hiyo, tulipoendesha gari aina ya Escalade ambalo tulikuwa tumekodisha kwa ajili ya kongamano letu, tulisema, “Tunapenda gari hili; tunapaswa kupata moja kama hili,”

hatukutarajia mtu atupigie simu na kusema alitaka kutununulia gari hilo. Lakini, bila shaka, ndivyo ilivyotokea. Na, kwa kweli, hatukuwa tumemwambia mtu yeyote kwamba tulilitaka. Kwa hivyo kama nilivyokuambia awali, Escalade yenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe, ilijitokeza na ilikuwa ya kushangaza. Ninaipenda sana.

Lakini kuna jambo la ziada la kushangaza zaidi kuhusu hadithi hiyo lililotokea msimu huu wa joto uliopita. Tulikuwa tumeendesha Escalade hii kwa muda wa mwaka mmoja na nusu wakati majira ya joto yalipoanza, na siku moja taa ya kuonyesha kwamba kulikuwa na tatizo katika injini iliwaka. “Hakuna tatizo kubwa,” nikawaza, lakini nilitaka iangaliwe, kwa hivyo niliipeleka kwa muuzaji aiangalie. Walisema kweli hakukuwa na tatizo. Kifaa cha kupima mafuta kilionyesha kwamba mafuta kidogo yalikuwa yakiingia kwenye sehemu ya kutoa moshi, lakini hilo halingeleta tatizo lolote. Injini ingedumu kwa muda wowote niliotaka kuiendesha gari hiyo. Niliwauliza kwa nini mafuta yaliingia katika ile sehemu ya moshi. Wakasema kwamba gari langu lilikuwa limeongezewa mfumo maalum wa kutoa moshi baada ya kununuliwa, na walifikiri kwamba hiyo ndiyo sababu mafuta yalikuwa yakiingia mle. Lakini walisema injini yenyewe ilikuwa sawa na ningetarajia injini idumu kwa muda mrefu.

Siku moja, katika mazungumzo ya kawaida na yule mtu aliyekuwa amenipa gari hilo, nilitaja suala la taa hiyo kuwaka naye akasema, “Naam, nimeona hilo likifanyika kwa magari mengine kutoka kwa kampuni ya GMC.” “Kwa kweli,” akasema, “ni jambo la kawaida sana katika miundo ya zamani.” Kisha akasema kwamba hilo halingeathiri gari kwa njia yoyote na kwamba ningendesha gari hilo kwa miaka 10 au zaidi bila shida.

Alifahamu kwamba mimi na Drenda tulikuwa tumenunua nyumba huko Florida. Niliketi pale nikiwa nimeduwaa aliposema, “Wajua nini, wewe endesha gari hili hadi Florida ili uwe unaitumia kule, nami nitakununulia nyingine ya kuendesha hapa Ohio.” Naam, sasa nina Escalade mbili zenye muundo mfupi na rangi ya lulu nyeupe, ambazo ziko kamili kwa kila njia, kando na ile taa inayowaka wakati mwingine katika gari la kwanza. Magari yote mawili ni makamilifu kwa kila njia! Tena huu ulikuwa moja ya wakati tunaposema, “Je! uliona hilo?” Mimi na Drenda huwa tunashangaa tunapodesha magari hayo mazuri. Hatukulipia hata moja ya magari hayo. Lakini tulijua hii ilikuwa sehemu maradufu.

Sikuambii hadithi hizi ili kujisifu kwa njia yoyote, lakini rafiki, nimebarikiwa! Ninafurahia sehemu maradufu, ambayo unajua sasa, ni kuwa na zaidi ya kutosha. Nina sefu ya bunduki iliyojaa, ambalo ni

jambo la kuwa na zaidi ya kutosha. Nina magari mawili aina ya Escalade yanayofanana ambayo sikulipia. Nafikiri utakubali kwamba ni zaidi ya kutosha! Na sio kwamba ninakutia moyo kutafuta vitu vya kimwili, la sivyo. Huwa nashikilia vitu kwa ulegevu, na siabudu vitu wala kuvifuatilia. Ninamfuata Mfalme na Ufalme Wake, na katika Ufalme ninapata zaidi ya kutosha, sehemu maradufu!

Subiri, bado sijamaliza kushuhudia wema wa Bwana na sehemu maradufu.

Mke wangu amekuwa na hamu ya kununua nyumba kando ya bahari kwa miaka 20. La, acha niseme hilo tena. Amekuwa akitamani kuwa na

**NINAMFUATA MFALME NA  
UFALME WAKE, NA KATIKA  
UFALME NINAPATA ZAIIDI  
YA KUTOSHA, SEHEMU  
MARADUFU!**

nyumba huko milele! Yeye anapenda bahari sana! Kwa hivyo amekuwa akichunguza nyumba zilizo kando ya bahari kwa miaka mingi. Zamani kulipokuwa na nyumba aliyoienda, pesa zetu kwa kawaida zilikuwa zimefungwa katika miradi ya

huduma na hivyo ilitubidi tungoje.

Hata hivyo, mwaka huu nilikuwa nikiomba katika chumba cha chini huku nikifanya mazoezi kwa aina ya baiskeli isiyosogezwa. Ghafla, Bwana alinisisitizia kwa nguvu sana, “Mwambie Drenda aende Florida, kwenye mji huo ambao ametamani kuwa na nyumba, na umwambie anunue nyumba yake ya kando ya bahari wiki hii.” Ajabu, wiki hii? Niliposikia hilo, nilihisi moyoni mwangu kwamba jambo hilo lilipaswa kufanywa haraka. Kwa hiyo nilimweleza Drenda yale ambayo Bwana aliniambia, na tukawasiliana na rafiki yetu aliyeishi katika jiji hilo ili kuona kama angetaka kumtembeza Drenda kwa siku chache kutafuta nyumba. Naye akakubali.

Kwa hivyo Drenda alienda mtandaoni na kuandaa orodha ya nyumba 25 alizotaka kuangalia. Alipofika huko, Drenda alipunguza orodha yake ya nyumba 25 hadi 5 ambazo kulikuwa na uwezekano na moja aliyoienda. Basi nilisafiri kwenda kuungana naye kisha akanionyesha nyumba zile 5 na ile aliyoienda. Tulipunguza zile 5 hadi 2—ile aliyoienda na nyumba nyingine iliyokuwa nzuri sana lakini si nzuri kama ile aliyoienda. Lazima nikubali nilipoiona ile nyumba aliyoienda nilijua hiyo ndio iliyokuwa ya Drenda kisha tukaiwekea ofa. Mwenyewe alikubali ofa yetu na tukafanya mkataba wa kununua nyumba yetu mpya.

Baada ya wiki chache, tulipokuwa nyumbani Ohio tukiwa tumepumzika tu, Drenda alishtuka na kusema, “Hiyo ni nyumba yangu!”

“Najua,” nikasema, “Hii ni nyumba yako. Mungu aliniambia nikununulie nyumba yako kando ya bahari ile wiki nilikutuma kwenda Florida.”

“La,” akasema, “Huelewi; hiyo ni nyumba yangu.” Aliendelea kueleza kwamba alikuwa akitafuta nyumba kwa miaka kadhaa katika eneo hilo, na siku moja aliona picha ya ile nyumba tuliyokuwa tukinunua katika matangazo. Alipoiona, aliipenda. Alipenda kila kitu kuihusu, usanifu wa Kihispania wa Mediterania, mpango wa sakafu, na eneo ambapo ilikuwa. Alikumbuka kwamba aliweka kidole chake kwenye picha hiyo na kusema, “Bwana, nataka nyumba hii!” Lakini alifahamu nyumba hiyo ilikuwa ya bei ghali sana na tayari tulikuwa tumeweka pesa zetu kwa miradi mingine, kwa hivyo aliendelea kutafuta nyumba zenye bei nafuu kwetu wakati huo. Lakini hakupendezwa na nyumba nyingine, na hatukufikia hatua ya kufanya mkataba kwa nyumba yoyote. Hatukuwa na amani kuhusu nyumba yoyote nyingine.

Unapaswa pia kufahamu kwamba tulikuwa tumetoa matoleo ya kifedha kama mbegu kwa ajili ya nyumba karibu na bahari katika mji huo zaidi ya miaka miwili awali. Tuliendelea kukiri kwamba tuna nyumba ya pwani katika mji huo, tayari tunayo, na tuliipokea siku ambayo tulitoa matoleo. Ninakumbuka mahali na wakati ambapo tulishikana mikono na kukubaliana kwa ajili nyumba ya Drenda ya kando ya bahari. Lakini sasa tulipokuwa tumefanya mkataba, ghafila Drenda alikumbuka ile picha aliyोजना miaka miwili awali na kutambua kwamba nyumba ilikuwa ile ile, nyumba yake!

Baada ya kuchunguza historia ya nyumba hiyo, tuligundua kwamba mwenye nyumba alijaribu kweli kuiuza miaka michache awali, lakini haikuuzwa kwa hivyo akaacha kuiuza. Huo ndio wakati Drenda alikuwa ameiona picha ya nyumba hiyo ikiwa imeorodheshwa kuuzwa. Lakini mwenye nyumba alikuwa ameamua kuiorodhesha tena, na hilo lilieleza kwa nini nilihisi kufanya haraka katika kumtuma Drenda kwenda Florida na maagizo, “Unapaswa kununua nyumba wiki hii.” Atakuambia mimi huwa situmii pesa hivyo. Wakati muafaka ni kila kitu kwangu. Wakati huu, pesa zangu hazikuwa zikitumika katika miradi mingine na zilikuwepo kwa ajili ya kununua nyumba. Nina hakika kwamba kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakiitazama nyumba hiyo na ndiyo sababu nilihisi uharaka huo. Ajabu ni kwamba bei haikuwa imepanda tangu ilipokuwa imeorodheshwa miaka miwili awali wakati Drenda alipoiona kwa mara ya kwanza. Naamini Mungu alikuwa ameishikilia kwa sababu yake!

Lakini sehemu maradufu ya hadithi hii ndiyo hii hapa. Wakati

tulikuwa tukisubiri kumaliza shughuli za mkataba ili kulipia nyumba ile, tulipokea simu kutoka kwa mama ya Drenda. Walikuwa na nyumba nchini Canada kwa miaka 32. Tulikuwa tumesafiri kwenda huko mara kadhaa na tulipenda nyumba hiyo na eneo ambapo lilikuwa. Nyumba iko kwenye kisiwa juu ya maji. Bahari iko karibu futi 30 kutoka kwenye sitaha ya nyuma. Wazazi wa Drenda walikuwa wakizeeka na waliamua kwamba hawakutaka kugharamikia utunzaji wa nyumba hiyo kwa sababu ilikuwa mbali sana. Walikuja kwetu na kutuuliza ikiwa tungependa kuinunua na nikasema la. Ilikuwa safari ya masaa 31 kwa gari kutoka Ohio, na ingawa niliipenda, sikuona kwamba ni kitu ambacho ningeweza kufanya mara kwa mara kwa sababu na muda mrefu wa kusafiri. Kwa hivyo waliweka katika orodha ya nyumba za kuuzwa na wakala wao wa nyumba, lakini baada ya kujaribu kuiuza kwa miaka miwili, hakuna mnunuzi aliyeonyesha nia kubwa ya kuinunua.

Kwa hivyo sasa tulipokuwa tuingoja kumaliza shughuli za kununua nyumba yetu ya kando ya bahari, walitupigia simu wakatwambia walikuwa wamejaribu kuiuza nyumba hiyo bila mafanikio na walikuwa tayari kupunguza bei hadi nusu ikiwa tungetaka kuinunua na kuidumisha katika familia. Nilitafakari kuhusu hilo, kwamba watoto wangu walikua wakienda huko na ilikuwa katika eneo zuri. Kwa hivyo mimi na Drenda tuliomba kuhusu jambo hilo kisa tukasema kwamba tungeinunua. Tulikuwa na pesa za kutosha mkononi kuinunua. Kando na hilo, tulikuwa tumenunua ndege kwa ajili ya kampuni yangu mwaka mmoja awali, jambo ambalo lingetufanya tufike huko kwa massa 5 badala ya masaa 31 yaliyohitajika katika usafiri wa gari. Hilo lilifanya kwenda huko kuwe rahisi.

Baada ya kununua nyumba zote mbili, siku moja nilikuwa nimeketi ofisini mwangu, ghafla nikapata ufahamu, “Subiri kidogo, hiyo ilikuwa sehemu maradufu!” Mke wangu alikuwa ameota kuhusu nyumba ya kando ya bahari kwa miaka mingi. Sasa, katika muda wa miezi miwili tu, alipata nyumba kusini mwa Marekani, yenye joto wakati wa majira ya baridi nyingi lakini iliyo na joto jingi sana kiasi cha kutotumika wakati wa majira ya joto. Lakini nyumba ya kule Canada ilikuwa na halijoto bora wakati wa majira ya joto lakini baridi sana wakati wa majira ya baridi nyingi. Tuligundua kwamba sasa Drenda alikuwa na nyumba kando ya bahari katika majira yote mawili. Ajabu. Hakika tulisema, “Je, umeona hilo?” tulipolipia nyumba hizo mbili. Nafikiri utakubali kwamba tukio hili linaonekana na kusikika kama kuwa na sehemu maradufu! Jamani inashangaza!

Nimetumia mifano kadhaa ya jinsi Mungu alivyoleta mambo mawili-



mawili kwangu na Drenda, ambayo naamini Mungu aliyatumia kutuonyesha wazi jinsi sehemu maradufu inavyofanya kazi. Lakini nataka kuhakikisha usifikirie kwamba sehemu maradufu ni kuwa na vitu viwili tu. Ukweli ni kwamba sehemu maradufu ni kuwa na zaidi ya kutosha. Mungu alikuwa akitumia mifano hii ya kipekee ya vitu viwili ili kuvuta mawazo yangu kuhusu sehemu maradufu. Kwa hivyo haijalishi ni nini, kuwa na wingi wa chochote ni sehemu maradufu. Natumai umelewa ukweli kuhusu sehemu maradufu na pumziko la Sabato. Maisha ni ya ajabu sana katika Ufalme! Ninapoandika sura hii, nimeketi nyumbani kwetu Canada, nikitazama nje ya dirisha kwenye bahari. Shakwe wa baharini na bata wanacheza kando ya ufuo yadi 25 tu kutoka kwa nyumba yetu. Kuna amani, hakuna kujitahidi, nyumba imelipiwa, na ni baraka. Nina kazi ya kushiriki habari njema za Ufalme wa Baba yangu, mimi ni mwana katika nyumba Yake, raia wa Ufalme Wake mkuu, na ninafurahia sehemu maradufu!

Mimi na Drenda tunaweza kuandika hadithi nyingi sana za jinsi Ufalme wa Mungu na sheria zake zimebadili maisha yetu, na pia maelfu ya watu wanaotutumia barua pepe na hadithi zao. Kama nilivyoshiriki, unaweza kusoma mambo haya yote katika Biblia, lakini inasisimua sana kuona mambo katika Biblia yakitimia mbele ya macho yako.

Ningependa kuongeza neno la ziada hapa. Kwa kweli si rahisi kwangu kuambia watu jinsi Mungu alivyotubariki mimi na Drenda na kuhusu safari yetu. Mara nyingi watu hukosa kutuelewa vyema. Wakati mwingine wao hufikiri sisi ni tuna kiburi au tunajisifu. Au wanafikiri kwamba tumechukua pesa zao za zaka au sadaka zao na kuzitumia sisi wenyewe. Tafadhali elewa kwamba mimi na Drenda hatuchukui pesa kutoka kwa matangazo yetu ya runinga, na hatuchukui pesa zinazotoka kwa mauzo ya rasilimali zetu. Naam, bila shaka huwa tunalipwa mshahara, na kanisa tunaloliongoza. Lakini sisi ni wamiliki wa biashara na tumekuwa nazo tangu zamani, na Mungu huzibariki. Ninataka kuhakikisha unajua mioyo yetu katika kushiriki hadithi zetu za kibinafsi. Nilihisi kwamba nilihitaji kukuambia kile ambacho tumeona kikitukia, na kile ambacho Mungu ametufundisha kuhusu matukio hayo. Matokeo ninayoshiriki nawe sio matokeo ya Gary na Drenda Keese; sisi sio wema kiasi hicho! La, yale ambayo tumeona na kufurahia ni matokeo ya Baba

yetu na Ufalme Wake maishani mwetu. Tunashiriki hadithi hizi kwa sababu tunataka upate ufahamu! Sisi hatukuwa na chochote mwanzoni, na sababu pekee ya kuandika kitabu hiki ni kwa ajili yako! Nataka ujue jinsi mambo yanavyofanya kazi ili uweze kuelewa na kupokea yote Mungu aliyo nayo kwa ajili yako pia.

Elewa kwamba ninachukia umasikini na moyo wangu wote. Miaka hiyo tisa ya kuishi katika dhiki na hofu daima ilikuwa jehanamu halisi duniani! Natumai utakumbuka kuwa pumziko la Sabato ni lako na langu pia! Katika sura inayofuata, nitakusaidia kuelewa jinsi ya kuingia kwenye pumziko la Sabato.

Neno la ziada katika sura hii. Nilipomaliza kuandika sentensi hiyo hapo juu, katibu wangu alikuja ofisini kwangu na kusema kuna kijisanduku kilichokuwa kimetumwa kwangu. Nilishangaa kukifungua na kupata bunduki mbili nzuri sana. Ajabu, hilo lilinitia moyo! Ilikuwa ni kana kwamba Mungu alikuwa akisema “Amina” kwa yale niliyokuwa nimesema.

Baada ya kitabu hiki kuanza kuchapishwa na nikapokea vitabu vya kwanza vilivyokuwa vimechapishwa, nilifurahi kufundisha kanuni hizi kwa mara ya kwanza kwenye mkutano wetu wa Mapinduzi kule Atlanta. Nilifurahi pia kuwa na kitabu changu kipya ili kuwafikia watu. Nilipokuwa nikijiandaa kuelekea kwenye ukumbi kuhubiri, katibu wangu alinipigia simu akaniambia kwamba nilikuwa nimepigiwa simu na yule bwana ambaye alinipa bunduki za kwanza, alisema alihitaji kuzungumza nami mara moja. Basi nikampigia simu haraka. Alisisimka sana aliponieleza kwamba alikuwa ametoka kwenye ofisi ya shirika la kusafirisha vifurushi ambapo alikuwa amenitumia bunduki zingine mbili! Mbali na hilo, pia alikuwa amemtumia Drenda bunduki, na kwa sababu alifahamu hakuwa mwindaji, alimtumia \$1,500. Nilishtuka. Nilihisi kwamba Mungu tena alikuwa akithibitisha kile nilichokuwa nikifanya na alikuwa akiniambia niendelee. Watu wanahitaji kujua mambo haya—Mungu anataka uyajue! Basi nilipofika nyumbani, nilifurahi kufungua kijisanduku kile. Mimi na Drenda tulipokea bunduki mbili aina ya *Browning*, nzuri zaidi kupita zote nilizokuwa nimewahi kuona, na zilikuwa na shimo mbili, juu na chini. Zote zilikuwa mpya kabisa. Pia nilikuwa na nyingine ndogo aina ya *Browning* yenye rangi ya dhahabu, na Drenda bila shaka alikuwa na dola zake 1,500. Sehemu maradufu!

Unaweza kuwa unajiuliza kwa nini ninamiliki bunduki nyingi hivyo. Naam, lazima nikubali kwamba nina bunduki nyingi nzuri sana, na sio za bei ya chini, nami pia nilimwuliza Mungu swali hilo hilo. Naye Mungu akaniambia kwamba alikuwa ametuma bunduki nyingi za kupendeza na

za bei ghali kwangu ili kunipa fursa ya kuona jinsi alivyo na aina nyingi ya rasilimali, na kwamba riziki Yake ilikuwa zaidi ya ile niliyotarajia na zaidi sana kupita kuishi maisha ya unusuru. Naelewa hilo! Naona hilo!

## SURA YA 10

# SIRI YA SEHEMU MARADUFU

Nimeshughulikia maana ya pumziko la Sabato na jinsi linavyowezekana kupitia kwa sehemu maradufu. Swali ambalo linapaswa kuwa akilini mwako sasa ni, “Ninawezaje kupata sehemu maradufu?” Naam, nimefurahi umeuliza! Ili kupata jibu la swali hilo, hebu turudi katika hadithi ambapo Yesu aliwalisha wanaume 5,000 kwa mikate mitano na samaki wawili.

*Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi wake walimwendea, wakasema, “Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula.” Akajibu, akawaambia, “Wapeni ninyi chakula.” Wakamwambia, “Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula?”*

*Akawaambia, “Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame.”*

*Walipokwisha kujua wakasema, “Mitano, na samaki wawili.” Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza*

*kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*

— Marko 6:35-44

Tulizungumza hapo awali kuhusu hadithi hii, lakini kuna vidokezo vikubwa hapa kuhusu sehemu maradufu. Katika hadithi hii, Yesu alizidisha mkate na samaki kwa njia isiyo ya kawaida, na watu wote wakala mpaka wakashiba. Nafikiri kulikuwa na watu takriban 20,000, wakiwemo wanawake na watoto; na hakika kulishwa kwa watu wengi na mikate mitano na samaki wawili hadi kila mtu akashiba ni jambo la kimungu kabisa. Na kwa sababu hiyo, tunaweza kusherehekea Ufalme na jinsi ulivyofanya kazi. Lakini kulisha watu sio picha nzima ya kile kilichotokea, na ukimalizia hapo, utakosa kupata ufahamu wa sehemu maradufu. Hebu tuchunguze kwa kina zaidi.

*Wakala wote wakashiba. Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.*

Kwa hivyo maandishi yanatuambia nini? Kwamba baada ya kila mtu kuridhika, vikapu 12 vilivyojaa mikate na vipande vya samaki viliokotwa. Ufafanuzi wa sehemu maradufu ni kuwa na zaidi ya kutosha. Inatosha kuridhika, lakini vikapu 12 vilivyobaki baada ya watu kuridhika ni sehemu maradufu, yaani zaidi ya kutosha. Tafadhali hebu tofauti hiyo iingie ndani ya ufahamu wako kidogo. Nataka upate picha dhahiri ya sehemu maradufu katika akili yako. Sina muda hapa wa kueleza kwa kina jinsi Yesu alivyoleta nguvu za Ufalme katika hali hiyo ili kutekeleza sehemu ya kwanza ya hadithi hii—ya watu 5,000 kuridhika. Lakini unaweza kupata maelezo kamili katika kitabu cha kwanza cha mfululizo huu, kiitwacho *Mapinduzi Yako ya Kifedha: Nguvu ya Kuwa Mwaminifu*.

Badala yake, ninataka kuzingatia sehemu maradufu, kufurika, na jinsi ilivyotimia katika hadithi hii. Naam, ni hadithi ya kustaajibisha—watu 20,000 wote waliridhika, ajabu! Lakini kuna mengi katika Ufalme kuliko kutosheka tu, ingawa hakika unahitaji kuridhika kabla ya kufurika. Kuridhika ni kitu kizuri, lakini vipi kuhusu kesho? Ninachosema ni kwamba ikiwa lengo lako ni kuridhika tu, ni nini kitatokea utakapohisi njaa tena? Wakristo wengi wako katika hali ya kuridhika lakini hawapati sehemu maradufu. Ni sehemu maradufu inayoleta pumziko la Sabato

ya Mungu. Kutosheka ni suluhisho la muda tu. Hakusuluhishi tatizo la ukosefu wa riziki. Kuwa na ufahamu kwamba utahisi njaa tena hata wakati bado huna njaa hufungua mlango wa hofu, na hutufanya tukimbie juu na chini kufanya kazi tukiwa na mtazamo wa manusuru. Hapana, kuna njia bora ya kuishi kuliko kuzingatia kuridhika tu. Huwezi kujenga mambo mengi ukiwa na mtazamo wa kuridhika. Katika kiwango cha kuridhika maono huwekewa mipaka maana unazingatia leo pekee. Kuridhika tu ni lengo la kuishi chini ya mfumo wa laana ya dunia wa kazi nzito yenye uchungu na kutokwa jasho.

### **Kuridhika hutosheleza leo tu; lakini sehemu maradufu hujenga kesho!**

Hebu nikupe mfano wa jinsi utamaduni na Wakristo wengi wanavyofikiri. Ukiuliza mtu yeyote kuhusu hali yake kifedha utapata

**KUNA NJIA BORA YA KUISHI  
KULIKO KUZINGATIA  
KURIDHIKA TU. HUWEZI  
KUJENGA MAMBO MENGI  
UKIWA NA MTAZAMO  
WA KURIDHIKA. KATIKA  
KIWANGO CHA KURIDHIKA  
MAONO HUWEKEWA MIPAKA  
MAANA UNAZINGATIA LEO  
PEKEE.**

majibu mengi, labda sio majibu mengi mazuri. Lakini akisema, “Tunaendelea vyema,” muulize, “Kwa hivyo ulimaliza kulipia nyumba yako lini?” Pengine atakukodolea macho na kusema, “Nyumba yangu bado haijalipiwa. Nilimaanisha tu kwamba tunalipa bili zetu zote na tuna pesa kwa benki. “Vyema!” utamjibu, “Nyinyi mnaendelea vyema sana. Niambie, una zaidi ya \$10,000 kwa benki?” Bila shaka, nafikiri hakuna mtu anayeweza kuuliza swali hili, lakini ikiwa utauliza kisha wakujiibu, wanaweza kusema,

“La, lakini tuna \$800.” Bila shaka watu kama hawa wanafikiri wako katika hali nzuri kifedha kwa sababu wana gari zuri, nyumba nzuri, na pesa kidogo kwa benki. Wanaishi maisha ya kuridhika. Lakini kuna zaidi! Je, vipi kuwa na nyumba iliyolipiwa pamoja na \$100,000 au \$500,000 kwa benki? Hii ndiyo picha ya maisha kwa watu wengi. Kuridhika ni jambo jema na muhimu, lakini kuwa na vikapu 12 vya mkate na samaki nyumbani kwako ni zaidi ya kutosha, na hilo huleta amani!

Siku moja niliketi chini na mteja wangu na tukajadiliana juu ya fedha. Nilipokuwa nikiangalia madeni yake, niliona kwamba alikuwa na madeni

takriban \$40,000 kwa kadi za mikopo. Na nilipoangalia mali yake, niliona kwamba alikuwa na takriban \$40,000 taslimu katika akaunti yake ya hundi. “Joe,” nikasema, “hakuna tatizo hapa. Una pesa taslimu kulipia kadi zako tatu za mikopo kabisa. Kiwango chako cha riba kwa madeni ya kadi ya mikopo ni 18%, na kiwango cha riba cha akaunti yako ni 1%. Lipa madeni ya kadi na pesa taslimu! Lakini wajua nini? Joe hakutaka kufanya hivyo. Nilikaa pale nikiwa nimeshangaa, kisha nikamuuliza kwa nini. Alisema kuwa na pesa hizo kwenye akaunti yake ya hundi kulimfanya ajisikie salama na tajiri kifedha. Nilimtazama tu. “Unamaanisha nini kunakufanya ujisikie tajiri? Huu ni uongo. Ingawa una \$40,000 katika akaunti yako, ukweli ni kwamba huna \$40,000 kwa sababu unadaiwa na makampuni ya kadi ya mikopo \$40,000. Mtazamo wako ni wa uwongo, na unalipa pesa nyingi kuamini uongo.”

Tulizungumza kwa muda wa saa moja hivi, na hakuweza kamwe kuelewa kwa nini alipaswa kuzingatia kutumia sehemu kubwa ya pesa zilizokuwa kwa akaunti yake ya hundi kulipia madeni, pesa ambazo alinikumbusha kwamba alikuwa amefanyia kazi kwa bidii. Nilikata tamaa baada ya saa nyingine na nikarudi nyumbani. Alikuwa amedanganyika; hakuwa na usalama katika kujaribu kuhifadhi pesa hizo zilizokuwa kwa akaunti yake ya hundi. Ah, najua alihisi vizuri alipokuwa akipokea barua ya taarifa iliyoonyesha kwamba alikuwa na \$40,000 kwa benki. Lakini ili kupata picha halisi ya mahali alipokuwa, alihitaji kufungua bili za kadi ya mikopo pia.

Kuridhika ni jambo zuri, na kunaweza kukuvutia na kukuweka katika hali ya uwongo ya usalama. Unahitaji kutazama mbele kidogo na kufahamu kwamba kile ulichotumia hivi karibuni hakitaweza kukupa kile utakachohitaji baada ya masaa machache. Utahisi njaa tena. Ikiwa unatafuta suluhisho la haraka, riziki inayoridhisha haraka, utakosa kile kinachoweza kubadilisha maisha yako kabisa—sehemu maradufu.

Maana mimi na Drenda kifedha tulikulia katika mfumo wa laana ya dunia wa kazi yenye dhiki na kutokwa jasho, sote tulikuwa na ndoto moja, kutoka kazini! Nilitaja hili katika sura iliyotangulia. Hatukuwa na ndoto ya kufanya kazi zaidi au kupata fursa nyingine kwa sababu, kwa kweli, tayari tulikuwa tumelemewa na maisha na tulikuwa tukishikilia tu hadi likizo iliyofuata. Wajua, watumwa hawana ndoto ya kazi zaidi. Watumwa huota kitu kimoja—Ijumaa jioni, wala sio Jumatatu asubuhi. Kwa nini? Kwa sababu watumwa huota jambo moja tu—kutoka kazini. Sikiliza, mtazamo wa mawazo ya kulemewa na kutamani kutoka kazini hautakupeleka

popote. Hata kama malaika angeingia chumbani mwako na kukuambia wazo kutoka kwa Mungu, mtazamo wako bado ungekuzuia. Andika hili.

## **LAZIMA UWE NA MTAZAMO WA KUWA NA RIZIKI ZAIDI YA ILE INAYORIDHISHA ILI UWEZE KUNYAKUA SEHEMU MARADUFU!**

Kauli hii ndio ufunguo wa sehemu maradufu. Najua haieleweki vyema sasa, lakini itaeleweka. Ili kukuonyesha ninachomaanisha, nataka kuangalia kwa mara nyingine ile hadithi ya kuwalisha watu 5,000 kutoka katika kitabu cha Yohana, badala ya kitabu cha Marko. Yohana anasimulia hadithi ileile lakini mtazamo wake una maelezo ya ziada tusiyoyaona katika hadithi ya Marko.

*Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka. Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, “Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee chochote.”*

— Yohana 6:11-12

Katika hadithi hii, tunaona kwamba ni Yesu aliyewaambia waende kukusanya vipande vilivyobaki ili wasipoteze chochote. Nataka uelewe jambo hili. Ilibidi awaambie wafanye hivyo maana hawakuiona fursa hiyo. Jiweke katika mahali pao. Umeshiba na umeridhika, na unachotaka kufanya ni kulala chini na kupata usingizi. Kwa sababu ya mafunzo yako ya laana ya dunia na mawazo yako ya utumwa, unaporidhika, ni wakati wa kuacha kazi. Wajua, mawazo ya utumwa hufanya kazi wakati inapobidi tu, lakini ikiwa sio lazima, na yanaporidhika, huwa yanaacha kufanya kazi. Ilimbidi Yesu awaambie wakusanye chakula kilichokuwa moja kwa moja mbele ya macho yao. Vipande hivyo vilikuwa vimewazunguka pande zote, lakini hawakufanya jitihada yoyote kuviokota. Lakini tena, akilini mwao, vipande hivyo vilistahili nini ila kuachiwa ndege?

Yesu alikuwa akiwafundisha jambo muhimu sana. Yesu alitoa maelezo baada ya kuwaambia wakusanye vipande hivyo, kwamba wasiache chochote kipotee! Lakini hiyo inamaanisha nini? Kila mtu ameshiba, kila mtu ameridhika, na hakuna mtu anataka mkate na samaki zaidi, vema kwa sasa. Lakini shida ni hii—hakuna pumziko la Sabato bila kukusanya zaidi ya kile unachohitaji. Waisraeli walipokusanya mana siku ya sita, waliagizwa



kukusanya zaidi ya hitaji lao. Chakula cha ziada walichokusanya siku hiyo ndicho kilichokuwa riziki yao katika siku ya saba, yaani siku ya mapumziko. Yesu alikuwa akiwafundisha wanafunzi Wake kuwa na mtazamo wa kuwa na zaidi ya kuridhika ili kuweza kupata riziki kamili ya Ufalme. Tena, unaweza kujenga na sehemu maradufu lakini huwezi na kuridhika tu. Kuridhika hula mkate wa leo lakini vikapu 12 vilivyosalia hukupa fursa ya kuchagua kesho.

Hapa kuna kanuni muhimu ninayotaka ufahamu.

Ingawa wanafunzi hawakuona vipande hivyo hadi Yesu alipowaonyesha, Mungu **tayari alikuwa amewapa pumziko la Sabato**, sehemu maradufu. Lakini hawakuona hilo. Tayari Ufalme ulikuwa umeandaa chakula, umezidisha mkate na samaki, na kuwalisha watu hao wote—daima Ufalme hutoa sehemu maradufu. Mungu hatoi ili kuridhisha tu; **Yeye atatoa riziki zaidi ya kutosha milele**. Suala ni kwamba labda huioni!

*Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa.*

— Luka 6:38

Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa. Lakini aya hii haimalizii hapa. Kipimo chako kilichoshindiliwa na kusukwa-sukwa, ni riziki yako ya siku. Lakini mstari huu unaendelea kusema, “hata kumwagika!” Kumwagika ndiko sehemu maradufu. Siku zote Mungu hutoa sehemu maradufu, wala sio ili kututosheleza tu!!!! Lakini kama hujui hilo, na nafaka inamwagika, unaweza kuiacha imwagike chini maana unazingatia kabisa sehemu inayotesheleza tu ambayo iko mbele yako na hukujitayarisha kunyakua ile ya ziada. Ukifanya hivyo, utashindwa kunyakua na kufurahia sehemu maradufu. Lakini ukitambua jinsi Ufalme unavyotenda kazi, kwa kuwa na ufahamu na kutazamia riziki kamili, utakuwa tayari kuchukua hatua ya kunyakua yote yanayotoka kwa Mungu.

Hebu nikupe mfano mwingine.

*Simoni akajibu akamwambia, “Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno Lako nitazishusha nyavu.” Basi, walipofanya hivyo walipata*

*samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kuwasaidia; wakaja, wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama. Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema, “Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana.” Maana alishikwa na ushango, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioupata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni. Yesu akamwambia Simoni, “Usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu.”*

— Luka 5:5-10

Tulisoma sehemu hii ya hadithi hapo awali. Petro alikuwa na mashua mbili zilizokuwa karibu kuzama na samaki kwa sababu ya Ufalme. Hii ilikuwa kinyume na ufahamu wake kuhusu uvuvi na hilo lilimshangaza. Lakini ni nini kingetukia wakati mwingine ikiwa Yesu angesema, “Ee, Petro, nenda kule kwenye kilindi cha maji, nawe utaweza kuvua samaki wengi kadiri unavyotaka?” Je, unafikiri angechukua mashua mbili? Sidhani. Angekopa mashua nyingi kadiri ya nambari marafiki zake wangempa. Kwa nini? Kwa sababu angekuwa na matarajio tofauti na ujuzi wa jinsi Ufalme unavyotenda.

Hoja ya mjadala huu mzima ni kuhakikisha umeelewa kwamba huwa hupati riziki yote ambayo Mungu hutuma kwako. Bila shaka, mara nyingi riziki hiyo haikuji kwa njia ya pesa taslimu. Bali inaweza kuja kwa njia ya mawazo, uteuzi wa kiungu, na maelekezo ya Roho Mtakatifu. Ikiwa hatujaandaliwa na ufahamu sahihi kuhusu sehemu maradufu, tutatembea moja kwa moja kando ya riziki yetu na kutoipokea kwa sababu tumefundishwa kuishi chini ya mfumo wa laana ya dunia wa kunusurika.

Katika hadithi ya mkate kuzidishwa, Yesu alikuwa akiwafundisha wanafunzi Wake jinsi Ufalme unavyofanya kazi, kile cha kutarajia na kutazamia. Kwa sababu mtazamo wao wa utumwa haukuona fursa katika mkate uliokuwa umetanda, ilimbidi awafundishe kutazama: “Mnaona nini? Tazama! Hamwoni yote ambayo Mungu amewaandalia.”

Nataka kukukumbusha Kutoka 16 kwa muda mfupi maana kuna jambo moja zaidi ninalotaka kutaja.

*Kila asubuhi kila mtu alikusanya mana kadiri alivyohitaji, na jua lilipokuwa kali, iliyeyuka. Siku ya sita, kila mtu alikusanya*

*pishi mbili, na viongozi wa jumuiya wakaja na kumpa Musa habari hiyo. Akawaambia, "Hili ndilo agizo la Mwenyezi-Mungu: 'Kesho ni siku ya kupumzika, Sabato takatifu kwa Yehova. Kwa hivyo oka kile mnachotaka kuoka na kuchemsha mnachotaka. Kisha mhifadhi chochote kitakachosalia mpaka asubuhi.'"*

*Kwa hiyo wakaiweka mana mpaka asubuhi, kama Musa alivyoamuru, nayo haikunuka wala kupata funza ndani yake. "Kuleni hivi leo," Musa akasema, "kwa sababu leo ni Sabato kwa BWANA. Hamtapata yoyote ardhini leo. Siku sita mtakusanya, lakini siku ya saba, yaani, Sabato, hapatakuwapo.*

*Hata hivyo, baadhi ya watu walitoka siku ya saba kuokota, lakini hawakupata. Kisha Mwenyezi-Mungu akamwambia Musa, "Mtakataa kushika amri Zangu na maagizo Zangu mpaka lini? Kumbukeni ya kuwa Bwana amewapa ninyi Sabato; ndiyo maana siku ya sita anawapa mkate wa siku mbili. Kila mtu atabaki pale alipo siku ya saba; hakuna mtu atakayekwenda kutafuta chakula." Basi watu wakapumzika siku ya saba.*

— Kutoka 16:21-30 (Tafsiri ya 'Manna')

Kama vile tumekuwa tukisema, sehemu maradufu ndiyo iliyofanya pumziko la Sabato liwezekane. Lakini cha kustaajibisha ni kwamba, ingawa Mungu tayari alikuwa ametoa sehemu maradufu siku ya sita, wengi wao walikwenda kuitafuta lakini hawakupata hata kidogo siku ya Sabato. Sio kwamba Mungu hakuwa mwaminifu kuitoa. Hawakuiona tu kwa sababu hawakuelewa vyema kuhusu sehemu maradufu ambayo tayari ilitolewa siku ya sita. Walikuwa wamekusanya mana ya kutosha siku moja, kama kawaida. Sasa, walihisi njaa siku ya saba lakini hawakupata hata kidogo. Labda kwa mtazamo wao Mungu hakuwa mwaminifu. Lakini Mungu hakuwa ameshindwa; bali walikuwa hawajafahamu kanuni ya sehemu maradufu. Ikiwa wangepanga, wangepanga vingine.

Je, ni watu wangapi leo wanaozunguka-zunguka wakijaribu kutafuta wanachohitaji, bila kutambua kwamba Mungu amekwisha kukitoka? Ni ajabu sana katika kifungu hiki kwamba Mungu alikasirishwa nao kwa kutokusanya mana ya kutosha!!!! Sijui kama hili linaweza kuhubiriwa katika makanisa yetu.

*Na Yeye ampaye mbegu mwenye kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa mbegu za kupanda na kuzizidisha, naye*

*atayaongeza mazao ya haki yenu; mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu.*

— 2 Wakorintho 9:10-11

Paulo yuko wazi sana hapa anapofafanua matokeo ya Ufalme wa Mungu kama kufanywa tajiri katika kila njia ili kwamba wewe uwe mkarimu kila wakati. Rafiki yangu, hilo linahitaji sehemu maradufu. Huwezi kuwa mkarimu kwa kila wakati bila zaidi ya kutosha.

Katika sura ya awali, nilishiriki nawe jinsi biashara yangu ilitoka katika kiwango cha uzalishaji cha dola milioni 3 hadi 4 kwa mwaka kupitia kwa mmoja wa wachuuzi wetu hadi kufikia zaidi ya milioni 11 kwa mwaka. Ongezeko hili lote lilitokea katika mwaka mmoja tu. Pia nilikuambia jinsi hilo lilivyotokea, kwamba Mungu alinipa ndoto usiku na kuniambia jinsi ya kulitekeleza. Lakini sasa nahitaji kukuambia alichoniambia kwa sababu kitakuwa na maana kwako. Katika ndoto yangu, alinipa maneno matatu tu. Hiyo ni kweli, maneno matatu tu. Maneno hayo matatu yalibadilisha mapato yangu kwa mamia ya maelfu ya dola mwaka huo bila mimi kufanya uuzaji au utangazaji zaidi ya ule niliokuwa nikifanya. Sikubadilisha chochote katika kampuni yangu ila mimi. Maneno hayo matatu yalinipa maagizo ya kubadili jinsi nilivyokuwa nikifanya jambo fulani, na mabadiliko hayo yalizidisha biashara yetu na mapato yetu mara nne. “Maneno hayo matatu ni yapi?” unauliza. Ndiyo haya—Nyakua Kila Fursa!

Naam, nyakua kila fursa. “Hayo tu? Hayo maneno matatu yalisababisha matokeo hayo yote?” Ndio. Ukishaelewa kuwa Mungu DAIMA hutuma sehemu maradufu pamoja na riziki Yake, utaelewa alichokuwa ananiambia.

Kampuni yangu, kama kampuni zingine zote za uuzaji, hupata faida yake kwa kusaidia watu. Kadiri kampuni inavyokuwa bora katika kusaidia watu, ndivyo watakavyopata pesa nyingi zaidi. Ingawa hii ni kweli, ni kweli pia kwamba makampuni mengi ya uuzaji hushindwa kukidhi mahitaji ya wateja wao kwa kutowafuatilia vyema au kutotafuta wateja wapya.

Kwa upande wetu, tulikuwa na shughuli nyingi sana, na ingawa hilo halikuwa jambo baya, wakati mwingine hatukuwa tukijibu wateja wetu haraka jinsi ningelivyopenda. Kwangu mimi binafsi, huwa napenda kufanya kazi na wateja wetu wa uwekezaji. Lakini kwa sababu ya ratiba yangu, mteja aliyetarajiwa kuwekeza aliponipigia simu na kukabidhiwa kwangu ili niwasiliane naye kibinafsi, wakati mwingine sikuwa nikimpigia simu katika masaa 24 ya kwanza. Nia yangu ilikuwa njema, lakini sikuwa

nimefanikiwa kufanya hivyo.

Kama unavyojua, watu wanapouliza maswali, majibu kampuni itakayotoa ndiyo yatakayoisababisha kupata biashara. Wakati mwingine kuchelewa kumpigia mteja simu ili kujadili mahitaji yake ya kibinafsi ya uwekezaji kunaweza kumfanya akate tamaa. Anaweza kutafuta mtu mwingine ambaye yuko tayari kujibu maswali yake. Mambo mengi yanaweza kwenda kombo, lakini suluhisho ni kuwa na majibu mara tu mtu anapotaka kujua.

Kwa hiyo Bwana aliponipa maneno hayo matatu, nilijua maana yake. Nilipaswa kuwa na mtazamo tofauti ikiwa kweli nilitaka kupanda jukwaa lile la watu 10 waliokuwa bora katika biashara na kupokea bonasi yangu ya \$100,000. Ilibidi ninyakue kila fursa ilipojitokeza! Kwa hiyo nilibadilisha jinsi nilivyofanya mambo. Nilijiwekea sheria kwamba ikiwa mtu yeyote angeomba ushauri wa uwekezaji, ningempigia simu baada ya dakika chache, kama ingewezekana, na ningemtembelea mara moja. Wateja wangu wako kote nchini na uamuzi huu ungekuwa mgumu kutimiza. Lakini nilimaanisha. Nilimpigia simu meneja wa kampuni yangu na kumwambia kile ambacho Mungu alikuwa amesema na kumwambia awaambie wawakilishi wangu wote wawe na mtazamo huo huo wa kunyakua kila fursa ilipojitokeza. Mwaka ulipoisha, tulikuwa na zaidi ya dola milioni 11 kupitia kwa mchuuzi mmoja ambazo zilihitaajika ili kuwa katika kiwango cha wale wanabiashara 10 bora. Lakini juu ya hayo, pia tulikuwa tumepata biashara ya ziada ya mamilioni ya dola kupitia kwa wachuuzi wetu wengine.

Jambo lenye ufunuo mkubwa ndio hili. Hatukufanya mabadiliko mengine tofauti ila kuitikia haraka tu wakati tulipokuwa na mteja ambaye alitaka kuzungumza nasi. Wajua, Bwana alikuwa akisema kwamba sehemu maradufu, yaani raha ya Sabato, tayari ilikuwepo, tayari alikuwa ameitoa. Lakini sikuwa nimeiona!

Kwa hivyo hakuna sheria ya Ufalme ya jinsi ya kupata sehemu maradufu. Sehemu maradufu ipo wakati wote. Mungu daima hutoa riziki kwa kiwango cha sehemu maradufu.

## **MUNGU KAMWE HATUMI RIZIKI YA LEO TU. YEYE DAIMA HUKUMUISHA SEHEMU MARADUFU NAYO!**

Shida yetu ni kwamba hatuoni sehemu maradufu.

**Lakini tatizo kubwa zaidi ni kwamba kwa kawaida huwa hatujui ili kuweza kuitafuta!!!!**

Napenda kile Yesu alichosema, “Msiache chochote kipotee!” Mungu alituma sehemu yote, na anataka uipate. Alikasirika kwamba watu walitoka kwenda kutafuta mana siku ya saba wakati tayari alikuwa ameitoa. Alimkumbusha Musa kwamba alikuwa ameituma siku ya sita ili waweze kuinyakua na kufurahia pumziko la Sabato. Kimsingi, alikuwa akiwaambia, “Sabato si Yangu, ila ni yenu. Ndiyo maana nikakutumia sehemu maradufu.” Ni kama unaweza kusikia Yesu akisema maneno hayo hayo. “Jamani chukueni vipande hivyo, ili mweze kupata kila kitu. Mungu aliwatumia kila kitu ili mchukue na kufurahia sehemu maradufu, na kupata pumziko.”

Yesu alipowalisha wale wanaume 5,000 kwa mikate mitano na samaki wawili, wanafunzi hawakuona vipande hivyo, wala hawakuwa wakivitafuta. Lakini Yesu aliwaambia waviokote ili mavuno yasiptee. Leo Roho Mtakatifu anapaswa kutusaidia kuwa na mtazamo wa kuwa na zaidi ya kile kinachoridhisha ili tuweze kunyakua sehemu maradufu. Atatuonyesha mambo tusingiyoaona ikiwa tutamuuliza. Jambo muhimu ambalo natumai umejifunza hadi sasa ni kwamba tayari umepewa sehemu maradufu; unahitaji kuinyakua tu.

Shetani anachukia sehemu maradufu kwa sababu ndiyo njia PEKEE ya kutoroka kutoka kwa mfumo wa laana ya dunia, wa kazi yenye dhiki na kutokwa jasho. Anaweza kujaribu kuwasadikisha Wakristo kwamba kufanya kazi nyingi ili waweze kujiendeleza na kulipa bili zao tu, ni jambo zuri. Lakini Mkristo aliye na pesa za kusaidia kazi ya Ufalme wa Mungu na anayeishi bila woga na wasiwasi kifedha—sasa huyo ndiye shetani anapenda kuwekea viziwi. Kusudi la Shetani ni kukufanya uwe masikini siku zote za maisha yako na uwe mtumwa wa maisha duni yasiyo na ushawishi wowote. Pesa ni ushawishi! Shetani hakika angependa kukuzuia usipate baraka za Mungu. Ndiyo maana ninachotaka kukuambia sasa ni muhimu sana kwako kuelewa.

**Sehemu maradufu huwa imefichwa!**

Sawa, sasa ni wakati wa kuondoa lawama kutoka kwa wanafunzi wa Yesu. Kulikuwa na sababu iliyowafanya wasione wingi wa riziki hiyo. Naam, kwa kweli, kama tumeshasema, hawakuwa wakiitafuta, lakini kulikuwa na sababu nyingine. Kwa kawaida huwa hatukusanyi mabaki! Yaani, akilini mwao, mikate na vipande vya samaki vilivyokuwa vimetapakaa vilikuwa mabaki tu.

Kwa nini sarafu ambayo Petro alihitaji kulipia kodi ilikuwa imefichwa mdomoni mwa samaki? Ni nani angewahi kufikiria kutafuta hapo? Ni nani

**KUSUDI LA SHETANI  
NI KUKUFANYA UWE  
MASIKINI SIKU ZOTE  
ZA MAISHA YAKO NA  
UWE MTUMWA WA  
MAISHA DUNI YASIYO NA  
USHAWISHI WOWOTE.**

angefikiri kwamba neno la rabi mmoja lingewafanya wavuvi wa kitaalamu wenye mashua mbili ambao walikuwa wamevua usiku kucha na kukosa kupata chochote, waweze kuvua idadi kubwa ya samaki ambayo hawakuwa wamevua maisha yao yote? Ni nani angefikiri kwamba yule mwanamke katika 2 Wafalme 4 ambaye hakuwa na pesa, wala chochote nyumbani kwake ila mafuta kidogo tu, na ambaye

alikuwa karibu kufilisika kabisa angekuwa na mafuta mengi kiasi kwamba yalilipia madeni yake yote na kumtoa kwa maisha ya madeni? Hakuna mtu. Ni nani angefikiri kwamba Gary Keese, ambaye alihitimu katika kiwango cha chini kabisa katika darasa lake, angekuwa milionea leo na angezungumza na maelfu ya watu duniani kote kila siku? Hakuna mtu! Katika hadithi hizi zote, Mungu alitumia yasiyotarajiwa kubadili hali iliyokuwepo.

Ikiwa wingi wa riziki, yaani sehemu maradufu ingekuwa dhahiri hadharani tu, Shetani angeiona na angejaribu kuizuia na kuiiba. Hii ndiyo sababu Mungu huwa haonyeshi hazina Yake waziwazi. Huwa imefichwa. Shetani anachukia unapotosheleka na kufurahia riziki, na anachukia hata zaidi unapovuka na kuingia katika utele na pumziko la Sabato.

Acha nikuonyeshe jambo unalohitaji kuelewa kuhusu jinsi Mungu anavyofanya kazi katika ulimwengu.

*Bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliazimu tangu milele, kwa utukufu wetu; ambayo wenye kuitawala dunia hii hawaijui hata mmoja; maana kama wangelijua, wasingalimsulibisha Bwana wa utukufu.*

— 1 Wakorintho 2:7-8

Kifungu hiki kinatuonyesha wazi kwamba kama Shetani angejua mpango wa Mungu, angebadilisha mbinu! Hii ndiyo sababu Mungu hufanya kazi kwa siri. Shetani huingilia jambo lolote lililo wazi. Utele wa riziki yako haufai kuwekwa wazi hadi wakati utakapounyakua au kuuvuna kwa sababu hiyo hiyo. Nina msembo ambao nimekuwa nikisema kwa miaka mingi. Hazina ya Mungu imefichwa, sio kwamba usiipate bali ili uweze kuipata wewe pekee.

### **Imefichwa *kutoka kwako kwa ajili yako!***

Watu wengi huniambia kwamba wanatamani Mungu asingoje hadi dakika ya mwisho kabla ya kuachilia majibu Yake. Lakini rafiki yangu, Mungu hana woga. Anajua wakati bili inafaa kulipwa, na ni kwa faida yako kwamba Mungu asionyeshe mkono Wake mapema sana asije akaingilia Shetani.

*Nami nitakupa hazina za gizani, na mali zilizofichwa za mahali pa siri, upate kujua ya kuwa mimi ni Bwana, nikuitaye kwa jina lako, naam, Mungu wa Israeli.*

— Isaya 45:3

Mali zilizofichwa mahali pa siri? Naam, hili ni jambo bora kuliko filamu nzuri ya Hollywood. Hebu nikupe mfano wa jinsi Mungu alivyonisaidia kunyakua sehemu maradufu katika biashara yangu. Miaka mingi iliyopita, nilikuwa nimeketi chini nikitazama taarifa yangu ya faida na hasara ya mwaka mzima katika kampuni yangu ya huduma za kifedha. Ingawa nilikuwa nimeridhika maishani—sikuwa na madeni tena na nilikuwa na pesa kwa benki—nilijua kulikuwa na mambo zaidi. Niliona miradi mingi sana katika Ufalme ambayo nilitaka kufadhili, mambo mengi sana ya kufanya, na yote yaligharimu pesa.

Nilipokuwa nikiomba juu ya jambo hilo, Bwana alianza kunizungumzia kuhusu neno *vipande*. Mwanzoni, sikuelewa alichokuwa akisema, lakini kadiri nilivyosali juu yake na kusikiliza, nilipata ufahamu. Vipande, kama tulivyosoma katika ile hadithi vilipuuzwa. Thamani yao ilionwa kuwa ya chini—kwa sababu ya nguvu zilizohitajika ili kuvinyakua maana vilionwa kama vitu visivyo na thamani au thamani yao ilitokana na mfumo wa thamani uliopitwa na wakati. Au labda, mtazamo wao mbaya na mdogo wa jinsi ya kuvitumia ulipunguza ufahamu wao wa uwezekano wa thamani yao kuongezeka, jambo ambalo lilikuwa kinyume na mtazamo wao wakati huo.



Nina hakika mara nyingi umesikia watu wakisema hivi, “Hivi ndivyo tumekuwa tukifanya kila wakati.” Naam, lakini kuna uwezekano kwamba labda sehemu maradufu haitakuja kwa njia hiyo.

Nilipochunguza taarifa za watu, Mungu alifungua macho yangu kuona vipande vingi nilivyokuwa nikiacha mezani ambavyo nilipaswa kukusanya. Moja ya vipaumbele tunavyofanya na wateja wote ni kufanya wasifu kamili wa taarifa zao ili kuona ni mali gani wanaweza kuwa nayo pamoja na madeni yao. Kisha tunafanya uchanganuzi kutafuta pesa zozote tunazoweza kuokoa ili kulipa madeni. Bila shaka, tunaorodhesha hali zao za rehani na kiwango cha riba, tukijumuisha masharti ya mkopo kwenye taarifa zao. Wakati huo, tulikuwa pia tukiwashauri wateja wetu kutumia nyumba zao kuchukua mikopo mipya kutoka kwa kampuni zao za rehani na kutumia pesa hizo kulipa madeni ya kadi za mikopo ambazo zina riba ya juu sana, na hivyo kupunguza kiwango chao cha riba za kadi kutoka kiwango cha kawaida cha 21% hadi kiwango cha 6%. Akiba iliyotoka kwa kufanya hivyo iliokoa familia ya wastani kiasi cha \$500 hadi \$600 kila mwezi. Hali hii ilipojidhihirisha, tuliwarudisha wateja wetu kwenye benki zao tena kuomba mikopo ya kibinafsi ambayo wangetumia kumaliza madeni ya kadi za mikopo.

Nilipokuwa nikichunguza taarifa yangu, Roho Mtakatifu alinielekeza kwa suala hili la rehani. “Mbona usishughulikie kazi hiyo ya rehani?” Nilipokuwa nikitafakari hilo, kwa kweli niliona lilikuwa na maana. Tayari tulikuwa na imani ya wateja; tayari tulikuwa na taarifa zao; na pia, sisi ndio tulikuwa tukipendekeza kwamba wafadhili upya madeni yao.

Kushughulikia upande huu wa biashara kungehitaji nijifunze biashara mpya kabisa, nipite mafundisho na nipewe leseni, na mengine mengi. Sikuwa na wakati wa kufanya yote hayo. Lakini nilipoendelea kuomba kuhusu hilo, Bwana alinisisitizia njia yote mwingine wa kuanzisha na kuendesha kampuni yangu ya rehani, jambo ambalo nilifanya. Kushughulikia kazi hiyo ya rehani sisi wenyewe katika mwaka wa kwanza pekee kulileta \$160,000 za ziada katika mapato halisi. Hizi zilikuwa pesa ambazo nisingekuwa nazo kama singemruhusu Roho Mtakatifu anionyeshe kipande kilichokuwa mbele yangu moja kwa moja lakini sikuwa ninakiona.

Niliendelea kunyakua vitu vingi zaidi ambavyo vilikuwa vipande Roho Mtakatifu alikuwa akinionyesha. Kipande ambacho nilikuwa nikipuuza—kwa sababu ya mawazo yangu ya awali ambayo nilikuwa nimejifunza au kusikia watu wengine wakisema kwamba biashara hiyo haikuwa na thamani—kilileta mafanikio makubwa kwetu. Hatimaye nilipoketi na

kuchunguza, niligundua kwamba taarifa zote nilizosikia kuhusu biashara hii hazikuwa sahihi na kwa kweli ilikuwa inafaa sana kwa kampuni yetu. Kipande hiki kimeleta mapato zaidi kuliko mfumo wangu wa kimsingi wa biashara. Kimeleta mamilioni ya dola. Kilikuwa kipande chenye mamilioni na mamilioni ya dola!

Kwa hivyo acha nikwambie wazi kabisa. Sehemu maradufu hunyakuliwa kwa njia ya ufunuo! Ufunuo ni kitu ambacho Roho Mtakatifu anakuonyesha ambacho usingelijua peke yako. Ni wakati Roho Mtakatifu anakufunulia au kufungua macho yako kuona jambo ambalo wewe mwenyewe hukulijua. Jambo hili linaitwa kupokea maarifa ya ufunuo.

### **Ufunuo ndio ufunguo wa sehemu maradufu!**

Kisha watu huniuliza, “Je, nitamsikiaje Roho Mtakatifu? Nitasikiaje jinsi ya kunyakua dhana na fursa hizi ambazo zimefichwa?” Maswali mazuri haya. Sina muda katika kitabu hiki kueleza kwa kina kuhusu kusikia sauti ya Mungu. Kwa hiyo nitakuelekeza kwenye kitabu kingine nilichoandika kiiitwacho, *Ubatizo wa Roho Mtakatifu*. Unaweza kukinunua kutoka Amazon au tovuti yetu. Katika kitabu hicho, utapata habari zaidi kuhusu jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi ili kutufunulia mipango ya Mungu iliyofichwa, ili tuweze kufanikiwa papa hapa katika ulimwengu, chini ya pua la Shetani; na hakuna anachoweza kufanya kuhusu hilo. Lakini ili kukuelekeza kwenye njia ifaayo, hebu tuangalie **1 Wakorintho 14:2**.

*Maana yeye anenaye kwa lugha, hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake.*

**Mstari wa 4** unasema,

*Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake.*

Neno kujenga maana yake ni kuleta mafundisho au ufahamu. Nahitaji hilo na wewe pia. Wakati Biblia inazungumza hapa kuhusu kunena kwa lugha au, kama Paulo alivyoeleza kuhusu kuomba katika Roho, nataka kukutia moyo—usijali umesikia nini kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu, labda mtu fulani alikuambia kwamba jambo hilo liliisha na mitume au kwamba hiyo ni kazi ya shetani—soma Biblia yako! Kuomba katika Roho ni Roho

Mtakatifu anayeomba kupitia kwako katika ulimwengu ili kutimiza mapenzi Yake bila ufahamu wa shetani. Kuomba katika Roho ni ufunguo muhimu katika kusikia ufunuo kutoka mbinguni, na ninakuhimiza ujifunze kile nimesema. Na ikiwa una maswali, pata kitabu changu na najua kitakusaidia kupokea ufahamu zaidi kuhusu kazi hii ya ajabu ya Roho Mtakatifu maishani mwetu.

Ninataka kuhitimisha kitabu hiki na mistari miwili ya Maandiko ambayo inajumlisha sura hii.

*Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.*

— Waefeso 3:20-21

Huwezi kamwe kuomba kupokea kitu ambacho hujawahi kufikiria. Kwa sasa ninamiliki ndege mbili, ndege ndogo zaidi ninayoendesha wakati ninataka kujifurahisha na ndege yangu ya biashara ninayosafiria ninapotaka kwenda kwa nchi yoyote. Nilipokuwa nikifikiria kununua ndege yangu ya biashara, nilishtushwa na bei. Hakuna ndege yenye bei nafuu! Nilianza kubadili mawazo na kufikiria, “Ninaweza kukaa bila ndege ya biashara. Kwa kuwa hii ni pesa nyingi sana.” Lakini kila wiki nilikuwa nikisafiri kwa ndege za abiria, na kuna mwezi nilisafiri mara 23. Hilo lilikuwa linachosha. Ndio, nilikuwa na riziki ya kutosha. Safari zangu zote za ndege zilikuwa zikilipiwa; wala hakukuwa na shida ya pesa ya kuzilipia. Lakini safari zangu za ndege za abiria hazikuwa na utulivu. Wakati mwingine safari zilikuwa zikighairiwa au kuchelewa, na hilo lilikuwa tatizo kubwa. Hili halikuwa pumziko la Sabato nililohitaji.

Hatimaye, nilikubali kwamba nilikuwa nimemwekea Mungu mipaka katika hilo. Yeye ni Mungu wa sehemu maradufu. Nasikitika kusema kwamba Mimi na Drenda tulisita kununua ndege kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hatimaye, Mungu alielekeza mawazo yetu kwa ndege fulani kisha akatuambia alikuwa amejaribu kutupea ndege hiyo kwa miaka miwili! Tulutubu na tukafanya uamuzi wetu. Tulitoa matoleo yetu ya kifedha kama mbegu kwa ajili ya ndege halisi ya safari za kibiashara ambayo tulitaka na tulihitaji; na tulipofanya hivyo, kabla ya miezi miwili kuisha tulikuwa nayo. Wakati huohuo, Mungu alinipa maarifa na kibali kwa mikataba fulani ya biashara, na pesa zilikuwepo nilipozihitaji.

Kweli, Mungu ni Mungu wa sehemu maradufu. Je, hilo lilileta tofauti? Naam, tofauti maishani mwangu katika kuweza kutumia ndege yangu mwenyewe unapolinganisha na kusafiri kwa ndege ya abiria ni kama kulinganisha kuendesha pikipiki yako au kuendesha gari lako umbali wa maili 50 kuhudhuria mkutano ulio nao. Kweli?! Na Mungu alikuwa akijaribu kuniletea suluhu kwa miaka miwili lakini nilikuwa nimeridhika na kukaa kipofu kwa sehemu maradufu ambayo Mungu alikuwa ameniandalia tayari. Nilihita tu kuiona.

Labda unaendesha gari ambalo linahitaji sana kufanyiwa marekebisho kiasi kwamba unaomba liwake unapoamka. Acha kuangalia akaunti yako ya benki iliyo tupu na kufanya maamuzi ya kuishi kulingana na hilo. Badala yake, acha Mungu wa sehemu maradufu akuonyeshe vipande vipande, mambo yaliyofichika ambayo unahitaji kujua ili uwe huru na ufurahie amani na pumziko la Sabato. Atakupa mpango na kukuonyesha jinsi ya kuutekeleza ikiwa utamwomba tu. Na kama vile Yesu alivyosema, “Usiache chochote kipotee!” Sehemu maradufu tayari imetolewa kwa ajili yako!

*Basi, imesalia raha ya sabato kwa watu wa Mungu. Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake.*

— Waebrania 4:9-10

# MAPINDUZI YAKO YA KIFEDHA

## Nguvu ya Kupumzika

### Je Umechoka?

**Umechoka kukimbia mbio za panya?  
Umechoka kuhisi kwamba umekwama?  
Umechoka kuwa na wasiwasi?  
Umechoka na kutokuwa na furaha?**

### Huna budi kuishi hivyo tena.

Jiunge na Gary Keesee katika safari hii ya ajabu ya ugunduzi, na UJIFUNZE MFUMO MPYA— ambao utabadilisha maisha yako kabisa, kama ulivyobadili yake baada ya miaka tisa mirefu ya kuishi katika *uchovu* na kukata tamaa kifedha, kimwili, na kihisia.

Gundua:

1. Jinsi kila kitu kilivyobadilika katika maisha ya Gary—jinsi alivyotoka katika hali ya kukata tamaa kabisa kifedha na kimwili, na kuwa mwenye afya na mzima, kulipia magari yake pesa taslimu, kujenga nyumba yake bila madeni, kuanzisha kampuni nyingi, na kufundisha mamia ya maelfu ya watu jinsi ya kuishi maisha ya Ufalme ... jinsi ya *kuishi maisha ya pumziko*.
2. Jinsi kila kitu kinavyoweza kubadilika maishani MWAKO pia—jinsi WEWE unavyoweza kuishi maisha ya pumziko.

Hata kama kila mtu unayemjua anaishi maisha ya uchovu na kukimbia hapa na pale kwa bidii ili kuishi, sio lazima uishi hivyo.

Kwa kuelewa kanuni muhimu ya Pumziko la Sabato, utaweza kuona matokeo halisi katika maisha yako. Utaweza kuishi mahali ambapo mahitaji yako yanakidhiwa; huku ukiwa huru kutoka kwa mbio za panya; huru kupata na kufanikiwa katika kusudi lako na shauku yako, mahali ambapo utafanikishwa wala sio kunusurika; na kuonyesha watu wa ulimwengu matokeo tofauti na yale ambayo wamezoea kuona kila wakati.

Usiendelee kukwama wala kuishi katika uchovu.

Gundua njia mpya ya kuishi!



Gary Keesee ni mwandishi, mmnenaji, mjasiriamali, mtaalamu wa fedha, na mchungaji ambaye ana shauku ya kusaidia watu kuwa washindi maishani, hasa katika maeneo ya imani, familia, na fedha. Gary na mkewe, Drenda, wameanzisha biashara kadhaa zilizo na fanaka, na ndio waanzilishi wa huduma iitwayo Faith Life Now, ambayo ina vipindi viwili vya televisheni— *Fixing the Money Thing* na *Drenda*, kongamano kote ulimwenguni, na rasilimali za vitendo. Wao pia ni wachungaji wa Kanisa la Faith Life karibu na Columbus, Ohio.

P. O. Box 779, New ALBANY, OH 43054, USA